ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 2 Julai, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe hati mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 88

Ujenzi wa Barabara ya Fuoni Kibondeni

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu) – Aliuliza:-

Wananchi wa Fuoni Kibondeni wana kilio cha ubovu wa barabara yao kwa miaka mingi. Ubovu huo unachangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma ari ya maendeleo ya wananchi hao pamoja na kukwaza shughuli za kiuchumi na za kijamii.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hiyo kutoka Fuoni Sokoni hadi Hospitali ya Kibondeni.

(b) Kama kwa sasa Serikali haina mpango wowote. Je, kwa dharura haiwezi angalau kuziba mashimo katika sehemu ambazo ni mbaya zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-
Barabara ya Fuoni- Kibondeni ilifanyiwa uchambuzi yakinifu (*Feasibility Study*) na ni miongoni mwa barabara zilizopelekewa maombi yake kupitia Mfuko wa Akaunti ya Changamoto ya Milenia (*MCC*) ambayo kwa bahati mbaya mradi huu hatukufanikiwa kwa upande wa Unguja. Hata hivyo, wizara yangu itaangalia namna bora ya utekelezaji wa mradi huu hali itakapo ruhusu japo kwa kuanzia Fuoni Polisi hadi Fuoni Kibondeni.

Mhe. Spika, barabara hii pia hivi sasa ambayo ina urefu wa kilomita 6.7 imeshaingizwa katika ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015. Kwa hivyo, matarajio yetu ni kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kwa kuwa malengo ya kuitengeneza barabara hii ni ya muda mrefu kuanzia mwaka 2010-2011. Je, serikali haina mpango wowote wa kuifanyia matengenezo ya dharura ili wananchi wale wakaondokana na tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni lengo la serikali kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo ziko katika hali mbaya zinafanyiwa angalau matengenezo ya dharura, lakini kuna bahati njema ni kwamba hivi sasa kwa bahati nzuri kuna mfuko wa majimbo umeshaanza kutolewa. Kwa hivyo, tunaomba viongozi wa jimbo aje tushirikiane kuifanyia matengenezo ya dharura barabara hii.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, ahsante naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri miezi mitatu iliyopita nilikuhoji sana kuhusu njia ya Bububu, njia hii ilipobomolewa tukaambiwa inakwangurwa lakini imejengwa nusu tu mpaka pale Mkapa Road haijamalizwa hali ya kuwa mashimo bado yapo yanasumbua sana watumiaji wa barabara hiyo. Nilipoangalia katika mfuko wa barabara niligundua kwamba barabara ile imeshalipiwa tangu mwaka 2008.

a) Je, Mhe. Waziri unatwambiaje sisi tunaokaaa maeneo ya kule njia ile itamalizika lini.

b) Njia kutoka Amani kwenda mpaka pale Jeshini Mkapa Road siku hizi ina ajali nyingi sana kwa sababu gari ni nyingi na barabara ni nyembamba. Je, kuna mpango gani wa kuongeza ile barabara ya pili ambapo ilikusudiwa pale awali.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba fedha ya kufanyia matengenezo ya barabara ya Kinazini-Bububu ukarabati ule zipo na lengo letu ni kufanya ukarabati mpaka Bububu kuna sehemu kama tatu bado hatujazifanyia ukarabati lengo letu ni kuingia Chuo cha Utalii na kuweka lami, kuingia Ikulu ya Kibweni kuweka lami na kumalizia sehemu iliyobakia zile ambazo ni mbevu. Lakini Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba tunaifanya sehemu nyengine tunaziruka nyengine tunaziacha kwa sababu serikali ina mazungumzo na Serikali ya Japani kuianza upya ile barabara kutoka Malindi mpaka pale walipofika Wajapani mara ya kwanza.

Kwa hivyo, hatutaki kugharamia sana tukapoteza fedha nyingi zaidi, tumefanya zile za dharura ili watu waweze kupita kwa usalama vizuri.
Mhe. Spika, kuhusu barabara ya Amani-Mtoni ni kwamba nafurahi kuliarifu Baraza hili kwamba ahadi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa fedha kwa barabara ya upande wa pili tayari fedha hizo zipo na tunatarajia kuijenga kupitia serikali yetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, barabara inayotoka Fuoni-Sokoni hadi Hospitali ya Fuoni inahudumia wagonjwa mbali mbali wakiwemo mama wajawazito na watoto na mara nyingi sisi katika kamati yetu tumepokea malalamiko mengi kwamba wagonjwa hao niliowataja huwa wanapata shida ya usafiri kufika hospitali.

Je, kwa kuwa suala hili Mhe. Waziri alisema kwamba yuko tayari uongozi wa jimbo washirikiane katika kuanzisha matengenezo ya dharura, kama atatokea mwanachama wa Chama cha Mapinduzi ambaye ni mkereketwa wa maendeleo hasa tukizingatia kwamba mama mjamzito na mtoto anaheshima yake, Mhe. Waziri atatoa ushauri gani juu ya suala hilo ili watengeneze pamoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, inaonesha kama Jimbo la Fuoni halina mwenyewe mimi najua Jimbo la Fuoni lina viongozi na wizara iko tayari kushirikiana na viongozi wa Jimbo la Fuoni na kama kuna mkereketwa ende kwa viongozi wa Jimbo la Fuoni tuko tayari kutengeneza kama ambavyo tunatengeneza barabara zote kwa kushirikiana na viongozi wa majimbo ikiwemo ya Kwahani na nyengine za Wilaya ya Mjini.

Nam. 80

Uimarishaji wa Biashara Zanzibar

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Biashara ni muhimili wa uchumi katika nchi nyingi ulimwenguni hasa nchi za visiwa kama vyetu ambavyo vina upungufu wa raslimali.

(a) Kwa kuwa hali ya biashara katika Visiwa vyetu imepungua katika miaka ya karibuni na mchango wake kushuka kwa kiasi fulani, Serikali ina mkakati gani wa kujiimarisha na kurejesha hadhi ya biashara Zanzibar kwa lengo la kuongeza mchango wake katika uchumi wetu.

(b) Kwa kuwa biashara nzuri ni ile yenye uwiano baina ya usafirishaji na uingizaji na kwa kuwa biashara yetu imeelemea upande mmoja wa upokeaji zaidi kutoka nje, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha sekta ya uzalishaji ili kusaidia kuleta uwiano huo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, taarifa zinaonesha kwamba hali ya biashara inakuwa na kushuka katika kipindi cha miaka minne iliyopita kwa pande zote mbili uagiziaji na usafirishaji kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa usafirishaji mwaka 2006 tulisafirisha bidhaa zenye thamani ya sh.15.424 bilioni, 2007 kutokana na ujenzi wa bandari tulisafirisha bidhaa zenye thamani ya shilingi 968 milioni, mwaka 2008 bilioni 30.1 na mwaka 2009 bilioni 29.7. Kwa hivyo, hali ya usafirishaji inaonesha kupanda na kushuka. Kwa upande wa uagiziaji tumekuwa tukiagizia kama ifuatavyo:-

Mwaka 2006 bilioni 87.5, mwaka 2007 bilioni 107.6, mwaka 2008 bilioni 93.4 na mwaka 2009 bilioni 120.8. Aidha, meli kubwa za uletaji wa mizigo zimeongezeka kutoka 2 hadi 5 ambazo ni:-

- MASK LINE
- MC
- CMA CGM
- METRO SHIPPING

- EMIRATE SHIPPING

Vile vile Mhe. Spika, ujaji wa makontena yanayowasili Zanzibar yameongezeka kutoka makontena 600 kwa mwezi na kufikia 1200 kwa mwezi.

Mhe. Spika, suala kubwa hapa la kulifanyia kazi ni uwiano wa biashara kutoka uagiziaji na usafirishaji. Serikali katika kulifanyia kazi hilo imepitisha mkakati wa usafirishaji bidhaa wa mwaka 2009 pamoja na kutayarisha mpango kazi wa utekelezaji huo.

Katika kutekeleza mkakati huo, Serikali inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Upembuzi yakinifu wa kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Huru la Kiuchumi (*Special Economic Zone)* ambapo Wizara ya Fedha tayari wameshatenga fedha za kufanyia upembuzi yakinifu huo.

- Kuanzisha Uwanja wa Maonyesho ya Kiashara ya Kimataifa katika eneo la Fumba na kazi hii tayari imeanza kufanyiwa kazi

- Kuweka mfumo wa sheria na taasisi kwa ajili ya viwango vya biashara ili kumudu ushindani katika soko. Rasimu ya sheria tayari imeshatayarishwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kwa kuhakikisha kwamba Zanzibar inaendelea vizuri na biashara za kusafirisha na kuagiza, lakini kwa kuwa hivi sasa Mhe. Spika, kuanzia jana tarehe 1/07/2010 Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza rasmi kutumia soko moja la Afrika Mashariki na kwa kuzingati hayo Mhe. Spika, tunaamini kwamba hapa sasa hivi patakuwa na ushindani mkubwa wa biashara za kutoka na kuingia. Hivyo, sisi kwa wafanyabiashara wetu ni sehemu gani ambayo Mhe. Waziri ataielekeza wajitahidi angalau kutoa bidhaa na kusafirisha katika masoko hayo ili nchi ipate tija.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi itayozalisha kwa wingi ndio nchi ambayo itafaidika na soko lile, lakini vile vile nchi itakayofanya biashara ya bandari huru ndio nchi ambayo itafaidika na soko lile. Kama nilivyosema katika jibu mama kwamba sasa hivi Zanzibar tuna lengo hilo na tayari Wizara ya Fedha wameshatenga pesa ya kufanya upembuzi yakinifu ili kuifanya Zanzibar yote kuwa eneo huru la biashara.

Kwa hivyo, mkakati wetu katika Soko la Afrika Mashariki ni huo wa kufanya eneo huru.

Mhe. Spika, pia niwasihi tu wazalishaji wadogo wadogo wa humu ndani kuongeza uzalishaji ili kuweza kuuza katika soko hilo.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika swali mama kulikuwa na swali la sekta ya uzalishaji, ili kuziba nakisi ya usafirishaji na uuzaji mali lazima pawe na sekta ya uzalishaji. Je, wizara yako imejidhatiti na imejitayarisha vipi kukabiliana na changamoto hilo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwanza wizara yangu inajiandaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na katika kufanya hivyo tumefanya mapitio ya sheria nne za biashara. Sheria ya Biashara Mizani na Vipimo, Sheria ya Kumlinda Mtumiaji na Sheria moja nyengine imenipita kichwani, lakini tuna sheria nne ambazo tutazifanyia marekebisho.

Jengine ni huu mkakati mzima wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo huru la kiuchumi. Mhe. Spika, jengine ni kwamba tunafanya kazi pamoja na *Chember of Commerce* kwa upande wao kama jumuiya na wao wazungumze na wanachama wao katika sekta yao kuhakikisha kwamba wanazidisha uzalishaji. Kubwa zaidi wafanyabiashara wetu ambao tunao sasa hivi watoke kwenye sekta ya kuagiza na kuuza, waingie katika sekta ya viwanda (uzalishaji). Ahsante.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba kwa mujibu wa majibu yake katika swali la msingi ni kwamba usafirishaji wetu wa bidhaa nje umeongezeka katika baadhi ya miaka, na kwa mujibu wa alivyojibu ni kwamba miaka ile ambayo ameitaja ni ile miaka ambayo uzalishaji wa karafuu umekuwa mkubwa, na miaka ambayo uzalishaji wa karafuu umekuwa kidogo basi usafirishaji wetu wa bidhaa nao umekuwa nje.

a) Mhe. Spika, lakini kwa kuwa Mhe. Waziri wizara yake haionekani kama ina mpango wa maana wa kustawisha mikarafuu yenyewe, hatuoni kwamba huko tunakokwenda hali yetu ya usafirishaji wa bidhaa itakuwa mbaya zaidi ukitilia maanani kwamba mikarafuu inaendelea kufa.

b) Ile ahadi ya serikali kwamba biashara ya karafuu ingebinafsishwa imefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, wizara yangu inatoa mchango mkubwa kila mwaka kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kuhakikisha kwamba zao la karafuu linaimarishwa. Kwa hivyo, wizara yangu ingependa sana kuona kwamba zao la karafuu na mwani linaimarika ili tuweze kukuza ukubwa wetu wa usafirishaji.

Lakini kwa upande wa pili kuhusu ubinafsishaji wa zao la karafuu. Kama ninavyojibu kila siku kwamba haya ni mageuzi ya kiuchumi ambayo yanashughulikiwa na Kitengo cha Uchambuzi wa Sera za Uchumi ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa hivyo, nadhani Wizara ya Fedha na Uchumi watakuwa kwenye *position* nzuri kujibu suala hili.

Nam. 96

Stahiki za Waliokuwa Wafanyakazi wa Baa ya Kilimani

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Baa ya Kilimani ilikuwa ni miongoni mwa Miradi ya Shirika la Utalii, lakini eneo hilo limerejeshwa Serikalini kwa kazi nyingine na kupelekea Wafanyakazi wa hapo wapatao ishirini (20) kutokulipwa baadhi ya stahiki zao tangu lilipochukuliwa eneo hilo. Wafanyakazi hao wanadai jumla ya Tsh 42, 237,439/-. Kati ya fedha hizo Tsh 2,161,187/- ni za mchango wa *ZSSF* na Tsh 40,076,252 za Kiinua Mgongo.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inachukua jitihada gani hukakikisha wafanyakazi hao wanapata haki yao.

(b) Je, wale ambao shirika lililazimika kuwaachisha kazi wamepatiwa sehemu nyengine ya kufanya kazi.

(c) Kama bado je Serikali ina mpango gani.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.96 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, waliokuwa wafanyakazi wa Kilimani Bar ilibidi wastaafishwe ili kupisha eneo hilo kutumika kwa matumizi mengine ya Serikali.
Aidha wafanyakazi hao kwa mujibu wa sheria walistahiki kulipwa malipo ya aina nne:-

- Notisi ya miezi mitatu
- *Severance Pay*
- Malipo ya kiinua mgongo lakini pia waliowajibika kulipiwa malipo yao ndani ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).
- Kusawazishiwa malimbikizo yote yanayodaiwa na *ZSSF*

Malipo yote haya tayari yameshalipwa na Wizara ya Fedha, isipokuwa deni la *ZSSF* ambalo tulikuwa tunavutana baina ya wizara yetu Shirika la Utalii pamoja na Wizara ya Fedha. Wakati wa kufanya malipo haya Shirika la Utalii waliiomba Wizara ya Fedha waingize deni hili ili lilipwe kule, lakini Wizara ya Fedha waliwajibisha shirika kwa sababu malipo haya ilibidi yalipwe nyuma kwa hiyo shirika lilipo malipo hayo.

Mhe. Spika, wizara yangu imechukua hatua ya kuliwezesha shirika waingiza pesa hii katika Mfuko wa ZSSF na kiasi cha fedha zilizokuwa zikidaiwa ni milioni mbili laki moja sitini na moja mia moja thamanini na saba. Kwa hivyo, kazi hiyo tayari wizara yangu imeshaichukulia hatua.

Kuhusu kuwapangia kazi sehemu nyengine kama nilivyojibu awali kwamba wafanyakazi wa eneo lile walistaafishwa kwa hiyo hakukuwa na haja tena ya kuwapangia kazi sehemu nyengine bali walijitafutia wenyewe.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba fedha za ZSSF bado wafanyakazi hawa hawajalipwa, tunavyofahamu sisi sheria ya ZSSF kwamba hizi fedha zinakatwa na zinakuwepo katika mfuko.

a) Je, inakuwaje hawa wanafukuzwa kazi halafu fedha hizo wanazikosa.

b) Hivi sasa katika jengo hilo la Kilimani Bar naona kumejengwa ukuta na linatengenezwa. Je, jengo hilo amepewa nani.

c) Tulisikia kwamba wenzetu hawa Shirika la Utalii walikuwa wanazalisha pale Kilimani Bar na kwa kuwa wameondoshwa ghafla waliahidiwa kwamba watapewa pesa ili wajishikize wasidorore kwenye kazi zao. Je, ahadi hiyo pia ilitekelezwa.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba malipo haya yalitakiwa kukatwa kwenye mishahara na kuwasilishwa

ZSSF, lakini shirika halikuwa likifanya hivyo kutokana na ugumu wa kiuchumi waliokuwa nao kwa wakati huo, ndio maana Wizara ya Fedha walikataa kulipa malipo haya na kuwataka shirika walipe wenyewe kwa sababu walifanya makosa huko nyuma. Kama nilivyosema kwamba wizara imeshawawezesha shirika kufanya kazi hiyo.
Mhe. Spika, kuhusu eneo lile amepewa nani ni kwamba mali zote za serikali ziko katika Kitengo cha Mitaji ya Umma ndani ya Wizara ya Fedha. Lilipotakiwa eneo lile sisi tulilikabidhi katika Kitengo cha Mitaji ya Umma na wao ndio waliopanga aliyepewa wa kwanza na aliyepewa wa pili. Kwa hivyo, sitakuwa kwenye nafasi ya kuweza kujibu sasa hivi liko mikononi kwa nani.

Kuhusu fedha za kujishikiza Wizara ya Fedha wametoa pesa hizi lakini kwa awamu, shirika limepata awamu ya kwanza na tunasubiri wapewe awamu nyengine.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa eneo la Kilimani Bar ambalo lilikuwa linamilikiwa na Shirika la Utalii lilichukuliwa kwa lengo la kuwapa watu wa *ZRB* kujenga jengo lao pale na kwa kuwa serikali baada ya kulichukua eneo hilo la Kilimani liliwataka Shirika la Utalii kupeleka mapendekezo yao serikali nini wafanyiwe. Pia kwa kuwa shirika lilipeleka maombi ya kupatiwa fedha kiasi cha shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kuhudumia ikiwepo hayo masuala ya ulipaji wa Mfuko wa Hifadhi ZSSF na mambo mengine.

a) Je, Mhe. Spika, ni kwa nini hadi leo serikali haijatoa fedha hizo ili kuwawezesha watu wa Shirika la Utalii kufanya hayo malipo ya wafanyakazi ambao wameondoka. Pia ni kwa nini baada ya ZRB kulirejesha eneo hilo serikalini kwa maana ya kwamba halikukidhi haja ya ujenzi wao.

b) Kwa nini eneo lile wasirejeshewe wenyewe watu wa Shirika la Utalii wakati wao tayari wameshalipangia mipango ya kujenga ukumbi pale wa burudani.

c) Pamoja na kuwa Mhe. Waziri ameeleza kwamba haelewi eneo hilo wamepewa nani lakini taarifa zilizopo ni kwamba wamepewa watu wa Idara ya Majenzi. Ni kwa nini wapewe watu wa Idara ya Majenzi wakati wao ndio wenye ardhi ambayo wanaweza kupata eneo jengine lolote kwa ajili ya kufanay shughuli zao.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, hii ni sawa sawa na mtu aliyepigwa na kimbunga ukenda ukamuuliza wewe kwa nini ulipigwa na kimbunga kwa sababu masuala yote haya mimi ndio mwenye hiyo

mali iliyochukuliwa, sasa ananiuliza mimi kwa nini hukulipwa, kwa nini hukurudishiwa, kwa nini kapewa mwengine. Mhe. Spika, kama nilivyojibu awali kwamba mambo yote haya ndani ya Kitengo cha Mitaji ya Umma ndani ya Wizara ya Fedha. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa suala la mshtukizo pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mhe. Waziri lakini nataka kusema tu kwamba kama serikali huwa tunakaa pamoja tunatizama maombi yaliyopo ya ardhi na uzito wa kazi. Tunakumbuka kweli hapo nyuma pale palikuwa Kilimani Bar lakini shughuli za bar kwa wakati huu kwa pale kidogo zimepitwa na wakati imebidi turekebishe hali na nafikiri kuanzia eneo lile pote pale naweza kusema ni kama pana maofisi ya maghorofa pale. Kwa hivyo, *management* ya Kilimani Bar ipo kama hawajafilisika na wako tayari na shughuli hiyo basi wairipoti serikali tutafanya mpango tutawapatia mahala pazuri kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba eneo husika wizara yake haikushirikishwa na Waziri wa Fedha amekiri kwamba eneo lile limechukuliwa lakini Kilimani Bar wanaweza wakapewa eneo jengine kama watahitaji, wote wawili watakubaliana na mimi kwamba ni kweli mali ya serikali kutoka bila ya utaratibu.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, unaposema limetoka bila ya utaratibu si kweli kama ninavyosema serikali wizara zimekaa na serikali ikakaa ikapanga. Sasa kusema bila ya utaratibu aa, na nimehakikisha kwamba hizo shughuli za Kilimani Baa zimepitwa na wakati kwa sehemu ile.

Mhe. Salmin Awadh Salmin alisema wazi kwamba kweli ilichukuliwa ardhi wakapewa *ZRB. ZRB* ikaonekana hapakidhi kwa kazi yao wakaliacha, sasa wamepewa wenye ardhi na watapasanifu vizuri. Wenyewe wanaojua mambo ya majenzi watakuwepo kufanya kazi wanayoilenga. Sio kama wamepewa kienyeji tu aa, kwa utaratibu, serikali imekaa imepanga.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa baraza lako likae katika Kamati ya Matumizi kupokea kujadili, kuchangia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kazi za maendeleo na kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya nzuri na kukutana tena mwaka huu katika Baraza lako hili na kuniwezesha kutoa hotuba yangu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kumpongeza Mhe. Dr. Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza nchi yetu vizuri na kwa uadilifu katika kipindi chake cha miaka 10 ya uongozi na kuiacha nchi yetu katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Spika, shukrani pia ziwaendee Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi Mhe. Ali Juma Shamhuna kwa utendaji wao wa kufuatilia na kutoa ushauri ili kufanikisha kupatikana mafanikio ya utendaji wa majukumu ya mawizara na taasisi zote za serikali. Pia kwa kumsaidia Mhe. Rais, kumshauri kwa uadilifu mkubwa uliomsaidia kuiongoza nchi yetu vizuri.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukushuru wewe binafsi na wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili kufuatana na Sheria, Kanuni za Baraza zikichangiwa na hekima na uvumulivu ulionao na watendaji wako.

Mhe. Spika, sitaki kuwa mchoyo wa fadhila kwa kutowashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, hususan Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali, ambao kwa namna moja au nyengine wamefanikisha kwa kiasi kikubwa na kwa ufanisi utekelezaji wa majukumu na malengo ya wizara yangu. Hii imetokana na michango mizuri na ushauri walioutoa wakiwa ndani na nje ya Baraza.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na wasaidizi wangu wote ndani ya wizara, nawapongeza kwa dhati kabisa wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa juhudi, bidii, ustahamilivu na kujituma katika kufanikisha kutoa huduma nzuri kwa wananchi wa Zanzibar, pamoja na hali ngumu ya utendaji kutokana na mazingira yaliyowazunguka.

Mhe. Spika, amani na mshikamano ni nyenzo muhimu katika kuendesha nchi yetu kwa amani na usalama. Hivyo basi, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*)

Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa mazungumzo yao ya kutafuta amani Zanzibar yaliyofanyika Ikulu Zanzibar tarehe 5 Novemba, 2009.

Hii ni ishara tosha ya jinsi Wazanzibari wanavyoweza kutafuta ufumbuzi na suluhisho la kudumu katika changamoto za kisiasa zinazotukabili. Mazungumzo yao yameonesha mwelekeo na maelewano ya kisiasa Zanzibar. Hivyo nachukua fursa hii adhimu kuwapongeza, kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu, kuwazidishia kheri, baraka na hekima. Aidha, ni matumaini yangu kwamba wananchi wote wa Zanzibar watalipokea suala hili kwa furaha kubwa kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kuwashukuru na kuwapongeza wahusika wote, naomba uniruhusu nitoe maelezo, utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MALENGO KWA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, majukumu na malengo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutekelezwa na kukamilishwa kwa mashirikiano makubwa ya Idara zote zinazounda wizara hii zikisimamiwa na Wakurugenzi wa Idara, Mkurugenzi Mkuu, Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Waziri mwenyewe. Idara hizo ni:-

1. Idara ya Mipango na Sera.
2. Idara ya Kinga na Elimu ya Afya.
3. Idara ya Tiba.
4. Idara ya Ustawi wa Jamii.
5. Idara ya Afya ya Jamii.
6. Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.
7. Idara ya Kupambana na Madawa ya Kulevya.
8. Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na
9. Afisi ya Mdhamini wa Afya Pemba.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera ni idara mama katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Idara hii ina majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya, kuandaa miongozo mbali mbali pamoja na mipango ya muda mrefu na mfupi. Aidha, idara ina jukumu la kusimamia upatikanaji na utunzaji wa fedha za wizara, uajiri na haki za wafanyakazi pamoja na kusimamia maslahi yao, kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa wizara na kutunza takwimu.

Mhe. Spika, sasa naomba nielezee utekelezaji wa malengo ya mwaka 2009/2010 ya idara hii kupitia vitengo vyake mbali mbali.

KITENGO CHA MIPANGO, SERA NA SHERIA

Mhe. Spika, Kitengo cha Mipango, Sera na sheria kina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya pamoja na mpango mkakati wa wizara, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa wizara wa kila mwaka, kusimamia miradi ya Wizara pamoja na kuandaa mpango wa muda wa kati wa matumizi – *Medium Term Expenditure Framework* (*MTEF*) na kuandaa Hotuba ya Bajeti ya Wizara. Aidha, kitengo kina jukumu la kufanya usimamizi wa vifaa na mali za serikali zilizomo ndani ya Wizara hii. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele namba 2.1.2 – 2.1.8.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo hiki kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini katika masuala ya jinsia kwa watendaji wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
b) Kutoa mafunzo ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
c) Kutoa mafunzo juu ya kuzingatia masuala ya Haki za Binadamu katika Mipango yote ya Wizara.
d) Kutoa ushauri wa kisheria kwa masuala yote ya kisheria yanayohusiana na Wizara ya Afya.
e) Kutayarisha mapitio ya matumizi ya fedha za serikali na wahisani - *Public Expenditure Review (PER)*.
f) Kupitia na kutayarisha mikataba mbali mbali ya sheria.

KITENGO CHA HESABU

Mhe. Spika, majukumu ya kitengo hiki ni kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya wizara pamoja na utunzaji wake kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Aidha, kitengo kina jukumu la kusimamia uchangiaji wa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 2.2.2 – 2.2.4.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 wizara imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 10,638,000,000 kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho na shilingi 1,020,000,000 kwa kazi za maendeleo. Wizara pia imepangiwa kuchangia jumla ya shilingi 17,191,000 katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo cha Hesabu kitaendelea na kazi ya kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya Wizara na utunzaji wake, pamoja na kusimamia uchangiaji wa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

KITENGO CHA UTUMISHI

Mhe. Spika, jukumu kubwa la kitengo hiki ni kushughulikia uajiri, haki na maslahi ya wafanyakazi. Aidha, kuhakikisha kuwa wastaafu pamoja na waliofariki wanakamilishiwa taratibu za kupata mafao yao. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 2.3.2 na 2.3.4.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo kitaendelea kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wote wa wizara ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

KITENGO CHA MAFUNZO

Mhe. Spika, Kitengo cha Mafunzo kina jukumu la kusimamia upatikanaji wa wataalamu wa afya kwa kuwapatia mafunzo ya ndani na hata nje ya nchi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Pia kwa kupitia Chuo cha Afya kuhakikisha kuwa wanapatikana watalamu wapya. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 2.4.2 – 2.4.7.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Kitengo cha Mafunzo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kutumia ripoti ya Mpango Mkuu wa Mafunzo *(Training Master Plan)*.

b) Kutumia kikamilifu Mfumo wa Taarifa za Wafanyakazi wa Afya *(Human Resource Information Systerm)*.

c) Kuhakikisha Divisheni ya Nguvu Kazi ina nyezo zinazohitajika kuiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

KITENGO CHA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Kitengo cha Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali kinafanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 2005. Majukumu ya kitengo hiki ni kusimamia manunuzi yote yanayofanywa na wizara kwa mujibu wa

sheria na taratibu zilizowekwa. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 2.5.2 na 2.5.3.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuandaa Mpango wa Manunuzi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
b) Kutoa elimu ya sheria ya ununuzi kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

KITENGO CHA TAKWIMU, MIENENDO YA MARADHI NA UTAFITI (*HMIS*)

Mhe. Spika, wajibu mkubwa wa kitengo hiki ni kusimamia shughuli zote za takwimu pamoja na taarifa mbali mbali kutoka Hospitali na Vituo vya Afya. Aidha, kitengo kina wajibu wa kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazohusiana na afya zinakusanywa, zinahifadhiwa, zinachambuliwa na kutoa viashiria (*indiicators*) mbali mbali kwa mujibu wa malengo ya milenia (*MDGs*), Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) na Mpango Mkakati wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya (*Health Sector Reform Strategic Plan*). Aidha, kitengo kina wajibu wa kutoa taaluma juu ya utunzaji na umuhimu wa utumiaji ya taarifa katika kupanga mipango kwa watendaji wote wa wizara hii. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 2.6.2 - 2.6.5.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kukusanya taarifa zote za afya kutoka katika hospitali na vituo vya afya vya serikali na binafsi.
b) Kukamilisha kitabu cha taarifa za mwaka 2009 (*Health Information Bulletin, 2009*)
c) Kutoa mafunzo kwa watendaji wakuu wa Wizara juu ya utumiaji wa *"Database"* ili waweze kupata taarifa popote walipo.
d) Kukamilisha mpango mkakati na muongozo wa mfumo wa taarifa za afya (*HIS*).

KITENGO CHA UFUNDI

Mhe. Spika, ili wafanyakazi wa afya waweze kufanya kazi kwa ufanisi wanahitaji mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kitengo cha Ufundi ndicho kilichopewa jukumu la kukagua vifaa vyote vya umeme, majengo yote ya wizara na kuyafanyia matengenezo yanayostahiki ili kuyaweka katika hali nzuri ya kutolea huduma. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 2.7.2 – 2.7.4

Mhe. Spika, tatizo kubwa lililokuwa likikikabili kitengo la ukosefu wa ofisi kwa sasa limeondoka kwani kitengo kimepata ofisi mpya huko Mwanakwerekwe kwenye eneo la karakana ya magari. Ofisi hii imejengwa kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) lililogharimu jumla ya shilingi milioni 228 za Tanzania hadi kumalizika kwake. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 2.7.3.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Kitengo cha Ufundi kitaendelea kufanya matengenezo ya hospitali, vituo vya afya pamoja na majengo ya Wizara ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi.

CHUO CHA TAALUMA ZA SAYANSI YA AFYA

Mhe. Spika, Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kina jukumu la kukidhi mahitaji ya nguvu kazi katika Sekta ya Afya Unguja na Pemba. Hii ni pamoja na Hospitali zetu Kuu, Vituo vya Afya vya Serikali na binafsi na jamii kwa jumla. Chuo hiki kinabaki kuwa ni taasisi pekee inayotambulika hapa Zanzibar kutoa mafunzo ya afya katika ngazi ya Cheti na Diploma. Ufafanuzi zaidi wa Kitengo hiki angalia kipengele namba 2.8.2 - 2.8.5

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 chuo kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa elimu ya kada mbali mbali za afya.
b) Kumaliza majengo yanayojengwa na Serikali ya Oman.
c) Kuongeza vifaa mbali mbali vya kusomeshea na mazowezi.

KITENGO CHA ELIMU YA KUJIENDELEZA

Mhe. Spika, Kitengo cha Elimu ya Kujiendeleza ni muhimu sana katika maendeleo ya wafanyakazi wa sekta ya afya. Kitengo hiki kina wajibu wa kuwatafutia wafanyakazi wa kada zote za wizara masomo ya kujiendeleza ndani na nje ya nchi. Pia kina wajibu wa kusimamia elimu ya kujiendeleza inayotolewa ndani ya wizara. Kwa maelezo zaidi ya Kitengo hiki angalia kipengele namba 2.9.2 – 2.9.6.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Elimu ya Kujiendeleza.
b) Kununua majenereta Unguja na Pemba kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma elimu masafa ili yatumike endapo umeme utakosekana.
c) Kuandaa mkutano wa kanda Unguja na Pemba.
d) Kusimamia utekelezaji wa muongozo wa mafunzo uliotayarishwa.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Spika, majukumu ya idara hii ni kusimamia utoaji wa huduma bora za afya Mijini na Vijijini na kubuni mbinu za kukabiliana na maradhi mbalimbali yakiwemo ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Aidha, idara hii inajukumu la kusimamia utoaji wa elimu ya afya kwa jamii. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele 3.0.2.

AFISI YA AFYA KANDA YA UNGUJA

Mhe. Spika, Afisi ya Afya Kanda ya Unguja ni kiungo kati ya wilaya, vitengo na taasisi nyengine za serikali na zisizo za serikali za ndani na nje zinazoshughulika na kazi za afya ili kuimarisha huduma za afya kwa jamii. Jukumu kuu la afisi hii ni kusimamia utoaji wa huduma unaofanywa na vituo vyote vya afya mjini na vijijini. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 3.1.2 na 3.1.8.

MRADI WA KUPAMBANA NA MARADHI YA MALARIA

Mhe. Spika, Mradi wa Kupambana na Maradhi ya Malaria una jukumu la kupambana na maradhi haya kwa kutumia njia mbali mbali ambazo zitasaidia kuondosha tatizo hili ambalo kwa muda mrefu limekuwa likiwasumbua wananchi hususan akinamama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Mhe. Spika, tatizo la homa ya malaria limeonekana kupungua kwa kiasi kikubwa. Utafiti wa Tanzania *HIV and Malaria Indicator Survey (THMIS)* uliofanyika mwaka 2007/2008 unaonesha kwamba kiwango cha malaria kimefikia chini ya asilimia 1. Maelezo kwa urefu ya mafanikio ya mradi wa malaria yanaonekana katika kipengele nambari 3.2.3 – 3.2.12.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Mradi wa Kupambana na Maradhi ya Malaria umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea na kazi za upigaji dawa majumbani kwa Unguja na Pemba katika maeneo maalum yatakayoonekana na maambukizo ya malaria.
b) Kuangalia uwezo wa dawa zinazotumika kwa kupigia dawa majumbani.
c) Kuendelea na kazi ya kuangamiza viluilui (*Larviciding*) kwa baadhi ya maeneo Mijini Unguja na Pemba.
d) Kusimamia uhakiki wa uchunguzi wa vimelea vya malaria kwenye vituo vya Afya vya Serikali na vya Binafsi.
e) Kuongeza vituo vya afya 28 kwenye mfumo wa uhakiki wa uchunguzi wa vimelea vya malaria Unguja na Pemba.

f) Kuendeleza ugawaji wa vyandarua kwa wananchi katika Wilaya za Chake Chake na Mkoani.
g) Kufanya utafiti kuhusu uelewa wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria nchini.

KITENGO CHA ELIMU YA AFYA

Mhe. Spika, Kitengo cha Elimu ya Afya kina majukumu makubwa ya kuelimisha jamii kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Kitengo hiki ni kiungo kikuu katika kuunganisha kazi zote za kuelimisha jamii zinazohusiana na masuala ya afya. Malezo zaidi ya utekelezaji wa shughuli za kitengo hiki kwa mwaka 2009/2010 angalia kipengele namba 3.3.2 – 3.3 5.

KITENGO CHA KUDHIBITI MARADHI YA KIFUA KIKUU NA UKOMA

Mhe. Spika, Kitengo cha Kudhibiti Maradhi ya Kifua Kikuu na Ukoma kina wajibu wa kuchunguza, kutibu, kufuatilia wagonjwa na kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya namna ya kujikinga. Kitengo hiki kinafanya kazi kwa msaada mkubwa wa shirika lisilo la Kiserikali la Kifua Kikuu na Ukoma la Ujerumani (*GLRA*) pamoja na Mfuko wa Fedha wa Dunia (*Gobal Fund*). Maelezo zaidi ya utekelezaji wa shughuli za kitengo hiki angalia kipengele namba 3.4.2. na 3.4.3.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 kitengo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kutoa mafunzo ya kupambana na maradhi ya Kifua Kikuu na Ukoma kwa wafanyakazi wa vituo vya afya.
b) Kufaya usimamizi wa vituo vinavyotoa huduma ya Kifua Kikuu na UKIMWI.
c) Kuanzisha ulaji wa dawa za kurefusha maisha kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu na UKIMWI pamoja na kufanya ufuatiliaji.
d) Kuendelea kufuatilia wagonjwa wanaotoroka kwenye matibabu.
e) Kuendelea kupima makohozi kwenye vituo vyote vinavyotoa huduma za kupima Kifua Kikuu.
f) Kuendelea kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya maradhi ya Kifua Kikuu, UKIMWI na Ukoma.

KITENGO CHA KUPAMBANA NA KICHOCHO, MINYOO NA MATENDE

Mhe. Spika, kitengo hiki kina majukumu ya kuzuia kuenea kwa Kichocho, Matende na Mabusha pamoja na kukinga na kuzuia ulemavu utokanao na maradhi haya. Kitengo hiki angalia kipengele namba 3.5.2 – 3.5.5.

KITENGO CHA KUPAMBANA NA MARADHI YA WATOTO NA MAGONJWA YA KUHARISHA (*IMCI*)

Mhe. Spika, kitengo cha *IMCI* (*Integrated Management of Childhood Illnesses*) kina jukumu la kusimamia utoaji wa matibabu sahihi kwa watoto walio chini ya miaka mitano kama muongozo unavyoeleza. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 3.6.2 na 3.6.3.

KITENGO CHA HUDUMA ZA MACHO

Mhe. Spika, Kitengo cha Huduma za Macho Zanzibar *(Zanzibar Comprehensive Eye Care Service - ZCES)* kina jukumu la kutoa huduma sahihi ikiwemo matibabu ya macho kwa wananchi wote. Lengo kubwa la kitengo hiki ni kupunguza na kutokomeza kabisa upofu unaoweza kuepukika pamoja na kutibu wagonjwa walioathirika. Kitengo hiki kinafanya shughuli zake kwa kushirikiana na shirika la "*Sightsaver International*" lenye makao makuu yake nchini Uingereza. Aidha, kitengo kinashirikiana na sekta nyengine za serikali na jumuiya zisizo za kiserikali zikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Jumuiya ya Watu Wasioona (*ZANAB*) pamoja na mtandao wa huduma za macho Zanzibar (*ZEHN*). Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 3.7.2 na 3.7.3.

IDARA YA AFYA YA JAMII

Mhe. Spika, Idara ya Afya ya Jamii ina jukumu kubwa la kusimamia, kushajiisha na kuelimisha jamii jinsi ya kuweka mazingira safi kwa ajili ya kujikinga na maradhi mbali mbali, yakiwemo maradhi ya miripuko kutoka ndani na nje ya nchi yetu. Kama vile magonjwa ya Mafua ya Nguruwe, *Ebola*, *Dengu Fever* na mengineyo. Katika kusimamia hayo, idara imeweza kukamilisha mpango mkakati wa kukabiliana na Mafua ya Nguruwe. Vile vile idara imeweza kuimarisha ukaguzi Uwanja wa Ndege kwa kujenga sehemu mpya za kukagua abiria wanaoingia nchini. Pia idara imeweza kuzipitia na kuunda upya Sheria ya Afya ya Jamii na rasimu ya mwanzo ya sheria hiyo sasa iko tayari. Aidha, idara pia ina jukumu la kuangalia afya za wafanyakazi wa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali. Idara hii ina vitengo vifuatavyo:-

KITENGO CHA AFYA ZA BANDARINI

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 kitengo kiliweza kufanya ukaguzi wa vyombo 304 vya baharini. Katika ukaguzi huo mapungufu yaliyoonekana ni pamoja na wafanyakazi kutofanyiwa uchunguzi wa afya zao (*medical checkup*), kuwepo kwa wadudu mbali mbali (Mende na Panya), ukosefu wa vifaa vya usafi na uelewa mdogo wa elimu ya afya kwa wafanyakazi. Utekelezaji zaidi wa kitengo hiki angalia kipengele namba 4.1.2 na 4.1.5.

KITENGO CHA LISHE

Mhe. Spika, Kitengo cha Lishe kina wajibu wa kusimamia shughuli zote za hali ya lishe, ikiwemo lishe kwa watoto. Pia kina jukumu la kuwajengea uwezo watoa huduma za afya juu ya ulishaji na ufuatiliaji wa maendeleo ya ukuaji wa mtoto. Kitengo kinafanya kazi kwa kushirikiana na vitengo vya Idara ya Kinga, Hospitali, Timu za Afya za Wilaya (*DHMTs*) pamoja na taasisi nyingine zilizo nje ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Utekelezaji zaidi wa shughuli za kitengo hiki unaonekana katika kipengele nambari 4.2.3 – 4.2.5.

KITENGO CHA AFYA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya ya Mazingira kina majukumu ya kudhibiti kuenea kwa maradhi na matatizo ya kiafya yanayosababishwa na uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli mbali mbali zinazofanywa ndani ya jamii kwa njia moja ama nyengine husababisha mazingira hatarishi kwa afya ya binadamu. Maelezo kwa urefu ya utekelezaji wa Kitengo hiki angalia kipengele nambari 4.3.2 – 4.4.6.

KITENGO CHA AFYA YA WAFANYAKAZI

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi kinatoa huduma za kufanya ukaguzi wa mazingira ya kazi, uchunguzi wa Afya za wafanyakazi, kutoa ushauri nasaha na elimu ya afya kwa wafanyakazi na kuongeza mashirikiano na vitengo vyengine ndani na taasisi nyengine za nje ya wizara kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 4.4.2 – 4.4.4.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imeundwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja yenyewe, Hospital ya Magojwa ya Akili – Kidogo Chekundu pamoja na Hospitali ya Wazazi Mwembeladu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo naomba uniruhusu nitoe maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya hospitali za idara hii.

HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja inatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa nje na ndani pamoja na huduma nyengine za uchunguzi kama *X-Ray, Ultra Sound, CT Scan* na kutoa huduma nyenginezo kupitia kliniki za maradhi maalum. Mafanikio mengine ya Hospitali ya Mnazi Mmoja angalia kipengele namba 5.1.2 – 5.1.10

Mhe. Spika, mwaka 2010/2011 hospitali itatilia mkazo mambo yafuatayo:-

a) Kuimarisha utoaji huduma bora za uchunguzi na matibabu.
b) Kuhakikisha vifaa na dawa muhimu zinapatikana wakati wote.
c) Kuboresha huduma za afya ya akili (*Mental Health Services*).
d) Kujenga *incinerator* kubwa ili kuondoa msongamano wa taka.

HOSPITALI YA WAZAZI MWEMBELADU

Mhe. Spika, Hospitali ya Wazazi Mwembeladu hutoa mchango mkubwa kwa akina mama wanaohitaji huduma za uzazi hususan kutoka mashamba na ng'ambo ya mji wa Zanzibar. Mafanikio mazuri yamepatikana katika utoaji wa huduma za uzazi katika hospitali hii. Kwa kipindi cha Julai, 2009 mpaka Machi, 2010 jumla ya akina mama 3,467 walilazwa na kati yao 2,550 walijifungua kwa njia za kawaida. Ufafanuzi zaidi unatolewa katika kiambatisho Nam. 5.3. kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 5.2.2 na 5.2.3.

HOSPITALI YA MAGONJWA YA AKILI – KIDONGO CHEKUNDU

Mhe. Spika, Hospitali ya Magonjwa ya Akili iliyopo Kidongo Chekundu inabakia kuwa Hospitali ya Rufaa kwa magonjwa ya akili hapa Zanzibar. Pia inaendelea kutoa huduma za kupelekea kurekebisha tabia ya kuacha matumizi ya dawa za kulevya. Kwa maelezo zaidi ya hospitali hii angalia kipengele namba 5.3.2 – 5.3 5.

IDARA YA TIBA

Mhe. Spika, Idara ya Tiba ni moja kati ya idara muhimu sana katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa sababu huduma za matibabu kwa kiasi kikubwa hutolewa kupitia idara hii. Idara inajumuisha Hospitali za Abdalla Mzee, Chake Chake na Wete kwa Pemba na Hospitali za Vijiji za Vitongoji na

Micheweni kwa Pemba na Makunduchi na Kivunge kwa wa Unguja. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 6.0.2 na 6.12.0.

HOSPITALI YA CHAKE CHAKE

Mhe. Spika, Hospitali ya Chake Chake ndio hospitali kubwa na inaendelea kuwa Hospitali ya Rufaa kwa Pemba. Katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa kuanzia Julai, 2009 hadi Machi 2010, jumla ya wagonjwa 72,163 walipatiwa huduma za nje. Kati ya hao wanawake walikuwa 38,286 na wanaume 33,877. Wagonjwa 5,355 walilazwa ambapo 3,587 walikuwa wanawake na 1, 768 walikuwa wanaume. Wagonjwa 118 (asilimia 2.2) walifariki wakiwemo wanawake 32 na wanaume 86. Ufafanuzi zaidi wa wagonjwa waliopatiwa huduma za nje, waliolazwa na waliofariki angalia kiambatisho Nam. 6.1.

HOSPITALI YA ABDALLA MZEE

Mhe. Spika, hospitali ya Abdalla Mzee imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wa Wilaya ya Mkoani na Pemba kwa ujumla. Jumla ya wagonjwa 23,516 walipata huduma za nje, wagonjwa waliolazwa walikuwa 3,454 kati yao wagonjwa 64 walifariki sawa na asilimia 1.8 ya wagonjwa wote waliolazwa. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatisho namba 6.1. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 6.2.1 na 6.2.3

HOSPITALI YA WETE

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2009 hadi Machi, 2010 Hospitali ya Wete imeendelea kutoa huduma za matibabu kama kawaida. Jumla ya wagonjwa 32,159 walipatiwa huduma za nje, 3,302 walilazwa na wagonjwa 42 sawa na asilimia 1.2 walifariki dunia. Kiambatisho namba 6.1 kinatoa ufafanuzi zaidi. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 6.3.2.

HOSPITALI ZA VIJIJI (*COTTAGE HOSPITALS*)

Mhe. Spika, hospitali za Vijiji ni-: Micheweni, Vitongoji, Makunduchi na Kivunge. Hospitali hizi zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwapatia huduma za tiba wananchi wa Unguja na Pemba hasa kwenye vijiji vinavyozunguka na vilivyo karibu ya hospitali hizo. Hospitali hizi zinakuwa pia hospitali za rufaa kwa wagonjwa kutoka vituo vya afya vya karibu. Sasa naomba kueleza utekelezaji wa shughuli za hospitali hizi moja baada ya nyengine. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 6.5.0 – 6.8.3

MPANGO WA DAMU SALAMA

Mhe. Spika, matumizi ya damu salama ni muhimu sana katika kuokoa maisha ya wagonjwa wanaohitaji kusaidiwa damu. Katika kufikia hilo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeanzisha Mpango Maalumu wa Huduma za uchangiaji wa damu salama katika maabara maalumu iliyoko Sebleni. Utaratibu huu una lengo la kuondoa usumbufu wa kutafuta jamaa wa mgonjwa kumchangia damu wakati inapohitajika. Pia unawezesha kuwepo damu wakati wowote ikiwa tayari imechunguzwa na inakubalika kutumika kwa wagonjwa. Kwa maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi za Mpango wa Damu Salama angalia kipengele Nam. 6.13.2 – 6.13.5.

IDARA YA USTAWI WA JAMII

Mhe. Spika, idara hii inatoa huduma za kijamii kwa watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, wazee wasiojiweza ambao hawana ndugu wala jamaa wa kuwatunza, watu wenye ulemavu, wanaofikwa na ajali kazini na wanaoanguka mikarafuu. Idara hii pia inatoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI, wananchi wanaofikwa na shida mbalimbali za kijamii na pia inatoa huduma ya kuzika maiti ambazo wenyewe hawajulikani au hawakujitokeza.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2010 Idara imezika jumla ya maiti 8 ambazo 7 hazikuwa na wenyewe kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na mmoja kutoka Nyumba ya Wazee Welezo. Jumla ya shilingi 1,650,000 zilitumika kwenye kununulia vifaa vya kuzikia, usafiri, uchimbaji wa kaburi pamoja na maslahi ya waoshaji na wazikaji. Utekelezaji kwa urefu wa shughuli za idara hii unatolewa katika kipengele Nam. 7.0.3 - 7.0.10.

Mhe. Spika, pamoja na kazi zake nyengine kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Idara imejipangia malengo yafuatayo:-

a) Kusimamia utumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Watoto waishio katika mazingira magumu (*MVC – Data Management System*).
b) Kutengeneza Sera ya Taifa ya Watoto waishio katika mazingira magumu.
c) Kuendelea kufanya utambuzi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwenye shehia 21 zilizobakia katika Wilaya ya Wete na Magharibi.
d) Kutoa mafunzo kwa Kamati za Watoto Waishio katika Mazingira Magumu katika shehia 120 za Unguja na Pemba.
e) Kukamilisha, kusimamia na kufanya tathmini ya miradi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

IDARA YA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA NA KUREKEBISHA TABIA

Mhe. Spika, Idara ya Kupambana na Madawa ya Kulevya na Kurekebisha Tabia ina jukumu la kuratibu mapambano dhidi ya biashara na matumizi haramu ya dawa za kulevya, kuelimisha jamii athari za matumizi ya dawa hizo kupitia njia mbali mbali ikiwemo vyombo vya habarí, taasisi za elimu, mikutano ya kijamii (shehia) sehemu za kazi na jamii kwa ujumla na kutoa huduma za ushauri nasaha pamoja na msaada wa tiba kwa waathirika wa madawa hayo. Maelezo kwa urefu ya utekelezaji wa shughuli za idara hii yanaonekana katika kipengele Nam. 8.0.2 – 8.0.15.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 idara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuandaa miongozo (*Guidelines*) juu ya huduma za Dawa za Kulevya.
b) Kuendeleza Huduma za upimaji Virusi vya UKIMWI kwa hiari (*Voluntary Counselling and Testing - VCT*) katika Kituo cha Huduma Rafiki kwa Vijana cha hapo Sogea kwa wateja na jamii kwa ujumla.
c) Kuelimisha jamii juu ya upigaji vita matumizi ya dawa kulevya.

MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu kubwa la kutoa huduma kitaalamu na kisayansi katika kuhakikisha ubora na usalama wa vyakula, vinywaji, vipodozi na madawa katika kuhakikisha usalama wa afya ya kila raia. Maabara pia ina jukumu kubwa la kutoa ushauri juu ya matumizi bora ya kemikali na kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka katika taasisi tofauti vinavyohusiana na makosa ya jinai. Utekelezaji wa shughuli za maabara unaonekana katika kipengele Nam. 9.0.1 – 9.0.4.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imelenga yafuatayo:-

a) Kukamilisha rasimu ya sheria ya maabara pamoja na sheria ya kemikali.
b) Kukamilisha ukarabati wa jengo na kuongeza vifaa vya kisasa vya uchunguzi.
c) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake.
d) Kuboresha huduma za *microbiology*.

MAABARA YA AFYA YA JAMII *PUBLIC HEALTH LABORATORY (PHL)*

Mhe. Spika, Maabara ya Afya ya Jamii inaendeshwa kwa mashirikiano na taasisi isiyo ya kiserikali ya *IVODE CARNERI* iliyopo Milan – Italy ikiwa na

malengo ya kufanya tafiti mbali mbali za afya, kuangalia mienendo ya maradhi mbali mbali yanayoathiri afya ya jamii hapa Zanzibar na kutafuta mbinu mbali mbali ya kuyadhibiti maradhi hayo.
Mhe. Spika, maabara ilifanikiwa kuweka *Solar Pannels (Installation of Solar Panels)* katika ofisi zake, kujenga banda la gari (*Car Park*), utengenezaji wa *incenerator (Incinerator and Construction of Refuse Pit)*, matengenezo ya nyumba ya wageni (*PHL Guest House*) pamoja na kufanya matengenezo ya *Generator*. Pia kupitia maabara hii mfanyakazi mmoja (*Accountant*) amepelekwa masomoni kwa udhamini wa *IVODE CARNERI*.

TAASISI MAALUM

Mhe. Spika, taasisi maalum ni vyombo vilivyoundwa kisheria kwa lengo la kusimamia mambo maalum katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Zanzibar. Vyombo hivi hujikita katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa. Baada ya utangulizi huo sasa naomba nieleze utekelezaji wa shughuli za taasisi hizo kwa kuangalia taasisi moja baada ya nyengine.

BODI YA USHAURI YA HOSPITALI ZA BINAFSI

Mhe. Spika, Bodi ya Ushauri ya Hospitali za Binafsi inafanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 1994 (*Private Hospital Regulation Act*). Majukumu ya Bodi hii ni kupokea, kushughulikia na kuamua maombi ya kuanzisha hospitali binafsi, kusajili na kutoa leseni na kuweka masharti ya kuanzisha na kuendesha hospitali hizo. Kwa maelezo zaidi ya utekelezaji wa shughuli za Bodi angalia kipengele Nam. 11.1.2 – 11.1.5 na 11.1.6**.**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Bodi itafanya marekebisho ya sheria ya kuendesha hospitali binafsi, kuzidisha mashirikiano kati ya serikali na sekta binafsi ili kuhakikisha wanatoa huduma za kisasa.

KITENGO CHA DAWA NA ZANA ZA TIBA

Mhe. Spika, upatikanaji wa dawa ni miongoni mwa mhimili mkuu wa uboreshaji wa huduma za tiba kwa wananchi**.** Kitengo cha Dawa na Zana za Tiba (*Medicine Management Unit*) ndicho kilichopewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa (*Medicine Policy*) ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu na zana za tiba (*Essential Medicine*), pamoja na utumiaji mzuri wa dawa hizo (*Rational Use of Drugs*). Kwa maelezo zaidi angalia kipengele no. 11.2.2 na 11.2.3

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2009 – Mei, 2010 wizara kupitia kitengo hiki imeweza kupokea dawa na zana za tiba zenye thamani ya jumla ya shilingi za Tanzania bilioni 1,485,428,111. Ufafanuzi zaidi wa thamani ya dawa zilizopatikana angalia kiambatisho namba 11.1.

BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA

Mhe. Spika, Baraza hili limeanza kufanya kazi zake mwaka 2009 chini ya sheria namba 8 ya mwaka 2008 likiwa na jukumu la kulinda afya ya wananchi wa Zanzibar ambao mara nyingi hutumia tiba za asili. Shughuli za Baraza kwa upande wa Pemba zinafanywa kupitia sekretariet ya Baraza hili. Kwa ufafanuzi zaidi wa shughuli za baraza hili angalia kipengele namba 11.3.3 – 11.3.5. na 11.3.6.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza limejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili.
b) Kutoa taaluma ya sheria kwa waganga wote juu ya taratibu za kisheria zinazotakiwa katika kufanya shughuli za tiba asili.
c) Kuwasajili waganga wote wenye sifa.
d) Kuendelea kusajili maduka na kliniki zote zinazoshughulika na dawa za tiba asili na tiba m'badala.
e) Kufanya ukaguzi wa maduka ya dawa na kliniki zote.
f) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji kwa waganga.
g) Kufanya utambuzi wa waganga wa tiba asili na tiba mbadala katika shehia zilizobaki.

BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA

Mhe. Spika, Baraza la Wauguzi na Wakunga ni chombo kinachofanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 1986. Chombo hiki kina majukumu ya kusimamia utoaji huduma za uuguzi, kusajili wauguzi na wakunga wa hapa Zanzibar, kutoa leseni kwa muuguzi na mkunga wa hapa Zanzibar na kutoka nje ya Zanzibar, kuchukua hatua za kinidhamu kwa mkunga au muuguzi yeyote atakayekwenda kinyume na maadili ya uuguzi na ukunga.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 Baraza limeweza kusimamia mafunzo ya wauguzi ya elimu masafa wenye vyeti na kupata stashahada na pia MCH kuwa PHNB. Aidha, Baraza liliendelea na kufuatilia maslahi ya wauguzi ili kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza litaendelea na kazi ya kufuatilia mafunzo ya wauguzi wenye vyeti na kupatiwa stashahada,

kuhakikisha wauguzi wote wanapatiwa sare kulingana na kada zao, kutafuta usafiri utakaosaidia ufuatiliaji wa kazi za kiuguzi zinazofanyika mahospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba.

BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI

Mhe. Spika, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi inafanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 2 ya mwaka 2006. Bodi hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba chakula, dawa na vipodozi vinavyoingia nchini ni salama kwa matumizi ya binadamu**.**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Bodi hii imeweza kufanya uchunguzi wa sampuli 591 za chakula, kati ya hizo 453 zilipasi na 38 zilifeli. Aidha, bodi ilichunguza sampuli 419 za dawa kati ya hizo sampuli 412 zilipasi na sampuli 7 zilifeli. Vile vile bodi iliweza kuteketeza jumla ya tani 530 za bidhaa mbali mbali zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Bodi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kuimarisha maabara yake inayotumika katika uchunguzi wa bidhaa mbalimbali zinazodhibitiwa na Bodi.
(b) Kuimarisha ukaguzi wa vipodozi vilipopigwa marufuku, vinavyobadilisha maumbile pamoja na kushuhughulikia udanganyifu unaofanywa na baadhi ya watoa huduma za Chakula na Tiba Asilia.
(c) Kushiriki kikamilifu katika mpango wa uwiano wa usajili wa Dawa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na mtandao wa ufuatiliaji wa Dawa duni na bandia ulimwenguni.

MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa Idara zote na taasisi za Wizara sasa naomba uniruhusu kueleza utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Uendeshaji wa miradi hii unatokana na fedha za Serikali, msaada na mikopo kutoka kwa washirika wetu wa Maendeleo. Kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekuwa ikitekeleza jumla ya miradi 7 ya maendeleo ambayo ni:-

1. Mradi wa Mabadiliko wa Sekta ya Afya.
2. Mradi wa Kupambana na Maambukizo ya Ukimwi.
3. Mradi wa Chanjo za Mama na Mtoto.
4. Mradi wa kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi.

5. Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto.
6. Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Akili.
7. Mradi wa Chuo cha Madaktari cha Zanzibar.

MRADI WA MABADILIKO YA SEKTA YA AFYA

Mhe. Spika, Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya unaongozwa na Sekretarieti ya Mabadiliko ya Sekta ya Afya ambayo Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Sekretarieti hii hufanya vikao vyake kila baada ya miezi mitatu na kutoa maamuzi ambayo hutekelezwa na vikundi vya kitaalamu vinne vilivyoundwa. Vikundi hivyo ni Kikundi cha Kuratibu Gharama za Kutoa Huduma za Afya, Kikundi cha Kuratibu Ubora wa Huduma za Afya, Kikundi cha Kuratibu Ufanisi wa Utekelezaji wa Kazi na Kikundi cha Kuratibu Rasilimali Watu kwa ajili ya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia mradi huu imefanya mapitio ya Sera ya Afya toleo la mwaka 1999. Sera hiyo kwa kiasi kikubwa ilikuwa imepitwa na wakati na haioani na baadhi ya sera za kitaifa. Kazi ya mapitio ya sera hiyo ilifanywa kwa mashirikiano ya mtaalamu mshauri kutoka nje ya nchi pamoja na wataalamu wa ndani. Mchakato wa kuifanyia marekebisho sera hiyo umechukua takriban mwaka mmoja. Jambo hili ni la kupigiwa mfano kwani ni nchi chache zinazoendelea zilizoweza kufanikisha kazi hiyo kubwa kwa kipindi kifupi kama hicho.

Mhe. Spika, rasimu mpya ya Sera ya Afya ya Zanzibar imebeba maoni ya wadau wengi wa sekta ya afya vikiwemo vyama vya siasa. Aidha, rasimu hiyo imekwenda sambamba na Sera ya Zanzibar Dira ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), masuala ya haki za binadamu, masuala ya jinsia na imefuata muongozo wa Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO).* Sera hiyo kwa sasa imeshatafsiriwa na imo katika mchakato wa kupata baraka katika vikao mbali mbali vya serikali ili iidhinishwe rasmi na kuanza kutumika. Kwa maelezo zaidi angalia kipengele Nam. 12.1.4 – 12.7.8.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, licha ya Wizara kuwa na mafanikio mengi katika mwaka wa fedha 2009/2010 bado zipo changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuweza kusukuma mbele gurudumu la kutoa huduma za afya kwa wananchi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa wafanyakazi pamoja na maslahi yao, ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Afya na

Ustawi wa Jamii pamoja na ongezeko la maradhi yasiyo ya kuambukiza hususan Kisukari. Hata hivyo, Wizara itaendelea na juhudi zake zote ili kuhakikisha kwamba matatizo haya yanashughulikiwa ipasavyo.

MALENGO MAKUU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA 2010/2011

a) Kujenga Wodi ya Wagonjwa wa Akili katika Hospitali ya Wete Pemba.

b) Kujenga Kituo cha Kuhudumia Waathirika wa UKIMWI huko Gombani Pemba.

c) Kujenga Kituo cha Kuhudumia Waathirika wa Madawa ya Kulevya na UKIMWI huko Tunguu.

d) Kuwapatia mafunzo ya kada mbali mbali wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kuimarisha huduma za kinga na tiba katika hospitali na vituo vyote vya afya.

e) Kujenga majengo matatu katika Chuo cha Afya Mbweni. Jengo moja kwa ajili ya madarasa na majengo mawili ya dakhalia kwa udhamini wa Serikali ya Oman.

f) Kujenga kituo kimoja cha afya na nyumba 2 za wafanyakazi katika wilaya ya Micheweni kwa udhamini wa *UNDP*.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 10, 810,300,000 kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho na shilingi 1,200,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2010 jumla shilingi 9,422,549,317 (87%) ziliingizwa. Kati ya hizo Tshs. 7,587,012,184 (91%) kwa ajili ya mishahara na maposho na Tshs. 1,835,537,129 (73%) kwa ajili ya kazi za kawaida *(Other Charges).* Aidha Wizara iliingiziwa jumla ya shilingi 737,919,716 (61%) kwa kazi za maendeleo. Wizara pia ilipangiwa kuchangia jumla ya Tshs. 19,000,000 katika mfuko mkuu wa serikali. Hadi kufikia Mei, 2010 jumla ya shilingi 13, 554,000 (68.4%) ya makadirio zilikwishakusanywa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Wizara imepangiwa kutumia jumla ya Tshs 10,638,000,000 kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho na Tshs.1,020,000,000 kwa kazi za maendeleo. Wizara pia imepangiwa kuchangia jumla ya Tshs. 17,191,000 katika mfuko mkuu wa Serikali.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ndiyo taasisi inayobeba jukumu la utoaji wa huduma za afya nchini mwetu. Lengo hili halitofikiwa bila ya mashirikiano makubwa baina ya Wizara yangu, Sekta za watu binafsi *(Private Sector)* na jamii *(community)* kwa ujumla. Sinabudi kuishukuru jamii ya Wazanzibari na sekta binafsi kwa kushirikiana kikamilifu na Wizara yangu katika utoaji wa huduma za afya. Nawaomba waendelee kutoa huduma zilizo bora zaidi kulingana na taratibu na sheria na kanuni za afya.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako pamoja na wewe binafsi mmekuwa mstari wa mbele kuchangia na kuielekeza Wizara yangu kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo yake kwa ufanisi. Sina budi kukushukuruni nyote. Natambua kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi, inawezekana sote kupata nafasi tena ya kurejea kwenye baraza hili kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mategemeo yangu tutapata fursa nyengine tena ya kuchangia, kuishauri na kuielekeza wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Kwa wale ambao hawatopata fursa ya kurejea kwenye baraza hili bado wana nafasi kama hiyo wakiwa nje ya baraza kwani michango yao itakuwa bado inahitajika kama ilivyo kwa watu wote wa nchi hii.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii adhimu kuwashukuru viongozi wote na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano waliyonipa kwa kipindi chote cha uongozi wangu, bila ya wao nisingaliweza kuongoza Wizara kwa mafanikio. Naomba mashirikiano ya aina hiyo yaendelee kwa yeyote ataepata fursa ya kuongoza wizara hii muhimu kwa ustawi wa Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, kuniwezesha mimi leo kusoma hotuba yangu mbele yenu mchango mkubwa umetolewa na wafanyakazi wa wizara yangu, nawashukuru sana. Pia naishukuru Idara ya Uchapaji kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii kwa uagalifu mkubwa na kupatikana kwa wakati.

Mhe. Spika, huduma za afya zilipata msukumo mkubwa kutoka kwa Serikali za nchi marafiki taasisi na mashirika ya kitaifa na kimataifa. Hivyo mimi binafsi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wananchi wote kwa ujumla, tunatoa shukrani zetu za dhati kwao. Hali hii mara nyingi imetuwezesha kutoa huduma za afya kwa ufanisi na kwa wepesi. Naomba wote waendelee kuwa nasi bila ya kuchoka. Shukurani hizo naomba ziende kwa nchi za Cuba, China, Misri, India, Israel, Oman, Saudi Arabia, Marekani, Germany, Korea, Italy, Netherlands, Ufaransa na Belgium. Pia shukurani ziende Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB), Agakhan Foundation, WHO, UNICEF, UNDP, UNFPA, WORLD BANK, ZAYEDESA, KAROLISNKA INSTITUTE, SAVE THE*

CHILDREN FUND, DANIDA, IVODE CARNERI FOUNDATION, AMD, GLOBAL FUND, CLINTON FOUNDATION, COLOMBIA UNIVERSITY, JICA, HIPZ, Italian Corporation, International Vaccine Institute (IVI), Research Triangle Institute Impact East Africa na wale wote ambao sikuwataja katika orodha huu.

Mhe. Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, utategemea kupitishwa kwa hotuba yangu. Naomba baraza lako liipokee, liijadili, liichangie kwa uwazi na hatimae liipitishe ili wizara iweze kutekeleza vyema majukumu na malengo iliyojipangia. Aidha baraza hili naomba liidhinishe jumla ya Tshs.1,800,000,000 kwa kazi za kawaida, Tshs.8,838,000,000 kwa mishahara na maposho Tshs.1,020,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwa idhini yako naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa na utulivu kwa muda wote Mhe. Waziri alipokuwa anawasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kuungwa mkono kwa hoja hii na Waheshimiwa Wajumbe inamaanisha kwamba sasa tuijadili. Taratibu za kanuni zinatuelekeza kwanza tumsikilize Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema leo hii. Namuomba Mola msifika anizidishie nguvu za kusimama imara mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunitengea muda katika shughuli za Baraza lako tukufu leo hii, ili niwasilishe yale yaliyoonekana na Kamati yetu kwa bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, pongezi za dhati tunazitoa kwa Mhe. Sultan Mohammed Mugheiry, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Shawana Bukheti Hassan, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Moh'd Saleh Jidawi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Pemba, Madaktari wetu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake katika Wizara hii.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilikutana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika siku ya Jumanne tarehe 01/06/2010 na kuijadili kwa kina bajeti ya Wizara hiyo ambayo inajumuisha jumla ya shilingi za Kitanzania 11,658,000,000/=.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sitatoa shukurani kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kutenga muda wao na kutekeleza majukumu ya Kamati yetu kila wanapohitajika kufanya hivyo, bila ya kujali wingi wa majukumu ya kifamilia na kitaifa waliyonayo.

Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanakamati hao kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe. Haji Faki Shaalí	-	Mjumbe
7.	Mhe. Hasnuu Moh'd Hají	-	Mjumbe
8.	Mhe. Moh'd Ali Salim	-	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
10.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
11.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
12.	Ndg. Salmin Amour Abdalla	-	Katibu
13.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Spika, inaonesha dhahiri kwamba kamati yetu hii kwa mwaka huu ilikuwa na watu wazito ambao kwa asilimia kubwa imehakikisha imefanya kazi vizuri juu ya kuwatetea wananchi wetu katika kupata maslahi mazuri ya afya.

Mhe. Spika, Kamati inaona fahari kubwa kwamba inamaliza msimu huu wa utendaji wa miaka miwili na nusu tukiwa tayari tumeshaipata mashine ya kisasa ya kuchunguzia maradhi ya *CT Scan.*

Tunampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume kwa jitihada zake za dhati katika kufanikisha upatikanaji wa kifaa hicho muhimu ambacho kitawaondolea usumbufu wananchi wa Zanzibar kufuata huduma ya uchunguzi huko Dar-Es-Salaam. Kwa miaka mingi Wazanzibari walisumbuka sana na kutumia gharama kubwa katika suala la uchunguzi na matibabu nje ya Zanzibar kutokana na uhaba wa vifaa.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi kubwa za Mhe. Waziri kuwapeleka wafanyakazi wake 48 wa kada mbali mbali kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ni jambo la busara pia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kufanya juhudi za makusudi kuwapatia wataalamu wazalendo ujuzi wa kutumia mashine hiyo ili kutatua tatizo sugu linalowakabili wananchi la kusubiri majibu yao kwa siku kadhaa. Hali hii imetokana na upungufu wa madaktari bingwa wa kuitumia mashine hiyo ipasavyo na hivyo kusababisha mzigo mzito kwa daktari mmoja wa Kichina ambaye ndiye anayetoa huduma hizo kwa sasa.

Mhe. Spika, Wizara kwa kupitia Kitengo cha Mipango, Sera na Sheria imetoa mafunzo kwa wafanyakazi wake 53 wanaoshughulikia uundaji wa mpango kazi *(plan of action)* kwa nia ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la makaazi bora kwa madaktari na wafanyakazi wengine wa kada ya afya, Wizara imejitahidi kuimarisha huduma hiyo kwa wafanyakazi wake ili nao wapate fursa nzuri ya kuwahudumia wananchi kwa urahisi zaidi, hasa kuhusiana na huduma za kinamama na watoto. Kazi ya ujenzi wa nyumba 20 za wafanyakazi katika vituo vya afya – Unguja imekamilika. Kwa upande wa Pemba nyumba 20 zilizopangwa kujengwa zimefikia asilimia thamanini (80%) na kazi iliyobakia inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Julai, 2010.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano makubwa na Serikali ya Cuba imeanzisha mafunzo ya madaktari 12 wakiwemo wanawake 3 na wanaume 9. Waheshimiwa huu ni mwanzo mzuri kwa nchi yetu angalau kuanza kutoa mafunzo ya udaktari, kwani ni moja ya kada zenye upungufu mkubwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, uanzishwaji wa mfumo mpya wa taarifa utaiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupokea na kutoa habari zake kwa ufanisi mkubwa na hivyo kwenda sambamba na ulimwengu wa leo wa sayansi na teknolojia. Mpango mkakati na muongozo wa mfumo huo utaanza rasmi mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2010 chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya *(EU).*

Mhe. Spika, Wizara inaendelea vyema na juhudi zake za kupambana na madawa ya kulevya nchini, ili kuwanusuru vijana ambao ndio nguvukazi ya Taifa hili. Hivi karibuni, Mswada wa Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya ulipitishwa na Baraza hili na hadi sasa uko tayari kwa kutumika.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukipatia Kitengo cha Ufundi afisi ya kufanyia kazi zao ambayo iko Mwanakwerekwe mjini Zanzibar kwa mashirikiano makubwa na Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA).* Kazi

kubwa iliyobakia ni kukilinda na kukihifadhi kituo hicho ili kiweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, hali ya upatikanaji wa dawa kwenye Hospitali zetu za Serikali imeimarika zaidi katika mwaka wa fedha 2009/2010. Kamati inaiomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kwamba dawa zote muhimu zinapatikana kwa wakati katika hospitali zetu kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 ili kukuza ustawi wa wananchi wetu.

Mhe. Spika, ukaguzi wa masuala ya jinsia katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii umefanywa na wataalamu walioshirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa malengo ya milenia, Wizara imefanikiwa kupunguza maradhi ya malaria kwa asilimia zaidi ya 99. Hayo yamethibitishwa na ripoti ya utafiti wa *Tanzania HIV and Malaria Indicator Survey (THMIS)* ya mwaka 2007/2008.

Mafanikio haya yamefikiwa kutokana na juhudi kubwa za Wizara kupitia zoezi la ugawaji wa vyandarua vyenye dawa maalumu ya kuuwa mbu waenezao malaria. Upigaji dawa ya kuua mbu waenezao malaria majumbani uliendelea kwa awamu ya tano katika Wilaya 4 za Unguja na Wilaya 6 za Pemba mwaka 2010.

Mhe. Spika, Kitengo cha Utumishi kilifanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi wa sekta ya Afya nchini. Taarifa ya wataalamu hawa inatarajiwa kuwasilishwa mbele ya Wizara katika mwaka wa fedha 2010/2011 na itasaidia sana kujua mahitaji halisi ya Wizara na kutafuta mbinu za kupunguza mapungufu ya wataalamu yaliyopo.

Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara kwa utanuzi wa Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya - Mbweni ambacho kimepata mafanikio makubwa baada ya ujenzi wa madarasa mawili, majengo mawili ya dakhalia na majengo mawili ya nyumba za wafanyakazi na kufunguliwa rasmi mnamo tarehe 23/3/2010.
Aidha, Kamati inaiomba Wizara kuwapatia nafasi maalumu ya mafunzo katika chuo hicho wanafunzi kutoka katika vikosi vya SMZ vinavyotoa huduma za afya kwa jamii.

Mhe. Spika, Kamati imefurahishwa sana na huduma zinazotolewa na Kitengo cha Macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, hasa baada ya kupata msaada wa vifaa vya kuchunguzia matatizo mbali mbali ya macho kutoka Serikali ya watu wa China. Aidha, ni jambo la fahari kwetu kuona kuwa wataalamu wetu wazalendo ndio wanaovitumia vifaa hivyo vya kisasa.

Tunashauri kitengo hichi kitafutiwe jengo lenye nafasi ya kutosheleza na kukidhi haja ya vifaa hivyo muhimu pamoja na kuimarishiwa wodi yake kwa ajili ya kuwalaza wagonjwa wanaoendeshwa operesheni.

Mhe. Spika, kwa msaada wa shirika la *Health Improvement Programme*, Hospitali ya Makunduchi ilifanya upasuaji wa mishipa kwa jumla ya wangonjwa 25. Hii ni hatua nzuri kwani imewaepusha wananchi wa kijiji hicho usumbufu wa kufuata matibabu hayo katika hospitali za mjini.

Mhe. Spika, Wizara kupitia Mradi wa Kupambana na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI imefungua vituo vipya 6 Unguja na 4 Pemba vya upimaji na ushauri nasaha ili kuviongezea nguvu vituo 36 vya awali kwa nia ya kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Upimaji damu kwa hiari unaendelea baada ya kampeni kubwa zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na Wizara.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, wagonjwa 67 wanaoishi na virusi vya UKIMWI walitembelewa na kupatiwa huduma majumbani mwao na akinamama wajawazito 30,311 walichunguzwa na kati yao 200 walionekana na virusi vya UKIMWI (VVU) na 158 kati yao walipewa dawa za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutokana na ushauri wa wataalamu.

Mhe. Spika, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi kwa mama na mtoto *(reproductive and child health services)* kwa mwaka 2009/2010.

Mikakati mbali mbali imebuniwa na Wizara, ikiwemo ya kuwaelimisha akinamama kujifungua katika hospitali au vituo vya afya vilivyo karibu nao. Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imetoa jumla ya vitanda vya kisasa 32 na mashine za kupimia mapigo ya moyo kwa watoto wakiwa tumboni.

Mhe. Spika, Kamati inaiomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kufikiria kwa kina mbinu mbadala na kuliondoa suala la kuchangia shilingi 40,000 kwa akinamama wanaohitaji kufanyiwa upasuaji wakati wa kujifungua. Kwa kweli akinamama hao huwa katika wakati mgumu na wanahitaji faraja kutoka kwa Serikali yao na jamii kwa ujumla. Hivyo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara hii kuondoa kabisa mchango huo ambao unawakatisha tamaa wananchi wetu, hususan wale wenye kipato kidogo kwani nchi nyingi duniani hutoa huduma hii bure.

Ingawa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii mara kwa mara huliarifu Baraza hili kuwa wazazi wasiokuwa na uwezo hawatozwi fedha hizo, Kamati imebaini kuwa ahadi hii haitekelezwi kiuhalisia.

Mhe. Spika, hospitali yetu ya Mnazi Mmoja inatoa huduma za utibabu katika kliniki maalumu kwa maradhi yaliyochaguliwa, ili kufanya wepesi wa huduma hizo kwa wananchi wetu kwa kuwatumia madaktari bingwa na wazoefu.

Kamati inashauri kliniki hizo ziendelezwe na zipatiwe jengo maalumu na vifaa vya kisasa ili kuweza kutoa huduma bora zaidi kwa nia ya kuweza kufikia pale ambapo wenzetu wa Hospitali ya Muhimbili wamefikia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita, Wizara imepokea jumla ya madai 89 ya fidia za ajali kazini. Kwa masikitiko makubwa, Idara ya Ustawi wa Jamii imeweza kulipa fidia za madai 11 tu na hivyo kuwabakisha wengi walioathirika kupigwa na butwaa bila ya kujua hatima yao. Kamati inaomba ufafanuzi wa sababu zilizopelekea Wizara kushindwa kuwalipa fidia wafanyakazi hao na lini watapatiwa malipo hayo.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, niwaombe sasa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na kuipitisha bajeti ya jumla ya shilingi 10,638,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 1,020,000,000/= kwa kazi za maendeleo kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa niaba ya Kamati yangu na wananchi wa Jimbo langu la Kwahani. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kutokana na makala iliyoandikwa na wataalamu watatu wa *WHO,Geneva,* akiwemo *A.F. Autunes,* G.*Carrin* na *David* B *Evans* kuhusiana na (*General Budget Support in developing countries ensuring the health sectors iterest*). Kutokana na maelezo ya wataalam hao kiujumla, misaada ya kibajeti yaani *General Budget Support* ilikusudiwa kutoa fursa kwa serikali kupitisha matumizi ya misaada kwa mujibu wa vipaumbele vya nchi. Waliendelea kueleza kuwa ilikuwa ni lazima kwa Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, kupata utaalamu na ujuzi unaohitajika kupata fungu lake katika hii misaada ya kibajeti (*GBS).*

Mhe. Spika, waliendelea kueleza katika makala hiyo kuwa Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, hupendelea sana kupata misaada ya kimiradi yaani (*Project*

Support Aid) kwa sababu huelekezwa moja kwa moja wizarani na haingiliwi sana na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Spika, hata hivyo Wizara ya Fedha na Uchumi huwapunguzia sana bajeti Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kisingizio kuwa wameshapatiwa misaada ya kimiradi. Mtaalamu huyo alitahadharisha katika makala hiyo kuwa Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, isikae kimya na kukubali nadharia hii kwa kutegemea misaada hii ya kimiradi na wakashindwa kujenga hoja kwa Wizara ya Fedha na Uchumikutengewa fungu katika lile fungu kubwa la misaada ya kibajeti ambapo italingana na vipaumbele vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Miradi mara nyingi ina vipaumbele vya wafadhili na kusita wafadhili wanapoondoa usaidizi wao.

Mhe. Spika, kwa kufupisha maelezo mwisho, wataalamu wanatoa wazo kwa Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, kuwa inapasa wawe na uelewa mzuri juu ya fungu hili la misaada ya kibajeti, uongozi wa Umma (*Public Administation*), maongozi ya Fedha (*Financial Management*) na mazungumzo ya kisera (*Policy Dialogue*) ili kujinyakulia fungu katika misaada hii. Mhe. Spika, yote haya yanahitajika katika kuongeza mfuko wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, katika Bajeti yake na hivyo kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, kwa ujumla wafanyakazi wa hospitali na vituo vya afya kuanzia madaktari mpaka wale wasaidizi wa wodini wakiwemo wauguzi,wakunga na wengineo katika vitengo mbali mbali wanafanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwengie yahatari. Vile vile wanahudumia wagonjwa wengi kiasi cha kuwafanya wasiweze kufanya shughuli nyengine kuengezea kipato chao. Hali ya mishahara ni duni kama ilivyo katika sekta nyengine za umma.

Mhe. Spika, tumeambiwa katika kitabu hiki kuwa Kitengo cha Utumishi, katika 2009/2010. Kimefanikiwa kutengeza *Scheme of Service*. Kwanza ningependa kumpongeza Mhe. Waziri kwa hatua hiyo aliyopiga ila matumainio yetu kuwa *Scheme of Service* hiyo basi ingekiwemo katika bajetti hii 2010/2011 na ingekuwa ni Hitimisho zuri ya awamu ya sita kwa wapendwa wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa hapa naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa uoni wake ni lini watumishi wema na wasikivu wa wizara yake watafaidika na mpango huo mpya?

Mhe. Spika, hali ya kuwatengenezea maslahi watumishi wa umma, siyo tu itazidisha ufanisi na kuwakwamua wafanyakazi hawa katika hali ngumu waliyonayo, bali pia itapelekea wataalamu wetu wakiwemo madaktari kubakia hapa Zanzibar kwa maslah ya nchi.

Mhe. Spika, hali ya kuondoka kwa wataalamu wetu yaani *brain drain* ni jambo la kusikitisha likichangiwa na mishahara midogo, mazingira magumu ya utendaji kazi, vitendea kazi pamoja na kukosa fursa za kuendeleza vipaji vyao, hupelekea wengine kuondoka nchini na kuacha mapengo makubwa. Hali hii pia inawakatisha tamaa hata wale Wazanzibari walioko nje na wao wangelipenda kuja kusaidiana na ndugu zao kulizungusha hili gurudumu husita kufanya hivyo.

Mhe. Spika, Kwa miradi ya maendeleo, mchango wa Serikali ni 1.02 bilioni tu ukiliunganisha na jumla ya billioni 9.085 zilizopangiwa. Hivyo mchango wa serikali ni asilimia 11.2 tu wakati fedha za wafadhili ni asilimia 88.8. Bajeti hii tegemezi kwa kiasi fulani inatia wasi wasi, kuhusan katika huu mtikisiko wa kiuchumi unaoendelea diniani. Pia nchi tunazozitegemea zenyewe au jirani zao wanakabiliwa na majanga mbali mbali ya kimaumbile yaani (*Natural disasters*), jambo ambalo linapunguza kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa misaada.

Mhe. Spika, kwa vile Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina muundo wa ngazi mbali mbali katika huduma zake, kuanzia kituo cha afya kule kijijini hadi kufikia hospitali ya rufaa. Ingefaa wizara ikafanya tathmini kwa njia ya kuongeza ufanisi wa hasa katika kuwapamdisha daraja wafanyakazi yaani (*promation*) na upelekaji wa zana na vifaa.

Mhe. Spika, kambi ya Upinzani imeingia moyo sana na kuvutiwa na mradi wa mabadiliko katika sekta ya afya, na mafanikio yake hivi sasa . Hata hivyo mapendekezo ya utekelezwaji wa mradi huo unapaswa usionekane kinadharia pekee, bali uwe wenye kutekelezeka na usimamiwe ipasvyo.

Mhe. Spika, nasema haya kwa vile utekelezaji wa mradi kama huu, huwa unakumbwa nachangamoto nyingi hasa wakati wa kupanga bajeti, kwani wataalamu wanailezea bajeti kuwa ni ni utaratibu wa serikali kugawanya mapato na hazina za nchi katika hali ya usawa. Hivyo sera za kibajeti huelekeza kule kuondoa upendeleo katika jamii zake.

Mhe. Spika, moja kati ya changamoto ni vile Zanzibar imebahatika kuwa na visiwa viwili unguja na Pemba, jambo ambalo linatoa changamoto za aina yake katika utekelezaji wa sera za wizara katika uendeshaji.

Mhe. Spika, je namna hospitali tafaoti kati ya Unguja na Pemba zinavyoshughulikiwa na kupatiwa nyenzo kuna muelekeo wa usawa? Afisa mdhamini aliyeko Pemba jee ana uwezo gani, unatosheleza kuzisghulikia kero za Pemba na mahitaji yao. Jee anashirikishwa kiasi gani katika maamuzi na Uongozi wa Wizara na uwezo wake wa kusimamia maamuzi hayo ukoje?

Mhe. Spika, sina wasiwasi na uadilifu wa Mhe. Waziri katika hili, lakini napenda kulizindulia tu ili hayo mabadiliko ya sekta ya afya yawe ya kweli na endelevu.

Mhe. Spika, katika kutoa mfano wa suala hili ninalolizungumzia wako madaktari bingwa wa hospitali ya Mnazi Mmoja wameanzisha ziara za kwenda Pemba na kuwashughlikia wagonjwa huko.

Hili ni jambo la kupongezwa sana lakini pia kwa Uongozi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wamelipa uzito gani na wanawezesha kwa kiwango cha kuridhisha kumudu safari hizo na kujikimu? Jee Wizara haioni kuwa ni moja wa ufumbuzi wa kuleta uwiano wa huduma kati ya Unguja na Pemba wakauchukua yaani kuu-(*ADOPT*) utaratibu huu na kuufanyia kazi ili uweze kuingizwa katika sera za wizara.?

Mhe. Spika, usambazaji wa wafanyakazi, wahitimu na wataalam mbali mbali wakiwemo madaktari ungetarajiwa uwiane kati ya Unguja na Pemba na kati ya vituo vya afya na hospitali hadi hospitali ziliomo katika wilaya mbali mbali.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa ukitoa hudma duni katika vituo vya afya, unakaribisha msongomano katika hospitali za wilaya. Hivyo hivyo ukitoa hudma duni katika hospital za wilaya unakaribisha msongomano katika hospitali ya rufaa.

Mhe. Spika, kutokana na udogo wa nchi yetu na yale ambayo nimeyazunagumza hapo juu, ni dhahiri kuwa ushughulikiaji na upelekaji wa zana na vifaa katika vitengo mbali mbali ni muhimu sana, liratibiwe ipasavyo na bajeti izingatie mapungufu yote yaliyopo.

Mhe. Spika, mahitaji ya hospitali yangepaswa kupewa uzito wa juu katika matayarisho ya bajeti. Upatikanaji wa zana na vifaa pamoja na matengenezo (*maintenance*) ya vitengo mbali mbali ingefaa zikatajwa wazi wazi (*specific*) katika bajeti.

Mhe. Spika, ingefaa zikagawanywa katika utaratibu ambao fedha inapopatikana tu zinaelekezwa panapohusika:

- vifaa vya wodi yakiwemo magodoro, mashuka vitanda na vifaa vya usafi
- vifaa vya kliniki vikiwemo fanicha na zana husika
- vifaa vya Tiba (*medical supplies*)
- madawa

- zana za uchunguzi zikiwemo zana za maabara, *X-rays, Ultra Sond* na nyenginezo na matengenezo yake.
- Majengo ya hospitali na vituo vya afya.

Mhe. Spika, ingefaa Wizara ikatoa uchambuzi katika maeneo haya, kwani hali halisi inayotokea ni kuwa kila mwaka kuna maeneo yanaangaliwa na mengine hayaangaliwi wakati maeneo yote hayo yana umuhimu wake katika huduma ya matibabu. Pia fedha inayopatikana inapokuwa ndogo mijadala ya wapi zielekezwe inakuwa myepesi.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa upatikanji huu wa vifaa na zana mbali mbali unakuwa endelevu, waziri anahitaji kuupatia uongozi maalum ambao utawajibika katika upatikanaji na matengenezo ya vifaa (*supply and maintenance*).

Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na serikali kwa jumla, kwa kusambaza vituo na kujenga nyumba za wauguzi na madaktari, Unguja na Pemba. Hata hivyo ili kutowavunja moyo wananchi mapema wizara inabidi ijipange vizuri kwa upelekaji madaktari, wauguzi na vifaa ili huduma zitakazotolewa ziweze kukidhi haja kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, katika fani ya matibabu hapa Zanzibar pamoja na mafanikio yaliyopatikana matibabu ya wale waliovunjika mifupa (*bone Fractures and cracks*) bado wanakabiliwa na matatizo makubwa.

Mhe. Spika, ukosefu wa madaktari wataalamu yaani (*Orthopaedic Surgeous*) katika hospitali nyingi na hata Mnazi Mmoja pamoja na sehemu finyu katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja inaleta usumbufu mkubwa kwa wagonjwa.

Mhe. Spika, bado hospitali za Pemba zinalia kuhusu chumba cha Dharura (*ICU*). Mhe. Waziri katika miaka mitano hii niliyokuwemo katika Baraza hili haoni taabu kumweleza kuwa imeshindikana.

Mhe. Spika, bado Hospitali ya Wagonjwa wa Akili iliyopo Kidongo Chekundu inahitaji mashughulikio. Lakini pia wananchi wa Pemba wanataka wizara kujenga hospitali ya wagonjwa wa akili huko Pemba, ili kuwapunguzia siyo gharama tu bali hata usumbufu.
Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza katika hotuba yake kuwa hospitali hii ya wagonjwa wa akili inatarajiwa kujengwa katika eneo la Hospitali ya Wete. Ujenzi huu uko lini na ulifanyiwa utafiti wa kitaalmu kuwa wagonjwa hao wa akili na matibabu yao hawataathirika kwa kuwa karibu na hospitali ya kawaida, na upande mwengine huduma katika Hospitali ya Wete na shughuli zake

hazitoathirika na kuweko kwa wodi za wagonjwa wa akili. Naomba Mhe.Waziri atupatie ufafanuzi.

KINGA NA AFYA YA JAMII

Mhe. Spika, tunatoa pongezi za pekee kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa namna walivyolivalia njuga suala la Malaria na homa za matende na mafanikio yake yanaonekana wazi wazi. Hata hivyo ingefaa tukapunguza utegemezi wa nje kidogo kidogo ili mafanikio haya yawe endelevu.

Mhe. Spika, ingefaa pia maradhi ya kichocho yakapata ushughulikiaji wa kina kwani watoto wengi huathirika na maradhi haya.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la maradhi ya sukari, saratani na presha ingefaa wizara ikaanzisha utafiti maalum, kama kuna sababu zozote na kuweza kupunguza uweneaji wa maradhi haya badala ya kungojea matibabu.

Mhe. Spika, moja kati ya nyenzo kubwa ya afya ya jamii ni usafi. Napenda nimuulize Mhe. Waziri anachukua hatua gani na wizara inashirikiana vipi na mabaraza ya miji, manispaa na halmashauri za wilaya katika kuhakikisha kuwa miji ni safi kuzuia usambazaji wa maradhi. Pia wizara inajihusisha vipi katika kuelekeza utupaji wa taka katika kulinda afya za watu. Kwa sababu wizara ndiyo inayobeba mzigo wa matibabu yakitokea maradhi ya mripuko, kutokana na uchafu wa maeneo hivyo ni mdau mkubwa wa kuona kuwa miji yetu na vitongoji vyake iko katika hali ya usafi.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza wizara, kwa kuendelea kuiunga mkono *PHL* yaani (*Public Health Laboratory*) iliyopo Wawi na tungelioomba Wizara izidi kuitumia maabara hii kwa tafiti zake na kutoa mkazo wa aina yake wa kuijengea uwezo wa utaalamu na zana izidi kuchukua sura ya Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, naomba sasa nichukue fursa kuzngumzia juu ya Chuo cha Sayansi ya Afya, Mbweni. Chuo hiki kina umuhimu wa pekee siyo katika kutoa taaluma ya afya tu hapa Zanzibar, bali pia inaokoa mamilioni ya shilingi ambazo zingehitajika kuwasomesha vijana wetu nje ya Zanzibar, lakini pia inajenga tanswira pekee juu ya hali ya kujitegemea kwa Zanzibar, katika sekta ya afya kuwa na taasisi inayotoa taaluma ya ngazi ya chini na ya kati, ambao ndiyo kada zinazohitaji wafanyakazi wengi.

Mhe. Spika, tunapongeza sana juhudi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kupata wafadhili kwa utanuzi wa chuo chenyewe, ikiwemo maabara

nzuri ya chuo hicho. Tunawashukuru sana wafadhili wetu hasa Serikali ya Oman.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Wizara inayo hatimiliki ya eneo la Chuo bado imeliachia kuvamiwa na baadhi ya wananchi, jambo ambalo linarudisha nyuma utanuzi wa chuo hicho. Mhe. Waziri ana mkakati gani wa kuhakikisha maeneo yake anayarudisha katika milki ya chuo.

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya utaratibu wa kuingiza wanafunzi yaani (*Admission*), ambapo inasemekana kuwa baadhi wanaoingizwa ni wale wenye viwango vidogo vya kufaulu au hata madarasa ukilinganisha na wale waliofanya usaili kwa jumla. Hali hii inadhihirika pale Kamati inapokwenda ikakuta darasa lina vijana 100 badili ya 40.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri aunde Kamati maalum akishirikiana na Bodi ya Chuo na wataalamu wengine kufuatilia tatizo hili kabla halijaota nabu na tukashindwa kulishughulikia.

Mhe. Spika, weye ulikuwa shahidi wakati ulipoletwa mswada wa kuanzisha Chuo cha Habari, ambapo mimi nilipendekeza kuwa kwa ajili ya kupunguza gharama na ufanisi, chuo hicho kisiwe cha kujitegemea lakini kuingizwe kama ni *College* ya *SUZA*.

Mhe. Spika, wizara na serikali kwa jumla ingefaa ikafanya utafiti kutokana na udogo wa nchi yetkuna haja ya kuwa na vyou vingi vidogo vidogo na kila kimoja kina bodi yake au viwe katika mwamvuli wa *SUZA* na bodi moja? Utafiti huu unahitajika. Pia Mhe. Waziri angeliushauri uongzi wa chuo kukiunganisha na chuo chengine duniani ili kunufaika na mitaala yao lakini pia hata utaalamu.

Mhe. Spika, jambo jengine la kusikitisha lililotokezea hapo chuoni ni kuwa mnamo mwezi wa nne 2010 ilipangwa kozi ya *PHNB* kwa ajili ya wafanyakazi 38 Unguja na Pemba chini ya manesi kunyanyua viwango vyao.

Kwa ubinafsi wa baadhi ya viongozi wa chuo hiki cha Sayansi ya Afya, wakachukua wanafunzi ambao si wafanyakazi, darasa likawa na wanafunzi 57. Kwa ubinafsi huo darasa hili limevurugika na kila mmoja amesharudi alikotoka. Pia Kitengo cha Mafunzo kama kilivyoelezwa katika uk.10-13 kingepaswa kuwajibika ipasavyo kwa nini kozi ya mafunzo kazini ivurugwe na watu wachache.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri afuatilie kwa kina suala hili ikiwa ni pamoja na kuundwa hiyo Kamati kuchunguza mazingira yaliyopelekea kutokea hivyo.

Mhe. Spika, pili namuomba Mhe. Waziri aimarishe Kitengo chake cha mafunzo kazini ili bado kukawa na haja ya kukitumia chuo hiki cha afya kunyanyua viwango vya wafanyakazi wa kada zote za afya ikiwa ni pamoja na kunyanyua utendaji wao wa kazi yaani (*Capacity building*) na azuie kabisa uwezekano wa mafunzo kuharibiwa na ubinafsi wa watu wachache.

Mhe. Spika, Kwa vile Mhe. Waziri amekiri katika hotuba yake ya kufuata malengo ya Millenia kuhusu mama na watoto. Umefika wakati sasa wizara kuangalia upya suala la kuchangia mzazi operesheni kwa kulipa 40,000/-. Operesheni hii ni ya dharura, haipangwi wala siyo kama operasheni nyengine ambayo mgonjwa anashauri, huu ni uamuzi wa daktari kwa kuokoa maisha ya viumbe viwili. Jee kumlipisha mzazi katika kipindi kama hiki ni vizuri, pamoja na bejeti finyu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi kwa nini suala hili wizara yake ina kigugumizi.

Mhe. Spika, kuna idadi kubwa ya wazazi wanafanyiwa operesheni katika ukurasa wa 120 kiambatanisho 5.3 katika hospitali ya Mnazi Mmoja kinamama wajawazito waliolazwa 7,445 na waliozaa kwa njia ya kawaida 4,933 na kwa operesheni 2,572. Mhe. Waziri una maelezo yoyote juu ya yale yanayopelekea idadi kubwa hii ya wanaofanyiwa operesheni za uzazi.

Mhe. Spika, kutokana na malengo ya Idara ya Kupambana na Madawa ya Kulevya na Kurekebisha Tabia, idara hii isingepaswa kuwekwa katika wizara hii ya afya. Mhe. Waziri angejitahidi kujipapatua ili wizara yake ibakishe na jukumu moja tu, la kutibu na kurekebisha tabia kwa waathirika wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwa sababu vita dhidi ya madawa ya kulevya inakusanya vyombo vya dola, Tawala za Mikoa, taasisi za bandarini na viwanja vya ndege. Kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii siyo kwa mzigo huu ni mzito sana kutokana na uwezo wake bali hata shughuli zake ni nyingi sana na za msingi.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri achangamke na sisi tunaiambia serikali iwapo wako makini kupambana na madawa ya kulevya, Afisi ya Waziri Kiongozi iubebe mzigo huu. Waziri Kiongozi ndiye anayeunganisha shughuli zote za serikali.

Mhe. Spika, kuendelea kulibakisha suala Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni kujindanganya na kuliachia hakutoondoa ukweli kuwa si pahala pake.

Mhe. Spika, ningelipenda kumaliza maelezo ya kambi ya upinzani kwa kusema kuwa pamoja na maeneo mengi ambayo yamo katika Wizara ya Afya ya Ustawi wa Jamii si rahisi kuyamaliza yote lakini naamini waziri ameielewa hotuba ya kambi ya upinzani.

Mhe. Spika, jambo zuri ni yale matumaini yetu kwa wizara hii, kuwa katika kipindi cha miaka mitano ambayo mimi nimekuwa kama Waziri kivuli nnavyoiangalia hali inavyokuwa ya kuridhisha mwaka hadi mwaka. Naweza kusema kuwa kuna upepo wa mabadiliko katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kunakoleta matumaini kwetu na kwa wananchi kwa jumla. Kwa hili nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote hadi kufikia wale wanaosaidia wodini. Tunaomba moyo huu udumishwe na kuendelezwa kwa maslahi ya umma.

Mhe. Spika, kwa sababu baadhi ya matibabu kwa maradhi kama presha ni utulivu, tunawaomba wananchi wote kushiriki katika kura ya maoni ya kuleta mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuiunga mkono hoja hiyo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Namshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, leo ni siku ya Ijumaa siku tukufu kwa Waislamu wote. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri pamoja na Naibu Wake, Katibu wake, Wakurugenzi wake pamoja na wahudumu wote wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, kabla sijaingia kwenye hotuba ya Mhe. Waziri, naomba nipeleke sifa za pekee kwa Mhe. Waziri leo katuonesha jinsi ya usomaji wake wa hotuba kitabu kikubwa na mambo mengi, lakini kakisoma kwa muda mchache. Hilo nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kuna jambo ambalo linahusiana na hospitali. Jambo hili kidogo nimeona nilisemee kwa wepesi na mwanzo nianze kabla sijaingia kwenye kitabu, suala ambalo Mhe. Spika, tunamuomba Mkurugenzi muhusika ile milango kweli tunaifurahikia, wametia mageti pale ni vizuri kutokana na kuzuia vibaka tunakubaliana nalo, lakini kidogo lina matatizo ya kufungwa milango yote ikabakishwa mmoja. Kwa sababu binaadamu linaweza likatokezea jambo la aina yoyote, badala ya kuokoa basi tukahatarisha maisha mabaya. Unafunguliwa mlango mmoja tu wa kwenye ngazi upande ule wa *maternity*, halafu kuliko bakia kote kunafungwa. Kule kila tukiwatizama walinzi mnao wengi basi ningeomba tu Mhe. Spika, kwa kupitia kwa Mhe.

Waziri awapange wale kwa sababu idadi kubwa ya wale walinzi wako wengi, basi wangewapanga kile geti wawili wawili inatosha kutokana na ile idadi waliyokuwepo. Lakini kufungwa milango yote Mhe. Spika, ni kufanya hatari.

Mhe. Spika, niingie kwenye kitabu kwenda kuchangia. Nianze kuchangia kwenye sehemu ya Idara ya Utumishi. Mhe. Spika, kama tulivyoelezwa hapo kwenye ukurasa wa 9 huu. Mhe. Spika, mimi siku zote hapa huwa nasema, lakini sipendi kumpa lawama sana Mhe. Waziri kwa sababu hana vianzio vya fedha vya kuweza kuwasaidia kuleta vifaa vingi hospitalini pamoja na mishahara ya wafanyakazi wake. Mara nyingi sana huelekeza kwenye serikali, hususan waziri muhusika ambapo mara nyingi sana hupeleka lawama huko.

Mhe. Spika, sasa hivi pamoja na mabadiliko yote ya mishahara tunayoambiwa kila siku, kwenda na kurudi bado Mhe. Spika, kwa wizara hii haijatosheleza. Mhe. Spika, wizara hii tulitegemea kuwa na wataalamu wengi sana, lakini kwa bahati mbaya tuna wasomeshaji wazuri tunawapeleka kusomeshwa, lakini hatimaye wanatutoroka kutokana na mishahara haikidhi haja.

Mhe. Spika, tukiwaangalia wenzetu Tanzania Bara, utakuta wenzetu sasa hivi wanapata mafao makubwa kabisa na ndio vishawishi vya wenzetu, wanaambizana Mhe. Spika, hawa kwamba eeh bwana mimi nimemaliza kozi juzi na sasa hivi nina Phd au nina diploma, lakini napata mshahara kiasi kadhaa. Sasa akiangalia huku Mhe. Spika, dokta anapata mshahara Shs. 400,000/= mpaka Shs.500,000/= na kule keshaambiwa kuna milioni 1,500,000/= na mapukupuku juu, gari na kila kitu pamoja na nyumba nzuri kwenye ukanda wa Osterbay, hivi kweli atakaa Zanzibar hapa labda kwa Mtipura. Suala hili linakuwa sio kitu rahisi sana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tungeomba kwa kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, hebu hili suala la marekebisho ya mishahara, Mhe. Spika, liangaliwe kwa kina kabisa. Mhe. Spika, utakuta *orderly* mshahara wake ni mdogo kabisa wala haukidhi haja na kazi zao nyingi wanafanya za usafi. Vile vile *nursery* naye mshahara wake ni mdogo kabisa haukidhi haja, suala hili linasikitisha tena sana Mhe. Spika.

Suala hili Mhe. Spika, siku zote tunalisemea, sijui kwa nini tunakuwa hatusikilizwi kwa sababu tunayaona yale mambo kwa hali halisi. Mhe. Waziri Kivuli kasema sasa hivi kuwa wataalamu wanatukimbia, mimi namuunga mkono mia kwa mia. Nina wataalamu nawahisi na ninawaona kila siku nikienda. Alizungumzia suala la mifupa ya miguu.
Mhe. Spika, mimi nilikuwa na dokta wangu mmoja mzuri sana nikimpigia simu tu mtu kakatika mguu, basi nikimpeleka kule anamsaidia. Juzi naambiwa na utu uzima wake kenda kachukua maberemende kwenye bega, kawa *brigadier* sijui

nani. Ni *specialist* wa mifupa, ndio tumeshamkosa sasa hivi. Amehiyari kwenda kule kuteswa, kuteswa kwake kuna manufaa. Maana yake kenda kule kapindwa, maana yake huwezi kwenda kule kupewa cheo bila ya kufanya *training* yenyewe ile, lakini kahiyari hivyo. Lakini nasikia *training* yenyewe ni vichekesho, anakwenda asubuhi kisha jioni anapigiwa simu anaambiwa kuna ajali imetokezea, si ndio kawaida ya Bara kwa sababu kule magari mengi, anaambiwa mzee unapata kupumzika. Anaendelea tena hivyo hivyo, hivi sasa tayari keshakuwa kamanda mkubwa begani vitu anavyo, ndio tumeshamkosa huyo. Tumekosa kwa sababu gani, ni sababu mshahara kidogo.

Sasa suala hili na mimi siku zote nasema Mhe. Waziri simtii lawamani nitamtetea, hana vianzio vya fedha, kwa sababu angekuwa na vianzio vya fedha kutokana na hali ya hospitali alivyoitengeneza, basi asingeweza kuwalipa wafanyakazi wake, anajitahidi kwa kila aina ya *project*. Mhe. Waziri katafuta wafadhili wa kila aina. Huo mwili msione mambo ni mnene lakini mwembamba kutokana na kuhangaika, anahangaika kutafuta fedha.

Leo tizama jengo lile pale *Alhamdulillah* linang'ara, ukweli tuseme tusifiche. Lakini Mhe. Waziri hana fedha jamani, wafanyakazi tusimlaumu waziri. Tuitizame serikali kuu ndio kutokana na kuwa ndio yenye vianzio vya fedha ili vimpe yeye. Pengine hii bajeti aliyoitaja humu asiipate kwa asilimia mia kwa mia, sasa ndio zaidi nalo kuwa gumu. Ataiandaa bajeti yake nzuri, lakini lengo anakuwa hafiki. Hatimaye tunasema waziri au katibu, wapi katibu atapata fedha wapi.

Kuna siku moja nilikwenda kule hospitali ya Muhimbili Mhe Spika, nilimpeleka kijana mmoja alikuwa na matatizo ya mkojo, nikaambiwa mbona nyinyi mna *professor* kule mzuri tu, mimi nikafanya kama simjui nani, yule Dkt. Moh'd Saleh Jidawi, niliwaambia hivi sasa Katibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa sababu hatuna fedha za kumlipa ndio tumempa cheo cha ukatibu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye ukara wa 16 Kitengo cha Ufundi. Kwa kweli nawapongeza sana na hasa wakati *lift* yetu inapokwama, hawa ni mahodari sana na wanakuja kwa haraka sana. Lakini katika ufanyaji wao kazi wanahatarisha maisha yao, sasa hakuna *allowance* kutokana na zile kazi zao za hatari.

Mhe. Spika, nimejaribu kutafuta sana kwenye kitabu sikuliona suala hili la *lift*, lakini namjua Mhe. Waziri kwa jitihada zake hili atalifanya. Kwa mfano, watu wengine wanakuwa na uzito mkubwa na leo kama vile mimi nianguke hapa na Mwenyezi Mungu aepushie mbali, hivi ataniweza nani kunibeba kwa ajili ya kunipeleka juu na uzito wangu 110, sasa nitakwenda vipi kule.

Kwa kweli watu wengine ni wazito sana, yaani utamkuta mtu anapata tabu na kufika kukodi watu kwa ajili ya kumbeba na hali hiyo inasikitisha. Mhe. Spika, jirani yangu hapa ananiambia na Mhe. Naibu Waziri naye pia mnene, lakini huko siko. Lakini suala hili tulione na tuweze kuweka *lift* mpya kwa sababu Hospitali yetu ni ya Rufaa.

Nikiendelea sasa niende kwenye ukarasa wa 34 Kitengo cha Macho. Mhe. Spika, kitengo hiki nakipongeza sana na vile vile niseme ni muokozi, kwa sababu wanaingia mpaka kwenye vijiji.

Kwa mfano, leo wazee wetu wamerudi ujana wanavaa miwani wakati zamani walikuwa hawaoni. Lakini kutokana na jitihada zao hao wanakwenda mpaka vijijini, kwa ajili ya kuwapa huduma mbali mbali zikiwemo kuwapima, dawa, miwani na hata kuwafanyia *operation*, tena *operation* wao ni rahisi sana.

Kutokana na hali hiyo, wanakuwa wanachangia zile huduma, kwa sababu kuna vitu vyengine lazima tukitaka tusitake huduma nyengine lazima tusaidie na wala tusisubiri fungu la serikali liingie pale. Kwa kweli zile fedha wanazokusanya sio kama wanatia matumboni, isipokuwa wanafanya mambo madogo madogo wananunua kama vile rangi, mashukaa na magodo hupatikana jambo kidogo na kupelekwa kule. Kwa hivyo, nakipongeza sana kitengo hiki.
Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alisema kuhusu suala la kutafutiwa eneo mimi naunga mkono. Hivi sasa kweli watu wengi wamekuwa wanaumwa na macho na wala sijui kwa sababu gani. Kwa hivyo, hili nalo naomba lifanyiwe uchunguzi Mhe. Waziri, kwa nini macho yanakufa nuru, mimi sijui vipi au hatuna *vitamin*, lishe yetu ndogo ama vyakula tunavyokula havina rutba au vyakula tunavyokula *chemicals* nyingi.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 43 kwenye Hospitali ya Mnazimmoja. Mhe. Spika, *ingeneral* hospitali hii kuna mambo mbali mbali yenye matatizo. Kwa mfano, *X-Ray*, wafanyakazi wote wameshaathirika na mionzi naweza kusema hivyo, kwa sababu ile mionzi inaathiri na wala sijui kama kuna fungu maalum la kuweza kuwakimu, jambo kubwa utaambiwa wanapewa maziwa lita moja na wala haitoshi.

Mhe. Spika, lita moja ya maziwa haijafanya uondoe yale matatizo ya mwili, kwa sababu sumu inaenea ndani ya mwili mzima kutoka na ile mionzi yenyewe. Kutokana na hali hiyo, siku zote wafanyakazi wale wanakondeana tu, kwa hiyo lita moja ya maziwa haijasaidia.
Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kama kawaida yake aombe, ili angalau kuwe na fungu maalum la kuweza kuwahudumia wale, kwa sababu kazi zao zinahatarisha afya zao. Kwa ujumla sio wafanyakazi wale wa *Department* ya *X-Ray*, isipokuwa ni wafanyakazi wote wa Hospitali ya

Mnazimmoja kuanzia *Orderly*, *Nurse* pamoja na *Doctor* kazi zao za kuhatarisha afya zao.

Mhe. Spika, suala hili tulione pamoja na kwamba bajeti ndio tayari imeshapangwa, lakini tuone kuwa kuna haja ya kupelekwa fungu la dharura kwa ajili ya kuwasaidia na kuwaondolea matatizo hayo.

Vile vile kwenye suala la vifaa vya kisasa. Kwa mfano, *Ultra Sound* ziko mbili na jambo hili kila siku nalizungumza kwamba ile *Ultra Sound* moja kioo kimekufa na thamani yake tunaambia shilingi milioni 6. Mhe. Spika, hivi kweli mashine nzima na tatizo ni kioo tu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba azungumze na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughuliki Masuala ya Fedha, ili amtilie fedha kwa haraka sana kwa lengo la kukibadilisha kile kioo na kuweza kuitumia mashine ile, kwa sababu kila siku inaingia mavumbi pamoja na *virus* na itafika pahala mashine ile itaharibika.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 56 Humuda katika *Clinic* Maalum. Mhe. Spika, watu wengi hivi sasa wanasumbuliwa na Maradhi ya Sukari, lakini humu sikuona neno la kitengo isipokuwa tumetiwa kwenye kundi la jumla jamala.

Kwa kweli wagonjwa wenye Maradhi Sukari hatukutendewa haki, kwa sababu nilifikiria tutakuwa na nafasi ambapo kimeandikwa Kitengo cha Huduma na Matibabu ya Sukari, matokeo yake tumetiwa kwenye sehemu ya Huduma katika *Clinic* Maalum, yaani tumeingizwa tu nadhani tumedharaulika.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia Katibu Mkuu wake suala hili kuhusu sisi Wagonjwa wa Sukari tupewe kipaumbele angalau tuweze kujisikia, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tunataka kuomba kwenu, ili muweze kutusaidia. Kwa mfano, juzi Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu ameomba ardhi kwa ajili ya kuweza kuwa na kitengo chetu.

Kwa hivyo, suala hili naomba Mhe. Waziri alifuatilie, kwa lengo la kutusaidia na sisi tuweze kujitenga, kwani ile sehemu tuliyopewa ni ndogo sana na wala haitoshelezi pale, kwa sababu wagonjwa ni wengi sana mpaka wengine wanasahau zile tarehe wanakwenda sio wakati waliopangiwa.

Lakini wale madaktari ni wazuri kupitia daktari wao mkuu basi wanahudumia, pengine ukiuliza daktari yule analipwa kiasi gani na kuambiwa shilingi 300,000/- usishangae ndio kawaida yetu hiyo. Kwa kweli jitihada zake anazifanya na Mwenyezi Mungu amjaalie na ushujaa wake aendelee kukaa pale

na asijekutukimbia, kwa sababu akitukimbia basi wagonjwa wa sukari tumeumia.

Mhe. Spika, kama nilivyosema sitokuwa na mchango mkubwa nikiendelea niingie kwenye ukurasa wa 59 kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii. Mchango wangu nataka nimalizie hapa, kwa kweli idara hii labda Mhe. Waziri anaweza kunisaidia, kwa sababu sijui ushahidi gani tuutoe kuhusu mgonjwa huyu ameshapona na wala hana mtu anatakiwa alelewe.

Mhe. Spika, leo kama si Mhe. Waziri wangu kumpenda basi ilikuwa niondoe shilingi kwenye kifungu hiki, kwa sababu ninayo masikitiko makubwa sana. Kwa mfano, mgonjwa wa kwanza nilimchukua hana mtu, isipokuwa jamaa zangu kutoka nyumbani huko bara nilikwenda na nikamuuguza na kupona, yaani nilikwenda mimi mwenye binafsi yangu kunakohusika na mkuu wenyewe anayehusika nilikutana uso na macho.

Kwa hivyo, nilimueleza kwamba huyu mtu hana kwao na baba yake ndio mimi, lakini hivi sasa nimeshamuuguza isipokuwa naomba mnisaidie au mnatumia sheria gani, basi nilifahamishwa zile sheria na nikagundua kuwa zote hazimhusu.

Kwa kweli yule hana jamaa wala mtu yeyote na kule amekwenda kujenga nyumba tu, kwa sababu na mimi mwenyewe nafuatilia pamoja na kuuliza jamani huyu mgonjwa nampeleka hospitali, lakini nani atanifuta nyuma, naambiwa wewe mwenyewe peke yako si unataka kura, hatimaye ndio hali kama hiyo, mashahidi *Nurses* kwenye Wodi ya Maradhi ya Homa.

Mhe. Spika, hivi sasa nimekuwa maarufu pale, sasa mimi nikisema naitwa *doctor* kwa sababu gani, kutokana na falsafa hiyo sijapata kuiona ya kuhudumia wagonjwa na hiyo mtaijua wenyewe. Lakini hali hii inasikitisha sana Mhe. Spika, kwa sababu nimeuguza na amepona na hatimaye amekufa pale pale na wale *nurses* wananitania leo Mheshimiwa maiti huyu tutakufunga mgongoni, ili umchukue sasa 5:00 za usiku niko hospitali na wala sijui nimpeleke wapi maiti yule.

Kwa habati nzuri kuna watu wasamalia mwema kwa siku ile nikawapata wakaja kumchukua saa 7:00 za usiku na kunipelekea sehemu huko na tukaomba na kuweza kumzika.

Vile vile hivi juzi hata wiki haijatimia nimepeleka mwengine ambaye nilikwenda kumchukua saa 5:00 za usiku nikatibiwa kwenye gari na wale wakanikimbia na kwa bahati Mwenyezi Mungu akajaalia askari wakawakamata jamaa wale, kwamba hivi mnavyosanya sivyo Mheshimiwa saa 5:00 za usiku

mmemuamsha na hivi sasa mgonjwa huyu mnataka kumkimbia basi tutakutieni ndani, baada ya kutishwa ndipo walipokubali wakaingia kwenye gari.

Lakini nilipofika kule hospitali baada ya kwisha kumuweka wodini na kutoa fedha za kusaidia kwa ajili ya chai, basi sikuwaona tena na mgonjwa alitibiwa, yaani amepimwa vizuri na niliambiwa *pressure* hana na hivi sasa mchukue mtu wako.

Mhe. Spika, nikaangalia nimchukue nimpeleke wapi, kweli nimeomba kura lakini nimpeleke wapi. Kwa hivyo, nilikwenda kunakohusika kwa Sheha na kuchukua barua kama utaratibu ikapelekwa, Mhe. Spika nimehangaishwa na matokeo yake hivi sasa amekufa na wamemzika wao wenyewe, yaani amekufa kwa njaa na wala sio kwa kuumwa, niseme ukweli. Kwa kweli mimi na *nurses* kwa mfano, leo nakosha mimi na kesho wanakosa *nurses. (Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awatafute wale *nurses* kwa ajili ya kuwapa vyeo pamoja na elimu ili waweze kuhudumia vizuri zaidi, kwa sababu walimtibu mpaka amefika pahala amepona, isipokuwa amekufa kwa njaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia suala hili ndilo ambalo nimenifanya nitake nizuie fungu kwa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika amrekebishe mhusika, ili wakati mwengine tusizungumze haya tena, kwa kweli si vizuri Mhe. Waziri wangu kumpiga buti, yaani naona tabu kabisa, kwa sababu ananisaidia mambo mengine sana *Alhamdulillah* na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atambariki kama liko ambalo analiomba zuri, basi Mwenyezi Mungu atamjaalia. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. (*Makofi)*

Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nami niweze kutoa mchango kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha bajeti yake kwa muda mfupi tena kwa ufanisi mkubwa. Kwa kweli ameonesha uwezo mzuri na kwa haraka tumefahamu na amemaliza mawasilisho yake.
Lakini nimlaumu kwa sababu nimefanya uchunguzi wa haraka wagombea wengi wa Urais Zanzibar *Doctors* hawamo. Kwa hivyo, ningependa na yeye angechukua fomu basi ingekuwa vizuri na kutuongoza hapa Zanzibar. *(Kicheko)*

Kwa kweli madaktari wanarejesha nyuma kwani hawataki kuchukua nafasi za kisiasa. Lakini Mhe. Waziri angechukua nafasi hii basi bila ya shaka Wazanzibari CCM wangempa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze na Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni, kwa kusema napongeza maamuzi ya serikali kwa kuanzisha chuo kile, kwa lengo la kuweka wataalamu hapa nchini na kuondosha tatizo la madaktari pamoja na wataalamu wengine.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapotoa malalamiko wanakuwa na lengo la kuelekeza, kutoa ufanisi kwa serikali pamoja na wananchi kwa jumla. Kwa hivyo, kwa sababu sisi hatuishi mbinguni wala hewani isipokuwa tunaishi na wananchi wa Unguja na Pemba. Sasa tunapoyasikia mambo basi hulazimika kuwaambia mawaziri pamoja na serikali, ili serikali iweze kufanya uchunguzi na wakiona kuna tatizo waweze kurekebisha.

Kwa kweli Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni, Mhe. Rashid Seif Suleiman (Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii) alizungumza malalamiko yake, kwamba kuna matatizo ambayo yanazungumzwa, yaani Wazanzibari wanasema chuo kile kina matatizo hasa katika fursa za kuwapata wanafunzi wanaotaka kusoma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba malalamiko ni ya wananchi ambao ndio wenyewe nchi hii wenye kuendesha uchumi wa nchi hii. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri asidharau ni vyema tungeunda tume kwa ajili ya kuchunguza malalamiko haya, ikiwa hakuna tatizo basi tumeisaidia serikali, lakini kama kuna tatizo wananchi wafanyiwe haki.

Wazanzibari wengi wanalalamika kwamba fursa za kuingia wanafunzi chuo pale haziendi kama inavyotakiwa, kwa sababu wapo wanafunzi walioomba ambao wenye sifa za *credit* tatu wameachwa, lakini kuna wanafunzi walioomba ambao hawana sifa ndio walioingizwa. Kwa hivyo, haya ni malalamiko ya wananchi, sasa kama ni malalamiko najua atakapokuja Mhe. Waziri atatetea, lakini ni malalamiko si ya Hija Hassan Hija wala Ame Mati Wadi.

Sasa kama wananchi wanalalamika maana yake utoe fursa ya kufanya uchunguzi, ili wewe ukae kama waziri na wizara yako na SMZ chini ya CCM basi iwe salama na isilaumiwe. Mhe. Spika, si kwamba kila mpinzani akilaumu ana nia mbaya, isipokuwa tunaumwa na uwezo wako ulioufanya katika miaka hii mitano, lakini wananchi wanayo malalamiko.

Kutokana na hali hiyo, namshauri Mhe. Waziri aunde tume kwa ajili ya kuchunguza mambo matatu ambayo ni muhimu sana. Kwa mfano, kuna wananchi wanaosema kwamba *interview* iliyofanywa mwaka jana kwa Pemba wanafunzi walioomba nafasi ile si zaidi ya 90 na wanafunzi wa Unguja si zaidi 203. Lakini kwa nini leo kuna wanafunzi zaidi ya 500, kwa sababu kwenye kitabu 440 mwaka wa kwanza, sasa hao 440 kama walioomba ni 300 kwa nini iwe 400, hayo ndio malalamiko ambayo Wazanzibari wanayolalamika.

Sasa suluhisho pekee ni kuunda tume kwa lengo la kuchunguza malalamiko. Je, walioingia ndio wale wenye sifa kama vigezo vilivyowekwa na bodi. Je, kweli wote walioingia wamefanya *interview* au kuna nini. Lakini Wazanzibari wanafika mbali zaidi na kushtumu ni maneno ya mitaani. Kwa hivyo, ikiwa ni maneno ya mitaani lazima yathibitishwe kwa uchunguzi, kwamba wapo watu wanaoingia kwa shilingi 500,000/-.

Mhe. Spika, mwakilishi akiambiwa hivi lazima Mhe. Waziri aambiwe, ili aweze kufanya uchunguzi, si kwamba kila kitu tutetee tu mpaka tufike pahala pakaharibika. Kwa hivyo, ninamshauri Mhe. Waziri alifanyie uchunguzi suala hili na kama kuchunguza inashindikana kwa upande wa Bodi basi unda Tume ya Baraza tukachunguze malalamiko hayo ya Wazanzibari.

Suala jengine kwenye Chuo hiki cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni kina tatizo la uvamizi wa majengo ya wananchi. Kwa kweli eneo la chuo ni zuri ambalo ni kubwa, lakini wananchi wamevamia, sasa kwa sababu wamevamia lazima tupate ufumbuzi wa wananchi wale kwa nini wakavamia na bila ya shaka waondoke kwenye eneo lile, ili chuo kiweze kubakia salama katika mipaka yake.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nichangie kwa haraka ni kuhusu Idara ya Hospitali ya Mnazimmoja. Kwa kweli niwapongeze kwa ufanisi wanaoufanya mkubwa kwenye upanuzi wa majengo, vifaa pia vinapatikana, vile vile niwapongeze hasa wakunga maana yake hivi juzi walinisaidia kupata mtoto wa Kiunguja. Kwa hivyo, lazima niwapongeze kwa jitihada zao hizo na ninamuomba Mhe. Waziri awasaidie zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumekuwa tukilalamika kwamba ile ni Hospitali ya Rufaa, kwa hivyo, Hospitali ya Rufaa lazima maabara yake iwe ya rufaa kweli. Kwa kweli mara nyingi tumekuwa tukilaumu kwa lengo la kuelekeza, lakini amekuwa akitetea sana kwamba ni nzuri na wala haina tatizo, yaani ni maabara ya kisasa, sisi ndio haja yetu na wala hatuna maana kama tunakosoa kwa kubeza yale mafanikio, haja yetu kweli iwe ya rufaa.

Lakini nikiangalia wafanyakazi kwenye maabara ile, wafanyakazi wapo tena wenye uwezo isipokuwa hawatoshi. Sasa ili iwe ya rufaa kweli basi wazidi kuongezwa na wafanyekazi vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu ubovu wa vifaa nadhani Mhe. Waziri atukubalie kwamba baadhi ya vifaa kwenye maabara ile havifanyikazi kwa njia moja au nyengine, yaani ni vimechakaa ama vibovu, pia vipo ambavyo vimeathiriwa na joto na kuharibika. Vile vile kuna suala ambalo linatia sifa mbaya kwenye maabara ile ni upungufu wa zile *reagnt* hazitoshi, upungufu huo hupelekea matokeo mabaya kwenye vipimo vya wagonjwa.

Leo nimekuja na vyeti viwili ili kuonesha kwamba wafanyakazi wapo ambao wenye uwezo, lakini hawatoshi na wanaathiriwa na ukosefu wa *reagnt* pale maabara.

Kwa mfano, hivi karibuni tumempeleka mgonjwa kwa ajili ya kupima tatizo la wingi wa damu, yeye mwenyewe alikuwa akisumbuliwa na kichwa, homa na alisema apelekwe Hospitali ya Mnazimmoja pengine ninao upungufu au ziada. Mhe. Spika, baada ya kwenda pale kupimwa na daktari, mimi naamini si kwa sababu ya utaalamu, isipokuwa ni upungufu wa matatizo ya *reagnt*, alisema wewe damu yangu ni nyingi sana, mimi wala si mtaalamu imeandikwa *HB* 15.8.

Kwa hivyo, alimshauri haraka akatoe damu chupa mbili, nikamwambia umesikia daktari alivyosema kwamba ukatoe damu kwa ajili ya kuchangia kwenye Benki ya Damu. Kutokana na hali hiyo, alinimbia mimi sina damu na wala siendi, nilimwambia usipingane na maamuzi ya daktari hii ndio homa yako, aliniambia siendi hata kwa bakora.

Kutokana na hali hiyo, nilimwambia sasa itakuwa kazi ya kuja hapa na kupima itakuwa ni ya bure, alisema siendi kwa sababu sina damu najijua mimi kama sina damu. Kwa hivyo, aliniambia twende hospitali nyengine tukapime wakati huu.

Mhe. Spika, kutokana na matokeo ya Hospitali ya Mnazimmoja ulinganisha na matokeo hospitali nyengine binafsi ambayo serikali wanaiamini na kuikubali ni tofauti yake ni 5. Hospitali ya Mnazimmoja aligunduliwa kuwa damu yake ni nyingi kwa HB 15.8 na kuambiwa akatoe damu chumba mbili, lakini kwenye hospitali binafsi aliambiwa damu ya ni kidogo HB 9.6 na kuambiwa haraka alazwe atiwe damu. Kwa kweli haya ndio mambo ambayo tunamwambia Mhe. Waziri na wala hatulaumu. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli mimi naamini kabisa yule daktari aliyepima anao uwezo tena ni mtaalamu, lakini ni matatizo ya vifaa. Sasa tukisema na hili akalikataa basi itakuwa hatuelewi. Mhe. Spika, mimi mwenyewe pia nilishawahi kwenda kupima malaria na niliambiwa ni *negative*, basi nilikwenda hospitali ya binafsi ambayo inaaminiwa nilimbiwa ni *positive*.

Kwa hivyo, nilimuuliza kwa nini kule niliambiwa *negative* na huku naambiwa *positive*, basi niliambiwa huu ni Mradi wa Marekani na wala hataki atiwe ila kwa hiyo tumeambiwa tusiwaambie hivi. Mhe. Spika, kama hili ni kweli vyeti vipo na hayo ndio malalamiko ya wananchi wa Zanzibari. Sasa tukisema najua atatetea sana, lakini nasema kwa nia safi kabisa kwamba madaktari wa Hospitali ya Mnazimmoja kuwa uwezo wao ni mzuri au mkubwa, isipokuwa vifaa pamoja na *reagnt* ndio matatizo.

Pamoja na hayo, kama hazipo mtu huyu tungemtoa damu juzi basi tungemzika, wakati anambiwa atoe damu chumba mbili kwa ajili ya Benki ya Damu na kule anaambiwa alazwe utiwe damu kwa ajili ya kuongezwa damu kama si hivyo atakufa. Hata hivyo, tumemfanyiakazi hiyo na hivi sasa hali yake nzuri.

Kwa hivyo, ndio malalamiko ambayo Mhe. Waziri lazima ayazingatie na wala asitetee kila jambo, isipokuwa mambo mengine atusikilize, kwa sababu sisi ndio wananchi tunaoishi Unguja na Pemba, hivyo tutatue matatizo ya Unguja na Pemba.

Sasa niende kwenye Kitengo cha Afya ya Mazingira. Mhe. Spika, kitengo hiki kimesema kimefanya ukaguzi wa uuzwaji wa vyakula, naomba niwapongeze kwa juhudi zao na waendelee. Hivi juzi niliwasikia wauza *chips* wakati walipokuwa wakihojiwa, walikiri kwamba baadhi ya wauza *chips* wamekuwa na tabia ya kuchanganya mafuta ya kawaida na yale ya *transformer*. Hata hivyo, walisema kwamba chupa moja ndogo ya mafuta yale wanaweza kuchomea gunia la mbatata na huo ndio mtaji wao.

Kwa hivyo, mimi ushauri wangu kitengo hiki kiendelee kuwachunguza wauza *chips* wa Unguja na Pemba vyenginevyo watatumaliza. Mhe. Spika, wamekiri kweli kuwa wao wanatumia mafuta ya *transformer* kwa ajili ya kupata faida kubwa kwenye biashara yao. Lakini sijui kiafya athari yake iko vipi na kama ina athari, basi ni vyema kudhibitiwa na kuweza kuchunguza hali hiyo, kwa sababu *chips* kwa Zanzibar ndicho chakula kikubwa ambacho watu wanakipenda.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu *Pesticide Management*. Kwa kweli sijui kwa kiasa gani kitengo hiki kinachunguza matunda yanayotoka Tanzania Bara na kuja Zanzibar. Hivi sasa Wazanzibari wanatumia kwa asilimia kubwa

matunda kutoka Tanzania Bara, hivi ni kwa kiasi gani matunda haya yanachunguzwa, ili kulinga afya za wananchi wetu.

Mhe. Spika, kunzia jana ndio tumeanza kuingia kwenye Soko Huria, bila shaka matunda ya Uganda na Rwanda yataingia hapa Zanzibar. Kwa hivyo, kitengo hiki lazima kiwezeshwe kwa utaalamu pamoja na fedha kwa lengo la kufanyakazi hiyo ya kuwatafutia usamala Wazanzibari.

Vile vile kuhusu ongezeko la nzi Zanzibar. Mhe. Spika, bila ya shaka ni kutokana na uchafu ambao nadhani unachangiwa na Baraza la Manispaa wenyewe. Mhe. Spika, hivi karibuni ulitupeleka Malaysia pamoja na wenzangu, sasa wakati tupo hoteli na Mhe. Omar aliniuliza mbona hawafuniki chakula, yaani wanakiacha chakula wazi baada ya kumaliza kupika mpaka wateja wanapokuja na tulikaa pale zaidi ya dakika 30 hatukumuona nzi.

Kutokana na hali hiyo, basi tuliwahoji kwa nini hapa hakuna nzi hapa Malaysia, walituambia kwamba nzi wapo, lakini hawathubutu kutoka kwa sababu wamedhibitiwa. Mhe. Spika, hivi leo nani mwenye kuweza kufunua sahani ya chakula, sasa baada ya kuweka mapambo kwenye nyumba basi makawa ndio yamekuwa mapambo, kwa kweli nzi ni wengi sana Unguja na Pemba. Kwa hivyo, kitengo hiki lazima kidhibiti ongezeko la nzi kwa ajili ya kuondosha maradhi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimuombe Mhe. Waziri anikubalie kuhusu kuunda Kamati ya Kuchunguza Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni, kwa lengo la kuondosha malalamiko ya wananchi, ili niinue mkono pamoja na ridhaa yangu na kuweza kuunga mkono bajeti yake kwa asilimia mia moja. Hili ndilo tatizo langu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi sina mchango mkubwa sana.

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake. Kwa kweli kumbe hapa tunao watu wengi wenye uwezo wa kugombea nafasi ya urais lakini mwenzetu amejitupa. *(Kicheko/Makofi)*

Nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 17 ambapo nimeona *contradiction* ndogo ambayo nataka kupata ufafanuzi kuhusu Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbeni ukisoma ibara ya 2.8.1 naomba kunukuu Mhe. Spika,

Ukurasa wa 17 kifungu cha 2.8.1 kinasema hivi:-

"Chuo hiki kinabaki kuwa ni taasisi pekee inayotambulika

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaotoka nje ninawahitaji sana kiasi baada ya dakika kumi hivi muwemo humu ndani, ili tusaidiane jambo la utaratibu. Kwa hivyo, wale wanaotoka nje baada ya dakika kumi warudi kwa ajili ya kuifanya hiyo kazi. Mhe. Mjumbe endelea.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, ahsante.

Ukurasa wa 17 kifungu cha 2.8.1 kinasema hivi:-

"…Chuo hiki kinabaki kuwa ni taasisi pekee inayotambulika hapa Zanzibar kutoa mafunzo ya afya katika ngazi ya cheti na diploma".

Kwa hivyo, katika sentensi hii inasema cheti na diploma. Lakini kwenye *paragraph* inayofuatia ya 2.8.2 naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 17 kifungu cha 2.8.2 kinasema hivi:-

"Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbeni kwa sasa kinatoa mafunzo ya stashahada pekee"…

Sasa *paragraph* ya mwanzo inasema cheti na diploma na *paragraph* ya pili inasema diploma pekee, ipi iko sahihi. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie katika hili.

Mhe. Spika, pia kwenye Idara ya Tiba tukiangalia maelezo ya idadi ya wagonjwa waliolazwa katika Hospitali za Chakechake, Mkoani na Wete, ukiangalia kwenye kiambatisho na baadaye ukaangalia kwenye maelezo ya hotuba hayalingani hata kidogo.

Kwa mfano, Hospitali ya Abdalla Mzee wagonjwa waliolazwa walikuwa 932 katika kiambatisho, lakini ukija kwenye maelezo ya hotuba wagonjwa waliolazwa walikuwa 3,450 na huo ni mfano mmoja. Kwa hivyo, tukiangalia hospitali nyengine za Wete, Chakechake takwimu kidogo zinababaisha. Hilo la pili.

Mhe. Spika, nisikitike tena kwa mara nyengine kuhusu hospitali yangu kwa bahati nzuri mimi ni mtu wa Mkoani, kwa hiyo lazima niizungumze Hospitali ya Abdalla Mzee kwa kadri ninavyoifahamu tokea ilipojengwa mpaka hivi leo.

Kwa kweli tokea wakati alipokuwa Mhe. Salim Juma Othman Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry Naibu Waziri wa Afya na

Ustawi wa Jamii, nilikuwa nikisifia uzuri wa hospitali hii hapo mwanzo wa majengo, usafi na huduma. Lakini hivi sasa kadri tunavyopiga kelele bado hali ya majengo yamechakaa mno, nashangaa kuambiwa kupata rangi, nadhani rangi ni hatua ya mwisho kwenye *finishing*.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema tukalifanyia matengenezo kwanza, lakini leo ikinyesha mvua kwenye lile jengo kubwa la utawala pamoja na idara nyengine linavuja tena ni bovu hasa, huku inasifiwa kwamba limepakwa rangi. Sasa kupaka rangi wakati jengo ni bovu kuna faida gani, nafikiri bora usipake rangi kabisa. Kiukweli hospitali ya Abdalla Mzee inahitaji mazingatio makubwa hasa lile jengo kubwa, tukikaa nje utasema hii hospitali ni nzuri lakini ukiingia ndani ukiangalia hali siyo, milango yote mibovu fanisha zimechakaa mno wakati mwengine utakuta madirisha yako wazi tena wakati wa baridi na upepo unaingia wagonjwa wanapata tabu ya baridi, ukweli hospitali imechakaa sana, nashukuru madaktari wenyewe walivyokuja wakaona hawawezi kuishi maisha ya kikwetu wamejisaidia wenyewe *Alhamdulilahi*, lakini sasa na hospitali yenyewe nayo inahitaji kuangaliwa.

Mara nyingi tulikuwa tunapiga kelele juu ya wodi ya watoto tunapewa ahadi lakini mara hii haijazungumzwa lolote kuhusu wodi hii, na vile vile huwa tunapiga kelele kuhusu madaktari wazalendo nadhani pale madaktari wazalendo hawapo kabisa. Nafikiri pana Dokta Mussa ndio *Clinical Officer* na wengine waliobakia *Medical Assistant* basi, sasa wale machine wanakuwa hawana kaunta pale. Sasa hili nalo ni jambo la kusikitisha na hata ukiangalia baadhi ya vitengo vyengine mwanzoni vilivyokuwa na leo ni tofauti.

Kwa mfano kitengo cha meno mwanzoni ile hospitali ilipofunguliwa mpaka miaka mingi alikuwepo daktari binga wa meno akafundisha vijana wa Kiswahili pale akiwemo ndugu yetu Juma Rashid ni mtu mtundu mtundu tu, lakini pamoja na kuwa na watu watundu kwa ulimwengu waleo wanatakiwa na watu waliokuwa *professional* nadhani ni uzuri zaidi na huwa tunapigia kelele sana wauguzi kidogo mpaka wenzetu wanalazimka kutumia wale *Red Cross* jambo ambalo sio zuri lakini nalo vile vile hatusikilizwi. Sasa sisi hatutaki kuwalaumu wale waliopo pale ukimlaumu mkuu wa hospitali hana kosa kwa sababu ana wafanyakazi wachache atatumia *Red Cross* lakini watu hawariziki hata kidogo kuhudumiwa na vijana wa *Red Cross* hili linaudhi hasa. Sasa hiyo ilikuwa ni hospitali ya kwetu Pemba ya Abdalla Mzee.

Mhe. Spika, halafu nimeangalia jaduweli kiambatisho namba sita nne hiki kinahusu juu ya taarifa ya hali ya uzazi katika wodi ya wazazi kwa hospitali za idara ya tiba, Julai, 2009 hadi Machi, 2010 ambayo inahusu hospitali ya Micheweni, Vitongoji, Chake Chake, Wete, Mkoani, Kivunge na Makunduchi. Sasa ukiangalia Mhe. Spika, hospitali ya Wete kwa bahati nzuri hajafa hata

mzazi mmoja kwa hivyo ni jambo zuri na la faraja, lakini Chake Chake wazazi saba wamekufa sasa hii kidogo inatisha ni jambo la kuchunguza pana tatizo gani pale haidhuru kufa ni kitu kilichoandikwa na Mwenyezi Mungu, lakini na sisi tunahaki vilevile kuona je, hakuna mamabo ya uzembe au mambo mengine. Mpaka tufanye utafiti ili tujua ama ni kudura ya Mungu lakini nadhani ni mambo ya kuyaangalia, kwa sababu Wete hajafa hata mmoja, Abdalla Mzee wamekufa wawili lakini Chake Chake saba. Sasa nadhani haya sio mambo ya kuyaachia hivi hivi tu ni mambo ya kuyafanyia kazi.

Halafu Mhe. Spika, nizungumze juu ya elimu ya afya. Mhe. Spika, elimu ya afya tumeambiwa kwamba inatolewa kwa kupitia kwenye TV lakini mimi nasisitiza bado vile vile itolewe kwa kupitia katika maskuli kama ilivyokuwa zamani, zamani ilikuwa tunapatiwa elimu maskulini na ilisaidia sana. Kwa sababu kuna sehemu nyengine hasa Pemba TV hazionekani kwa hivyo napendekeza kwamba utaratibu wa zamani haidhuru ulianzwa na wakoloni lakini si kila kilichofanywa na wakoloni kibaya, kile kibaya tukiache kizuri tukiendeleze. Mimi nadhani huu ni utaratibu mzuri au mnasema kwamba mnatoa elimu ya afya pale kwenye miripuko sasa unasubiri miripuko tayari ndio unakwenda kutoa elimu ya afya nadhani itakuwa sio sawa, lakini ukipita kwenye maskuli hili suala litaingia kwenye mioyo ya watu kwa sababu watoto ukiwambia tu wanawaelimisha na wazee wao na wao watakuwa na tabia ya kujua hili baya na hili zuri inasaidia.

Halafu nije katika kitengo cha Afya bandarini hili jambo linanisikitisha sana kwamba vyombo vingi havikaguliwi vizuri utakuta mameli yanasafiri vyoo vichafu, au utakuta meli ina uwezo wa kuchukua abiria mia sita au mia tano lakini ina vyoo viwili sasa sijui hili kosa ni la wapasishaji tuseme watu wa bandari, watu wa afya hawana *Role* lakini haiwezekani meli inachukua abiria mia sita ikawa na vyoo viwili. Halafu kuna meli nyengine ukiingia uchafu maji ukenda vyooni utarudi maji mpaka kwenye magoti, sasa kwa kweli hapa inaonekana kwamba hapa katika nchi yetu tunacheza na afya za watu, sasa haya mambo naomba yaangaliwe, hapa panahitaji ushirikiano mkubwa wa Wizara mbili kati ya afya na mawasiliano lakini kwa kweli meli zinatisha kwa hali ya uchafu.

Halafu nije katika bodi ya chakula dawa na vipodozi nimesoma hii habari kwamba kuna vipodozi vinapigwa marufuku ambavyo vinakuza maumbile ya watu, juzi nilikuwa nasikiliza redio moja nafikiri redio imani wanasema kuna mwanamke mmoja anatumia vipodozi vya kukuza makalio likakua moja na jengine halikukua. Sasa mimi suala langu ni hili inakuwaje bandarini tuna wafanyakazi wetu wa afya lakini dawa hizi zinaingia mpaka kwenye maduka ya madawa na vipodozi inakuwaje, uzembe wa nani lakini pia siku moja nilisikia tangazo la katazo kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwamba

kuna wauza supu ya pweza wengine wanatia dawa za kuongeza nguvu kwa wanaume kwa hivyo tunapewa tahadhari na watu hawa.

Sasa hapa mimi nashangaa baada ya kutoa tahadhari kwa wananchi je, hawa wanaofanya haya hatua gani wamechukuliwa kwa sababu bora kuchukua hatua watu wakapata adabu kuliko kuwatangazia watu wasinywe supu, supu hatuwezi kuzikosa kabisa *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine la mwisho mradi wa mabadiliko ya sekta ya afya hapa nimeona mambo nimefurahi sana ukurasa wa thamanini na moja, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri tena kwamba Mhe. Waziri na wenzake wana *vision* na wanakubali kuiga mambo mazuri labda ninukuu anasema.

"Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi wa mabadiliko wa sekta ya afya umejiwekea malengo yafuatayo:-
(A) kutengeneza muongozo wa kuanzisha bima ya afya kwa wafanyakazi". Mhe. Spika, kwa wenzetu bara wanayo zamani bima ya wafanyakazi Rais Obama kagombana na *Republican* miezi mitatu kwa suala hili lakini mswada wake ukapita, haidhuru kwa uchache wa kura saba lakini kwa kuhakikisha bima ya afya kwa wananchi wote sio wafanyakazi, sasa kuwa na bima ya afya angalau kwa wafanyakazi ni jambo zuri. Sasa Mhe. Waziri nakutakia kheri na hili na ishaalla nakuombeni muliharakishe ili wafanyakazi wetu waweze kuwa na bima ya wafanyakazi.

Halafu (B) mnasema kuanzisha mfumo wa ugawaji wa wafanyakazi wa afya hivyo niulize suala, sasa hapa ndio wataalam wengi wazalendo wamejazwa Mnazi Mmoja kwa sababu hamjakuwa na mfumo wa kugawa wafanyakazi, na mpaka huu mtakapotengeneza huu mfumo ndio mtaweza kugawa wafanyakazi wa afya katika nchi nzima kwa visiwa vyote viwili kwa haki.

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru na nakuomba ukifika wakati huo nigombee kwa sababu huenda nikasahau kuweka muda, mimi naomba nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mipango, wakubwa wengine pamoja na madaktari na wauguzi, Afsa Mdhamini Pemba na kundi lake kubwa alilokuwa nalo ukweli wanafanya kazi nzuri sana. Ukweli wanafanya kazi ya kizalendo katika hali ngumu bajeti waliyopewa inavunja moyo hata kufanyiwa kazi, lakini kwa sababu ya uzalendo wao wameamua kutusaidia sisi ambao tunaumwa mara kwa mara kwa hili nawapa pongezi kubwa sana.

Nawaomba wajue kwamba kazi wanayofanya ni ya wito na Mungu ndio atawalipa malipo wasitegemee mshahara tu lakini mwenyezi Mungu atawalipa zaidi, sasa baada ya dibaji hiyo naomba nikiri kwamba Mhe. Waziri na watu wake ni watu wenye huruma sana mimi binafsi nawaheshimu sana, kwa sababu tuna ukaribu tunashauriana na wananisaidia sana nikiwa na matatizo yangu kwa hili naomba wapokee pongezi zangu.

Lakini katika bajeti yake hii ya leo nakusudia kuzuia fungu la kurugenzi ya mipango pamoja na hisani kubwa tuliyokuwa nayo hadi hapo atakaponiondoa kwenye dhamira yangu basi ninaweza kumuachia, lakini bado nina tatizo kubwa mimi Mhe. Subati Khamis hapa ni jirani yangu namuheshimu sana lakini nikigundua kwamba ana mpango wa kunidhulumu basi hisani huondoka. Sasa na Mhe. Waziri katika bajeti yake hii katika idara ya tiba siifahamu vizuri na nahisi kwamba ana tatizo kidogo na tatizo hili sio la idara ya tiba ni kurugenzi yake ya mipango na sera kwa sababu wao ndio wasimamizi wa mambo.

Mhe. Waziri katika kitabu chake anasema kwamba Idara ya Tiba ina hospitali saba, Hospitali ya Kivunge na Hospitali ya Makunduchi kwa Unguja na Hospitali ya Wete, Abdalla Mzee, Chake Chake, Vitongoji na Micheweni kwa Pemba, Idara ya Tiba Unguja yenye hospitali mbili ameiwekea milioni mia mbili arubaini, Idara ya Tiba Pemba yenye hospitali tano ameiwekea milioni thamanini na tisa. Sasa hapa nahisi hanifanyii haki shughuli za hospitali Pemba zinaathiriwa na mgao mbaya wa kibajeti na nilipokwenda ndani kwa mgao katika wa mafungu ya Idara hii ya Tiba nimeona pana tatizo sana Mhe. Spika, Fungu 14000 Gharama za Mafuta na Nishati kwa hospitali mbili za Unguja zimewekea Shilingi ishirini na tisa milioni, kwa hospitali tano za Pemba zimewekewa ishirini milioni sasa hii haiwezekani.

Fungu 15000 Huduma za Vifaa vya Ofisini kwa Asifi mbili za Unguja zimewekewa ishirini na tatu milioni, kwa hospitali tano za Pemba amewekewa milioni nne.

Fungu 1700 Spea za Mashine na Matengenezo kwa Unguja hospitali mbili ameweka milioni nane kwa Pemba hospitali tano ameweka milioni moja.

Fungu 1800 Gharama za safari kwa hospitali mbili za Unguja wamewekewa milioni kumi na tano za Pemba wamewekewa milioni tano.

Fungu 2600 Matengenezo ya magari kwa unguja zimewekwa shilingi milioni kumi na Tano kwa Pemba zimewekwa shilingi mioni moja na nusu.

Fungu 2700 Ununuzi wa vifaa vya majumbani thamani na mapazia Unguja hospitali Mbili zimewekewa shilingi kumi na tano milioni, hospitali tano za Pemba hazikuwekewa kitu.

Nilipoangalia zaidi niliporudi nyuma nimeangalia kwamba kwa miaka minne basi za Unguja kwa mwaka wa kwanza ziliwekewa Shilingi milioni moja laki nane, za Pemba hazikuwekewa kitu. Mwaka uliofuatia Unguja zikawekewa laki tano Pemba hazikuwekewa kitu, mwaka jana Unguja zikawekewa shilingi milioni ishirini na moja za Pemb zikawekewa laki sita na mwaka huu zimewekwa milioni kumi na tano Unguja na pemba hazikuwekewa kitu.

Fungu 3000 Ununuzi wa madawa hospitali mbili za Unguja zimewekewa sabiini milioni za Pemba hazikuwekewa kitu labda hizi za madawa na Pemba zinakuja kidoto.

Katika kuendesha hospitali fungu la Unguja limewekewa milioni kumi na Pemba limewekewa milioni tatu na nusu, gharama za ufuaji nguo hospitali mbili za Unguja zimewekewa milioni mbili nukta saba za Pemba tano zimewekewa milioni moja.

Gharama za Chakula cha wagonjwa hospitali mbili za Unguja zimewekewa thalathini na sita milioni za Pemba tano zimewekewa thalathini na tisa milioni, ukigawa hospitali mbili za Unguja maana yake kila moja milioni kumi na nane, za Pemba kila moja milioni nane.

Vifaa vya Kulalia na kulia hospitali mbili za Unguja zina milioni saba na za Pemba hazina kitu, Matibabu ya Nje kuna milioni mia moja na kumi na nne kwa Unguja na Pemba kuna milioni moja nukta mbili.

Mhe. Spika, labda Mhe. Waziri swahibu wangu sana mwenzangu sana hadi hapo atakapokuja na majibu maridhawa sana tena ya uhakika basi vyenginevyo nakusudia kuzuia fungu la idara ya mipango kwa sababu mipango ndio wanaosaidia kupanga hii bajeti ambayo haiku sawa hata kidogo, wanaweza kumfanya jitihada nzuri ambazo Mhe. Waziri anafanya ikapata doa sana katika masuala haya. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri bahati nzuri Mhe. Spika, umenipa nafasi wakati mzuri ambao wasaidizi wake na watendaji wake watapata nafasi ya kumsaidia kujibu hoja yangu basi naomba umuwekee tada zake vizuri ili aje anifafanulie kwa upana sana vyenginvyo ninaweza kuwa mgumu na sipendi nifanye jambo hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo naomba nilizungumze ni suala la malipo ya wafanyakazi madaktari na watu wengine katika hospitali wanafanya kazi moja ngumu sana kama nilivyosema mwanzo lakini bado malipo yao ni ya

kusikitisha sana, wimbo wa *scheme of service* umekuwa ukiimbwa siku nyingi lakini sijui unakwama wapi na hili linatuathiri sana katika jambo ambalo Mhe. Waziri anajitahidi ni kusomesha, lakini vijana wanapokuja hapa wakiona kile wanacholipwa hawakai sasa tutalaumiana madaktari hawawezi kukaa hawezi kuja mtu hapa na *Master degree* yake mtaalam mzuri akapewa laki tatu wakati hapo Dar es Salaam au Kenya pengine anapewa milioni moja au mbili.

Sasa hili Mhe. Waziri anasema ametengeneza *scheme of service* hili ni jambo jengine lakini kusimamia na kufanya *lobbing* ili iweze kufanya kazi ni jambo jengine, sasa mimi ningeomba tuongeze jitihada katika hilo na naiomba serikali imsaidie katika hili, kwa hili tutapata tabu sana kuna vijana wengine hivi sasa wanakaa wanasubiri muda wa *scheme of service* utekelezwe wakiona hakuna kitu watatukimbia sasa hili ni tatizo kubwa hatuwezi kutegemea waquba tu.

Mhe. Spika, mwisho kabla hujanikumbusha Chuo cha Afya Mbweni wenzangu wamesema lakini mimi nataka kuzungumza mambo mawili la kwanza ni uvamizi wa ardhi haipendezi kuwa Chuo kimeshapewa waraka halafu wajanja walivamie eneo tena walijenge majumba makubwa, sasa ukiuliza vipi mambo hayo utasema wamejenga Jumamosi na jumapili haiwezekani, jumba lina kuta kuliko hili Baraza la Wawakilishi haliwezi kujengwa jumamosi jumapili likamaliza ni jumba la fahari ambalo limechukua eneo zima la ardhi. Tumeambiwa kwamba kuna msaada wa Oman unajibana bana kwa sababu ya ardhi ambayo iliwekewa kwa chuo imemalizwa.

Mwisho ni suala la mafunzo mimi ningeshauri kwamba wakati umeshafika sasa chuo kile kikatoa shahada inayohusiana na elimu ya tiba, tunashukuru kwamba waziri amejitahidi kupata darasa la madaktari wa Quba, sasa mimi ningeshauri kwamba lile liwe *transition* baina ya Diploma anayotoa na *Degree* ambayo ninaishauri kwamba wale madaktari wa Quba ambao wanafundisha elimu ya Degree ya kwanza ya mambo ya Tiba, basi liledarasa lisife na liendelee moja kwa moja kwa msaada wa Chuo ionekane kwamba sasa vijana wetu japo kumi kwa mwaka kutoa elimu hii ya shahada ya kwanza ya elimu ya afya.

Mhe. Spika, nakushukuru na hadi hapo Mhe. Waziri atakaponijibu suala langu kuhusiana na ubaya bajeti yake baina ya Unguja na Pemba kwa Idara ya Tiba basi naweka kusema naunga mkono hoja au laa, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nakushukuru Mhe. Said Ali Mbarouk na nakushukuru vile vile kwamba sasa ule muda umeniongezea kidogo niliokuwa nimekuomba uniachie, waheshimiwa wajumbe tunaelewa kwamba tunakabiliwa na uchaguzi mkuu na sisi hapa ni wadau wakubwa wa uchaguzi huo sio tu kwa kupiga kura lakini wengine kwa kupigiwa kura, kwa sababu hiyo ratiba yetu ya mkutano huu wa

bajeti itakuwa ina marekebisho ya mara kwa mara kwa sababu ya kukidhi hiyo hali tuliyonayo.

Huko nyuma atulipokuwa kwenye vikao vyetu tulifikia pahala tukakubaliana kwamba siku ya Jumaapili tufanye kila njia inayowezekana tusije, tukasema tuzingatie jambo hilo lakini kila tunapoangalia hali imetubana kweli kweli na bado tulipanga kwamba tumalize shughuli zetu tarehe 16/7/2010 bila ya kuzidi muda wowote, kwa sababu hapo mbele tena ndio kuna kazi kubwa zaidi ambayo wajumbe itakuwa ni vigumu sana kuwapata kuendelea na shughuli zetu hapa barazani.

Sasa kesho tarehe 3/7/2010 kuna kamati maalum ya Chama cha Mapinduzi, lakini Kamati maalum hii inachukua sehemu kubwa ya wajumbe wa upande wa Mkono wangu wa Kulia, mbali ya hivyo kuna wengi wana hamu ya kujua kitakachotokezea pale afisi kuu ya CCM tukisema kesho tuendelee na shughuli zetu kama vile tulivyopanga kwa kweli shughuli zetu zinaweza kushindwa kwenda. Kwa hivyo tukaona kwamba kesho tuiwache kabisa na badala yake kwa masikitiko makuba zile siku za jumapili tulizosema hizo tupumzike ile kazi iliyokuwa inafanyika Jumamosi tukubali hapo baadae utaratibu utapokuja kwa mujibu wa taratibu zetu, jumapili ya tarehe 4/7/2010 tuitumie kwa kazi.

Halafu siku ya tarehe 7 ambayo ni siku ya saba saba yaani ni *holyday* siku inayofuata na kabla ya hapo mchakato mwengine katika Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa CCM vile vile ambayo inachukua karibu wajumbe wote hatimae na mkutano mkuu wa upande huu nao tutakuwa na kazi kubwa sana, sasa tukaona tarehe 8/7/2010 ndio siku ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM ambapo anategemewa kupatikana mjumbe mmoja wa CCM ambae atasimama kugombea uchaguzi wa Rais wa Zanzibar tunashukuru upande wa kushoto mchakato huo umekwisha salama.

Mlinisaidia sana kupanga ratiba zetu zisiingiliane na shughuli zetu za Baraza kwa kweli nawashukuru sana sisi tulichelewa kidogo huku upande wa pili, lakini hii inahitaji mchango wa pande zote mbili kwa sababu hili jambo ni la kidemokrasia katika nchi yetu na ni jambo letu la ndani ya nchi, sasa naomba tuje tukubaliane baada ya hoja itakapotolewa rasmi na waziri anayehusika kwamba siku ya kesho 3/7/2010 tusije katika vikao vyetu hapa. Badala yake tuje siku ya Jumapili tarehe 4/7/2010 tufanye kazi kama kawaida.

Lakini pili siku ya tarehe 8/7/2010 wajumbe wote watakuwa hawapo wa mkono wa kushoto na wengine wanaopenda pengine kwa mkono huu wanaweza kuenda kusikiliza kinachoendelea kwa sababu hatimae atakayekuwa rais anakuwa ni kiongozi wa nchi hii, atoke huku au huku. Kwa hivyo pande zote mbili zina hamu ya kujua nani huyu Mhe. Hamza Hassan Juma au Mhe.

Hamad Masoud, kwa hivyo kazi yetu tuifanye ile siku ya saba saba ambayo ni *holiday* utaratibu wa *holiday* tunajuana tunafanye na tuiwache tarehe nane iwe wazi ili wale wenye hamu ya kwenda pale Dodoma kusikia, kushuhudia na wengine kufanya kazi waweze kufanya kazi bila ya wasi wasi ya ratiba ya baraza inakwendaje.

Sasa tuliona tufanye hivyo ili kufanya shughuli zetu ziende bila ya kuja kuongeza muda huko usoni ambako huko mbele ni kugumu zaidi, kwa sababu wajumbe wenyewe kila mmoja wakati huo atakuwa yuko kwenye heka heka, ningeona ile bashasha yenu iko je ili baadae nimwambie Mhe.Waziri atoe hoja hapa juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

Nashukuru kwamba makofi ya pande zote mbili yamekuja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Naomba kutoa hoja kwamba baraza lako tukufu siku ya Jumamosi yaani kesho tusije kama ulivyotoa utaratibu na badala yake tuje siku ya jumaapili, lakini vile vile niombe tena kutoa hoja kwamba siku ya tarehe saba yaani siku ya mapumziko tuendelee na shughuli zetu za baraza na siku ya tarehe nane iwe mapumziko.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika. Nashukuru imeungwa mkono pale, sasa niwahoji wanaowafiki wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika, waheshimiwa wajumbe nakushukuruni sana kwa kutusaidia kuweka utaratibu wa shughuli zetu ili twende na mambo mengine ya kidemokrasia yaende sawa sawa.

(Saa 6.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza linaendelea)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Moh'd Ali Salum: Ahsante Mhe. Spika, kwa jioni hii kunipa nafasi kuwa mtu wa mwanzo katika kuichangia Bajeti hii ya Elimu. Bajeti yenye uhai wa watu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Allah kama kawaida yangu kwa sababu yeye ndiye pekee anayestahiki kushukuriwa kwa yote aliyotupangia na anayotupa tukaweza kufaidika hapa duniani na *Inshallah* akatufaidishe huko akhera tutakapokwenda kwa uwezo wake. Amina.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba katika Wizara hii nianze kwa kutoa shukurani nyingi sana. Kwanza nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi kubwa aliyoifanya, ukiachilia mbali kuwa sasa hivi tumekuwa ndugu wa toka nitoke lakini pia akamchagua Mhe. Mugheri kuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mtu ambaye kwa kweli ana uwezo mkubwa katika Wizara hii. Mimi huwa nafurahi sana pale anapokuwa anatoa majibu. Anatoa majibu kwa kujiamini kabisa na anatoa majibu ya kitaalamu ambayo anaonekana wazi kuwa hii Wizara anaimudu vizuri sana. Ama kwa hili naomba nimshukuru sana.

Mhe. Spika: Na sauti yake anasikia kila mtu. (*Vicheko*)

Mhe. Moh'd Ali Salim: Hakika.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba sasa niingie katika mchango wangu mdogo nilionao katika Wizara hii ya Afya kwa kuanzia Mhe. Spika, nataka nianze na kitengo cha hesabu. Moja katika kazi ya kitengo cha hesabu tulivyoambiwa katika kitabu hiki ni kufuatilia upatikanaji wa pesa ambazo zimeidhinishwa na Baraza hili kupewa Wizara ya Afya katika sehemu mbali mbali.

Mhe. Spika, nina masikitiko kidogo, masikitiko yangu katika mwaka uliopita mpaka mwezi wa mwisho tuliokwenda kwenye Kamati Pemba nilikuta Idara ya Ustawi wa Jamii imepatiwa fedha asilimia 20 tu. Wakati Idara nyengine zina 60 na zaidi au 50 na zaidi. Idara ya Ustawi wa Ujamii inawashuhulikia wafanyakazi walioumia wakiwa kazini. Hivi kweli jamani wafanyakazi wameumia wakiwa kazini wanastahiki kufidiwa angalau waweze kuendesha maisha yao au angalau waweze kupata matibabu yao au angalau waweze kusaidia familia zao walizonazo. Lakini wanapewa pesa asilimia 20 ukiachilia mbali kuwa mgao wao ni mdogo tangu hapo. Hivi kweli wamekusudiwa wafanyakazi hawa walipwe, hili naona ni moja katika upungufu tena upungufu mkubwa ambao serikali ilibidi wauangalie vizuri ili watu wawe na moyo zaidi wale waliokuwa hawajaumia kwa kuwaona kuwa wenzao walioumia angalau wamefaidika mapema kabisa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa niingie kwetu kidogo nisije kugeuka vya muazima jamvi, nikaanza kupiga mazungumzo akaja mwenzangu akaazima jamvi akatoka akenda zake na mimi nikabaki aah! Na mimi nilikuwa nikilitaka hilo.

Mhe. Spika, nakuja katika hospitali ya Abdalla Mzee kwa mujibu wa kitabu hiki cha Mhe. Waziri kuna masuala mazima ya kutengenezwa magari ya wagonjwa. Humu tumeambiwa habari hiyo. Hapa ninalotaka nilizungumze magari ya wagonjwa kutengenezwa ni jambo moja tena ni jambo dogo, ukilinganisha na jambo la pili ambalo hilo halipo. Magari ya wagonjwa hata yakiwa mazima hayawezi kwenda kuchukuwa wagonjwa.

Tatizo kubwa linalojitokeza ni mafuta, ikiwa magari haya hayana mafuta hata siku moja hayawezi kwenda Wambaa, Chambani, Chokocho, kuchukua wagonjwa, kwa sababu mafuta yanakuwa hapana. Inapofika pahala anatakiwa mgonjwa akachukuliwe pengine mjamzito anataka kujifungua uchungu tayari anao lakini mtoto hatoki anataka akachukuliwe ukipiga simu ipeleke gari ya wagonjwa ikawachukuwe unaambiwa utoe mafuta. Si kila mtu mwenye uwezo wa mafuta, hasa wa vijijini, miye nnao uwezo wa mafuta. Mhe. Spika, hili nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hizi gari akizitengeneza lakini pia azipatie na mafuta.
Mhe. Spika, kwa muda mrefu katika Baraza hili tumekuwa tumekizungumzia wodi ya watoto katika Hospital ya Abdalla Mzee, hakuna wodi ya watoto kuna kijichumba cha watoto ambacho hawaenei inafika pahalil inabidi walazwe chini kwenye magodoro. Hili si jambo la kuliangalia hivi hivi tu, ilikuwa kuna haja ya nguvu za makusudi pale Hospitali ya Abdalla Mzee.

Ukiacha hiyo wodi ya watoto pia kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi, kuna upungufu wa ma-*oderly*, wauguzi, madaktari pamoja na kuwa kuna madaktari wageni wa Kichina lakini bado kuna upungufu wa madaktari, hatuna daktri wa meno, daktari wa watoto, hatuna daktari wa macho. Upungufu huu unasababisha watu kupewa kazi ambazo. kuwa sio zao *Read Cross* sio kazi yake kufuatana na daktari katika *rounder* asubuhi. Ndio inafika pahali anakwenda mgonjwa kafanyiwa *operation* mgonjwa anashtakia anasema jamani nakohowa. Read Cross anamwambia kula *cofter*.

Mhe. Spika, hivi kweli dawa ya mgonjwa aliyefanyiwa *operation* na ikawa ana kikohozi ni *cofter*. Sasa katika hali hii kwa kweli tutauwa bila ya kukusudia au pengine kwa kukusudia, maana yake tunatarajia kuwa wale watafanya vizuri lakini kumbe hana utaalamu wa kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, ubovu wa Abdalla Mzee Hospitali inavuja, ndio jambo la mwisho. Kwa sababu nyumba inaweza ikawa mbovu mambo mengi lakini la mwisho

kuliko yote ni kuvuja. Sasa kunahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa ili mambo yaweze kwenda vizuri angalau irudie katika hali yake iliyokuwa zamani.

Mhe. Spika, nije katika suala zima la maabara. Pemba tuna maabara moja nzuri sana. Maabara ile inafanya kazi nzuri sana, lakini nilikuwa napenda kujua hivi maabara ile hivi sasa inachukua nafasi kutoka hospitali mbali mbali za kufanyiwa uchunguzi. Kwa mfano inafanya *culture an sensitivity* kutoka *spaceman* za hospitali mbali mbali. Kama hilo halifanyiki kuna haja ya kuandaa mpango maalum maabara ile licha ya kufanya yale yaliyopangwa hivi sasa. Lakini pia ikachukua *spaceman* za hospilitali mbali mbali kuangalia maradhi. Kwa sababu lazima tufike pahali tuseme sasa basi tena kutibu kwa kufikiria.

Mhe. Spika, mtu akwenda kwa daktari anamuuliza unaumwa na nini. Hapa pananichoma hapa pananiuma hivi. Daktari anafikiria pengine itakuwa kitu fulani unamwandikia dawa. Lazima tufike pahala tuachane na haya, aambiwe nenda pahali fulani ukachunguzwe, ukimaliza kuchunguzwa inaonekana ni kitu gani ulichonacho kinachokuletea matatizo unapewa dawa na unatibiwa kwa uhakika. Hili nalo nilikuwa naomba lingefanyiwa kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, nikija kwenye Idara ya Mipango na Sera. Katika suala zima la kuwafundisha wafanyakazi. Ukweli tunawafanyakazi wauguzi wa muda mrefu waliyopo hospitali tena hospitali nyingi. Wauguzi hawa wamekaa pale pale ni wauguzi tu, hawaondoki kwenye uunguzi wakapata nafasi nyengine. Yaani hawasomeshwi na baadaye angalau wakakuzwa wakawa badala ya kuwa wauguzi wakapata nafasi nyengine kubwa zaidi, pangine hata wakafikia madaktari wasaidizi au wakafikia madaktari wenyewe kabisa.

Hivi suala hili huwa haliwezekani au hawa waliyopo wauguzi hawana sifa ya kufanyiwa hivyo. Kwa nini wauguzi kila siku tuwaone wanabakia wauguzi tu pale kama ni mpiga sindano kila siku tumkute anapiga sindano tu pale. Hili nalo kuna haja kubwa ya kulishuhulikia ili wale wauguzi na wao wakapata moyo.

Katika uwalimu nashukuru mimi mwenyewe nilianza kama mwalimu wa cheti, lakini nikaendelezwa nikafika kuwa mwalimu wa diploma, nikaendelezwa zaidi nikawa mwalimu wa Chuo Kikuu mwalimu wa *degree* tumetoka pamoja na Mhe. Mugheri. Sasa hivi ndio inavyotakiwa, unapata moyo wa kufanya kazi. Lakini tena leo tena wewe muuguzi ndio muuguzi tu moja kwa moja mpaka unastaafu muuguzi. Hili nafikiri Mhe. Spika, kuna haja ya kulifanyia kazi nzuri sana.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie kidogo mafao ya wafanyakazi. Ni ukweli usiofichika, ukweli kila mtu anauzungumza kuwa bado mafao ya wataalamu wetu ni madogo. Tumekuwa tukisikia huu mpango wa *scheme of service* serikalini muda mrefu sasa. Tumeambiwa kuwa Wizara ya Elimu imeanza lakini nadhani kuanza Wizara ya Elimu haijafanya na Wizara ya Afya nayo waridhike, kuna haja na Wizara ya Afya nayo wafanyiwe ili na wao waridhike, tuweze kufika pahala tusitie maji katika pakacha bovu. Tuna wanafunzi tele tunaowafundisha lakini wakitoka hao kila mmoja anatafuta njia, tunawatia kwenye akacha bovu wanavuja.

Mhe. Spika, ni lazima tuizibe pakacha tukisha kuiziba tukiwatia kwenye pakacha watabakia ndani ya pakacha. Katika suala hili la Chuo bado napendekeza kuwa kuna maeneo ya mbali, maeneo magumu, yenye matatizo wakitokea watu waliosoma na wana sifa wa maeneo yale jamani wakifanya *Interview* wachukueni chuoni kwa sababu wengine wako tayari kurudi wakafanya kazi pale pale. Mimi nnao, nawajua, wako tayari, Wambaa, sifa wanazo na wako tayari kurudi kwao kuja kufanya kazi na mimi dhamana.

Mhe. Spika, Ahsante nakushukuru.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa umahiri wake wa kusoma hotuba hii. Kitabu kilikuwa kikubwa sana lakini ameweza. kufanya *summary* nzuri ya kufahamika na kwa kweli ni kitabu kilichojaa *materials* sio kitupu, kizito kinadata nyingi sana na kina taarifa za kutosha. Tumpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Mkuu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Baada hayo ningependa kuchangia kwa kuanza na kuwapongeza kuwa Afisi yao wameijenga vizuri sio kama Maafisi ya Wizara nyengine katika Mjimkongwe yananing'inia. Afisi yao wameijenga wameitengeneza vizuri na wanaiangalia ipo safi kabisa, hili nalo pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri.

Vile vile nampongeza Mhe. Waziri kwamba Wizara ina *Website* yake WWWZanhelth.imfor. Kwa hivyo hii mimi nilitaka kila wizara iwe na *Websit*e kama hii. Kwa hivyo hili vile nampongeza Mhe. Waziri kwamba *imformation* nyingi tutazipata katika *websit zao*. Ahsante sana.

Mimi nitaanza na Chuo cha Mbweni, mimi nakikumbuka kwa sababu ujenzi wa awali mimi nilikuwa ndio mkandarasi pale. Mipaka yote naielewa mimi na

beacons zote nilikuwa nazijua. Hii ilikuwa ni sehemu kubwa sana ilianza juu mpaka pwani kule. Sasa hivi imemegwa megwa imebakia kidogo sana.

Katika kipindi kilichopita Wawakilishi walipiga kelele sana kuhusu lile eneo lililobakia linatiwa uzio. Mhe. Naibu Waziri hapa alituahidi kwamba uzio utatiwa katika majengo haya. Kwa bahati mbaya nimeangalia ukurasa wa 19 kwa mwaka 2010 chuo kimelenga yafuatayo (a), (b), (c) ile (d) ya (d) ya kujenga uzio katika Chuo hiki sikuiyona. Kwa hivyo ile ahadi tuliyoahidiwa na Mhe. Naibu Waziri hapa haikuonekana. Nikitaka kujua kuna sababu gani iliyopelekea kwamba Chuo kile sasa hivi hakitiwi uzio na sasa hivi kimo katika hali ya hatari. Wanawake wengi ndio wanaosoma katika chuo kile. Mtu yeyote anaweza akaingia katika mabweni yao na akasababisha tatizo lolote.

Vile vile sasa hivi Chuo kina majengo mengi na mengine yanaongezwa kwa hivyo ni Chuo kitakuwa na hadhi ya kuwa ni chuo hasa. Kwa hivyo kuwa na geti huku kukawa kupo wazi nafikiri si jambo la busara. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atueleze kuna matatizo gani mwaka huu wasitie katika bajeti yao.

Vile vile kutokana na majengo haya yanavyokwenda na yanavyojengwa ningewashauri Wizara ya Afya wakageuza chuo hiki kuwa ni Chuo Kikuu. Majengo ni mengi yenye hadhi kubwa na kwa kweli ipo haja ya kutoa Chuo Kikuu cha tiba. Kwa hivyo hili ningemuomba Mhe. Waziri walitafakari na ikiwezekana walifanyie utaratibu.

Mhe. Spika, nikichangia ile mada iliyozungumzwa asubuhi Mhe. Said Ali Mbarouk, alizungumzia mgawanyo wa fedha kwa Hospitali mbili za Kivunge Mkunduchi na Pemba Hospitali tano, Chakechake, Abdalla Mzee, Wete, Micheweni na Vitongoji. Mimi nikitaka kuonesha *concern* yangu kwa kweli *it very un fair* . Ukiangalia katika mwaka wa 2009/2010 Kivunge na Makunduchi imehudumia wagonjwa wa nje 22,594 na imelaza wagonjwa 3195 waliofariki 23.

Chakechake peke yake Abdalla Mzee, Wete, Vitongoji hao wamehudumia wagonjwa 162,216 wa nje na wamelaza wagonjwa 13,085 na waliokufa 284. Ukiangalia hizi takwimu utakuta kwamba hospitali zile kule zinahudumia zaidi wagonjwa kuliko za huku, lakini bado zimepewa kasma ndogo sana ya fedha. Hata ukichukua hospitali kama ya Makunduchi mwaka uliopita imehudumia wagonjwa 5746 tu ambao Pemba hakuna hata kituo kimoja kilichohudumia chini ya watu 14,900 na kitu. Kwa hivyo nasema uwiano kama huu ni lazima uangaliwe na ningeiomba Wizara ikaliangalia suala hili ili iweze kuwezesha hospitali za Pemba kuweza kufanya kazi zake vizuri zaidi kwa sababu watu ni wengi, masafa ni makubwa. Inatakiwa. ipatikane *fairness* katika mgawanyo wa fedha katika hospitali zetu.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba kumshauri Mhe. Waziri kwa sasa hivi ICU yetu ni ndogo na ilijengwa sio kwa sababu ya ICU ilikuwa ni wodi ikawa *converted* ikawa ICU sisi tumeona ile itakuwa *40 per measure.*Wakati umefika sasa hivi wa kuona kwamba tunajenga ICU yetu ambayo itakuwa na *standard* ya ICU na tumeshaona umuhimu wake ni mkubwa kabisa. Ningemuomba Mhe. Waziri aliingize katika *vision* zake za muda unaokuja.

Vile vile a*uthopaedic unit is very important* sasa hivi wagonjwa wengi sana wanakaa katika koridoo, chumba kidogo sana cha kuwahudumia wale wagonjwa. Kwa hivyo ipo haja ya kuanzisha *unit* kama vile Moi Dar-es-Salaam Muhimbili. Pia ipo haja ya kujenga maabara kubwa zaidi ili iweze kutoa huduma vizuri zaidi. Clinic vile vile ipo haja yakufanya *extension* kwa sababu msongamano ni mkubwa sana.

Mimi naeleza haya kwa sababu hatuwezi kuzungumza suala la biashara katika nchi hii wala hatuwezi kuzungumza habari ya utalii katika nchi hii, wala hatuwezi kuwaita wawekezaji kuja katika nchi hii ikiwa huduma zetu za afya zipo katika hali ya chini kabisa. Mtalii akija Zanzibar anataka kuona kwamba akipata maradhi anapata tiba safi tena ya haraka. Muwekezaji vile vile akitaka kuja hapa na familia yake kuja kukaa na kuwekeza anataka kuona anapata huduma ya matibabu safi tena ya haraka. Vile vile na wanaokuja kwa biashara nao vile vile wanataka kujua je, kumepatikana *services* ya hospital.

Wenzetu sasa hivi Tailand na India ni moja katika njia za Uchumi kuna utalii *medical tourism* utakuta India imeingiza watalii mwaka jana laki tano na ushei kwa matibabu tu na Tailand imeingiza watalii zaidi ya laki saba kwa matibabu tu. Kwa hivyo hili ni suala muhimu sana kuona kwamba viwango vyetu vya tiba tunazidi kuvipandisha juu ili wawekezaji na watalii wapate imani yakuja kutembea katika nchi yetu.

Vile vile Wizara hii ina umuhimu mkuwa sana ikiwa leo hapa patatokea maradhi ya mripuko kama *cholera* na maradhi mengine ya kuharisha haya au malaria ikapanda juu sana hii inapunguza utalii, watalii wakisikia tu kama Zanzibar kuna cholera wana-*cancel booking* zote. Kwa hivyo hii ni wizara muhimu sana na ni wizara ambayo kwamba inatakiwa iangaliwe kwa makini sana ikiwa kweli kwa dhamira ya kuweza kushajihisha biashara, uwekezaji na utalii basi ni lazima wizara hii ipewe umuhimu unaostahiki.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya mimi nimevunjika moyo sana kuona kwamba bajeti ya wizara hii ndogo sana ukiangalia na bajeti za wenzetu katika Wizara ya Afya, ukitoka Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ni wizara ambazo zinashuhulikiwa sana. Serikali iliyokuwa makini kabisa inaangalia bajeti zake katika Wizara mbili hizi kwa ajili ya huduma ya jamii.

La kusikitisha kwamba Serikali yetu haijaangalia umakini ikaleta fedha za kutosha katika hii Wizara ya Afya ili waweze kuzimudu hizi huduma zote umuhimu wa Wizara hii ni mkubwa sana kwa vile tunataka kujenga nchi, tunataka kujenga uchumi wa nchi, kwa hivyo lazima tuhakikishie wageni kwamba hapa tiba ipo na vile vile wananchi wa nchi hii wawe na afya njema waweze kuajirika na waweze kuwa na afya ya kuweza kufanya kazi na kuzalisha mali.

Mhe. Spika, tukiendelea naomba kuwapongeza Wizara ya Afya kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushuhulikia masuala ya malaria. Malaria kusema kweli imepungua sio kama haipo lakini imepungua kwa kiwango kikubwa sana. Mimi Mhe. Spika, nilikuwa napata malaria kila mwezi naugua malaria lakini sasa hivi *alhamdulillah* naweza kukaa miezi minane, tisa mpaka mwaka sijapata malaria.

Kwa hivyo nasema kama kwa kweli imepungua kwa kiwango kikubwa sana na naamini tukishirikiana baina ya wananchi na Wizara ya Afya basi maleria tutaitokomeza kabisa kabisa nchini mwetu. Hili ni jambo la kushukuru sana kwa sa babu maleria vile vile ilikuwa ni kitu katika moja linalowatia hofu wageni kuja kwetu kwa sababu wakija hapa wanakuja kuchukua vimalea vya malaria na wanapeleka katika nchi yao.

Kitengo cha Afya Bandarini, kitengo hiki kinafanya kazi Bandarini kwa kuangalia meli na lakini kusema ukweli bado kazi haijawa nzuri. Kwa sababu bado katika meli hizo ukitoka na begi lako unatoka na mende unakwenda kuwatia nyumbani kwako, vipanya vidogo vinaingia. Kwa hivyo bado naona wafanye bidii ili kitengo hiki kifanye kazi zake vizuri kabisa. Vile vile tunawashukuru sana wizara hii inaangalia kwa uzuri kabisa kwa kuchunguza afya za wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 69 ni suala la maabara kule Pemba iko maabara ambayo kwamba fedha inakuja kwa msaada. Serikali ina *commitment* ya kutoa fedha angalau kidogo tu nafikiri kama milioni 30. Kwa bahati mbaya serikali inashindwa kutoa pesa maabara ile, suala hili linawavunja moyo sana wenzetu katika maabara. Wizara ya Afya utakapowaambia wanakwambia lakini wale wana fedha za kutosha za kufanya kazi zao, bajeti yao iko *full* kwa hivyo haina haja ya kuongeza pesa. Si masuala ya bajeti ni masuala ya *commitment* je, serikali imeji–*commit* kuchangia kiasi kadhaa katika mradi ule hata kama bajeti inafurika lazima serikali iwe *commited* kulipa ile *amount,* kutokulipa inaonekana kwamba serikali yetu haipo *serious*. Kwa hivyo ningeomba kwamba serikali lazima ifate ahadi zake, *commitment* walipe zile ada zao za kila mwaka katika maabara hii ili serikali ioneshe *commitment* zake ili wale wengine ambao watakuwa na hamu ya kuja kumsaidia katika mambo kama

yale wasije wakasikia kwamba kuna matatizo kuwa Serikali ya Zanzibar haina *commitment*. Kwa hivyo, ningeiomba wizara hii ishughulikie masuala hayo.

Mhe. Spika, kwa sababu muda wangu umemalizika ningeomba nimalizie hapo ingawa kuna mengi wenzangu watakuja kuyachangia. Ahsante sana Mhe. Spika kwa niaba ya Jimbo la Ikulu naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, mimi nitaanza moja kwa moja kwenye sehemu ya malaria.

Mhe. Spika, malaria ipo ijapokuwa tunaambiwa haipo lakini tunasema ipo japo kwa kidogo, lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake kubwa, Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa jitihada zao za kuweza kuipunguza malaria. Tunajaribu kutaka kufanya *eradication* ya malaria kwa jitihada zao nzuri wamejaribu kuweza ku-*eradicate* kwa kiasi fulani. Lakini katika suala hili la malaria mimi niseme kwamba athari kubwa nichukue watu wawili ambao mimi naona athari kubwa kwao inawapata.

Kwanza tuje katika sehemu ya wazazi ambao ndio inaowaathiri sana wanapopata homa hizi inakuwa ni athari kubwa sana. Kwa hivyo, mbali ya hawa wajawazito ambao wanapata athari kubwa ya malaria vile vile na watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano pia maradhi ya malaria yanawaathiri kweli kweli. Ndio nikasema kwamba japokuwa malaria imepungua mpaka kufikia asilimia 1, lakini hata hivyo tunasema kwamba malaria ipo.

Mhe. Spika, kwa ushahidi mwengine zaidi ambao unaojitokeza kuna tofauti ya majibu baina ya vituo vya hospitali mbali mbali. Mhe. Spika, wagonjwa wengi wa malaria wanapokwenda hospitali mara nyingi huwa wanaambiwa hawana homa lakini huwa wanajihisi wana homa na wanapokwenda hospitali nyengine wakiangaliwa inakutikana homa ya malaria ipo. Kwa hivyo, labda tuseme ni kwa sababu baadhi ya hivi vyombo wanavyotumia huwa zimeingiwa na *virus*, inawezekana labda baadhi ya darubini nyengine zina *virus* na ndio maana labda hawazioni. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba hili suala la madarubini zichunguzwe zisije zikatoa jibu ambalo sio sahihi.

Mhe. Spika, vile vile suala la ulaji wa dawa ovyo pia linaweza kumuathiri mtu, mtu anaweza kuwa malaria hana lakini akala dawa za malaria ile itakuwa ni athari katika mwili wake. Mimi nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba hizi tofauti zilizoko yeye bado hajazielewa na hizi kila siku zinazungumzwa kwamba kuna tofauti baina ya hospitali na hospitali katika majibu ya maradhi haya. Kwa hivyo, tunaomba baadae atueleze hii ilikuwaje

hata ikapatikana tofauti wengine wanasema wanayo wengine wanasema hawana, na sisi tunasema "*Prevetion is better than cure".*

Mhe. Spika, nasema mbu wapo ndani ya majumba, mbu wapo nje ya majumba na hawa mbu kwa mujibu wa dawa zinavyokwenda dawa inatiwa ndani ya majumba, dawa haitiwi nje ya majumba na huku nje ya majumba kwenye vijiji mbali mbali, kwenye miji mbali mbali kuna mambo mengi ambayo yanaonekana nje ambayo ni vizalio. Mhe. Spika, kuna madimbwi ya maji, kuna mahodhi ya maji, kuna vifuu, kuna magae, kuna mashimo ya maji, kuna madebe kuna mambo chungunzima ambayo yanaweza kusababisha wadudu hawa wakazaliwa.

Kwa hivyo, kama sisi tunatibu ndani ya nyumba kwa taarifa zao ni kwamba mbu akiingia ndani ya nyumba kwa kipindi kile mbu yule atakuwa hana athari. Mimi nasema pamoja na hayo yote wale wanaoingia wanatoka nje wako tayari na wakiingia ndani wanasema wanakufa, wanakufa wengine na wengine wanatuathiri. Kwa hivyo, mimi ningemshauri Mhe. Waziri kama kutakuwa na kitengo maalum katika sekta zake zote za afya suala hili kupatikane kamati au zamani ninavyojua mimi kwenye kila kituo cha hospitali kunakuwa na *healthing inspectors*, hawa hawapatikani na ndio maana maradhi haya bado yanaendelea kwa sababu wao ndio watakaopita kuhamasisha watu kwenye usafi wa mazingira. Kwa hivyo, uzalishaji unakuwa nje.

Mhe. Spika, vile vile niseme kwamba pamoja na hayo yote tulikuwa tunahitaji nyumba hizi kufukizwa nje na mwenendo huu sasa haupo tena wa kufukizwa majumba nje, ufukizaji wa siku za nyuma ulikuwa unaweza kusaidia kupunguza idadi ya watu. Malaria inaweza kupatikana pamoja na hifadhi kubwa ya kwamba tunatumia vyandarua lakini bado watu wanapata malaria mle wanamokaa katika mazungumzo, nje kwa hiyo ikiwa dawa haikufikizwa nje athari ya malaria huko ndiko iliko sio ndani ya nyumba, ndani ya nyumba unatumia chandarua lakini nje ukitoka malaria utaipata.

Kwa hivyo, namwambia Mhe. Waziri achukue juhudi hizo za kuhakikisha mambo haya yanatendeka. Mhe. Spika, pamoja na matumizi mazuri ya vyandarua tunashukuru kwamba wizara hii imejitahidi kuwahamasisha watu kupata vyandarua na wengine wananunua kwa bei wanazozitaka madukani na mambo yanakuwa mazuri.

Mhe. Spika, katika sehemu nyengine nataka nizungumzie ni sehemu ya Kitengo cha Elimu ya Afya. Kweli kitengo hiki kina majukumu makubwa sana yakujaribu kuwaelimisha watu katika kujikinga na maradhi mbali mbali. Lakini mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri pamoja na kitengo hiki ambacho ni muhimu sana cha kuelimisha jamii, najua hapa nafasi zinazotokezea ni mbili.

Moja ikiwa ni ndani ya redio na moja ikiwa ndani ya televisheni, lakini tuangalie ni wangapi wenye TV na ni wangapi wenye redio.

Mhe. Spika, hizi taarifa zinakuwa zinapatikana kwa wale ambao wenye matumizi ya vitu hivi. Kwa hivyo, mimi ningelipendelea Mhe. Waziri hapa kwa heshima yako Mhe. Spika, aweze kuweka kamati maalum za kuweza kufuatilia katika maeneo yao, kama ile niliyosema kwamba healthing *inspector* ni muhimu na hii nasema ni muhimu kwa sababu ya kuwaelimisha watu. Mhe. Spika, redio na TV hakiwezi kuwa kigezo kikubwa sana cha kuweza kutoa elimu hiyo kwa sababu sio wote wenye TV na sio wote wenye redio, lakini kama kila eneo kwenye kituo chake cha afya kutawekwa kitengo maalum cha kuangalia watu ambao wanaathirika kwa namna mbali mbali itasaidia pakubwa sana.

Nahisi kwamba mara nyengine yalipofanywa majaribio sehemu nyengine majaribio hayafanywi kwa mfano kama haya majaribio yaliyofanywa kutizama watu ambao wale wameanza kuathirika katika miili yao, wenye miili ya wastani, wenye miili ya kidogo kidogo na wale ambao wameshakuwa katika hali mbaya kiwango ambacho kinaweza kikasababisha maradhi. Kwa nini mambo kama haya na sehemu nyengine hafanywi ikawa sehemu nyengine zinafanyiwa majaribio na sehemu nyengine hazifanyiwi majaribio.

Kwa hivyo, ikiwa suala pahala panafanywa majaribio na sehemu nyengine zifanyiwe, takwimu kama hizi ni muhimu kwa kila Wilaya. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akafanya juhudi kubwa sana ili kupunguza hili. Mhe. Spika, wakati mwengine tunapata wageni wengi ambao wanaingia katika nchi, wakiingia katika nchi hawa vile vile hatujui maradhi wanayokuja nayo. Pia suala hili linaweza kuhudumiwa katika sehemu zao walizo.

Mhe. Spika, sehemu nyengine ambayo nataka kuizungumzia ni suala la kichocho. Mhe. Spika, katika mazungumzo yake mengi amezungumza katika kitabu kuonesha kuna sehemu maalum ambazo zinahudumiwa habari za kichocho. Hii ni athari kubwa sana kwa watoto wetu ambao wale wanaokoga katika mito na katika taarifa za mara hii katika kitabu hatukuona sehemu nyengine kuelezewa juu ya suala la kichocho sisi kwa kipindi hiki kwa Pemba tumepata mvua nyingi sana zaidi ya miezi mitatu mvua ni kubwa, mito yote ilijaa maji na maziwa yote yalijaa maji na penye maji watoto huwa wanakoga. Suala hili ni zito na ni baya kwa watoto lina athiri afya yao mpaka watakapokuwa watu wazima linaweza kuleta athari kubwa sana.

Mhe. Spika, haya maradhi kidogo sio mazuri na huyu anayesababisha ni konokono. Hili suala mimi nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri ni njia gani unaweza ukawasaidia watu walioko katika sehemu hizo za vituo vya afya

ambao wamezungukwa na mito ili kuweza kujaribu kuwauwa wale makonokono waliokuwa sehemu zile na kuweza kutoa ushauri kwa watoto ambao wanakoga sehemu hizo kwani humo ndio sehemu ya mazalio ya wadudu wa kichocho. Kwa hivyo, hili suala ni muhimu nikitaka nimwambie Mhe. Waziri alichukulie hatua ipasavyo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kumuuliza Mhe. Waziri kulikuwa na ile *routine* ambayo baadhi ya maskuli ilikuwa inafanywa kuweza kupita katika mashule kuweza elimu hasa kama hii ya kichocho na elimu kadha wa kadha zinahitajika. Mhe. Spika, naona *routine* ile imekatika sasa katika maskuli, *checking* ya afya ya wanafunzi naona imetoweka. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akafanya jitihada ya kuweza kutoa elimu kwa wanafunzi katika maskuli mbali mbali, ukaguzi wa shule uwepo wa kuangalia maradhi mbali mbali.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa nataka niende katika hospitali yangu ya Konde. Kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watu wote kuwaambia kwamba mimi *alhamdulilah* nashukuru kwa kipindi changu cha miaka mitano nimeweza kufaidika hospitali namna kwa namna. Mhe. Spika, katika kipindi hiki nimeweza kupata hospitali katika *the big five* ambayo hospitali hiyo tunayo Makangale na hospitali moja ambayo ni nzuri kabisa ambayo tayari tumeshaanza kujengewa Konde. Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na kulifuatilia hili suala hospitali ni kubwa, nzuri ambayo itakuwa ya wazazi pengine na *operation*.

Mhe. Spika, kitu ambacho kitakachotutia wasi wasi katika hospitali hiyo, mimi katika Jimbo langu la Konde nina matatizo makubwa sana, mimi nina gari mbili natoa kwa ajili ya wazazi, gari zangu inakuwa ni kama *ambulance* mafuta natoa kwa wingi kwa gari hizo. Kwa hivyo, hili suala ili kutusaidia sisi ningemuomba Mhe. Waziri kwamba aweke gari kwa ajili ya kuchukua watu kuweza kuwapeleka katika vituo vya hospitali hasa kwa wazazi na watoto wadogo.

Mhe. Spika, hospitali hii hatujaambiwa bado lini itafunguliwa lakini nina wasi wasi kwamba hospitali hii kwa daktari aliyepo hawezi kutosheleza. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri akafanya juhudi na bidii ya kutuletea madakatari wa kutosha kwa sababu daktari aliyepo atakuwa hatoshelezi kabisa.

Mhe. Spika, la mwisho kwa kuwa muda umemaliza ni jambo muhimu moja kubwa ambalo nataka nilieleze. Mhe. Spika, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya Ungi ambacho kiko katika Jimbo la Konde. Mhe. Spika, tulimpata Mhe. Rais kuja kufungua skuli ile katika kufungua skuli ile kulikuwa na risala ambayo

wenyewe wananchi walitoa risala ile kwa kumuomba Mhe. Rais kwamba wanamuomba wapate kituo cha afya.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya tangu siku ambayo Mhe. Rais amezungumza maneno yale mpaka hii leo hakuna hatua yoyote ambayo ilichukuliwa kwenye ujenzi wa kituo hicho. Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi baada ya kunifuata na mimi kumuona Mkuu wa Mkoa kumuelezea hili suala kwamba wananchi wanadai hospitali yao. Mhe. Spika, Katibu wa Mkoa ametoa barua kumpelekea Waziri wa Afya napenda kwa ruhusa yako Mhe. Spika, niisome ile barua ambayo ilikuja.

Mhe. Spika, agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume, Mheshimiwa naomba uhusike na mada ya hapo juu. Kufuatia ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliyoifanya tarehe 14/12/2009 kwa ajili ya ufunguzi wa Skuli ya Ungi Msuka aliniagiza kufuatia ombi la wananchi katika risala yao katika Kituo cha Afya alinitaka nikuandikie barua wewe ili wajengewe kituo hicho. Kwa barua hii naomba utekelezaji wa agizo hilo ufanyike ili wananchi wa eneo hilo waweze kuondoa kilio chao na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi uweze kukamilisha mambo haya. Nawasilisha kwa hatua zako. Dadi Faki Daki.

Mhe. Spika, hii ni barua ambayo ilikuwa imepelekewa Mhe. Waziri. Labda nimuulize tu Mhe. Waziri je, barua hiyo umeipata na kama barua hiyo umeipata ningeomba Mhe. Waziri uweze kuichukulia hatua ili kwa ujenzi wa Kituo cha Afya Ungi Msuka Jimbo la Konde.

Mhe. Spika, nakushukuru na mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Kwanza awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote jioni hii ya leo kuweza kuhudhuria hapa katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya kujadili hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kutayarisha hotuba hii nzuri, pia kwa kufanya kazi ngumu ya kusimamia wizara hii katika mazingira magumu.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni wizara ambayo ina umuhimu wa aina yake na kwa sababu ndio iliyobeba dhamana juu ya afya za watu. Mhe. Spika, taifa ambalo lina watu wagonjwa wagonjwa wasiokuwa na afya maana yake taifa hilo litakuwa halina maendeleo. Kwa hivyo, wizara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha watu katika nchi hii wanakuwa na afya, wanakuwa wazima na wanaweza kufanya zao za kila siku.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tunapozungumzia juu ya jambo au tunaposisitiza juu ya jambo fulani maana yake jambo hilo lina umuhimu mkubwa wa aina yake, na inakuwa si vyema kwamba jambo hilo likapuuzwa bila ya kuzingatiwa. Pamoja na kwamba moja kati ya kazi zetu ni kusema lakini hatusemi tu, isipokuwa tunasema yale mambo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi, yanayohitaji kufanyiwa kazi yafanyiwe kazi na yale yanayohitaji kufanyiwa kazi baadae basi yafanyiwe kazi baadae kwa sababu yanakuwa na uzito wa aina yake.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake amezungumzia changamoto mbali mbali zinazomkabili katika wizara. Mimi nataka nimpongeze sana kwa sababu hii ni mara ya kwanza katika hotuba zake kuelezea jambo hili. Ameelezea kwamba miongoni mwa changamoto ambazo zinamkabili katika wizara yake ni upungufu wa wafanyakazi pamoja na maslahi yao, ufinyu wa bajeti ya wizara yake. Kwa kweli haya ni mambo ambayo yapo, na tumekuwa tukiyazungumzia mara nyingi. Lakini kama nilivyotangulia kusema kwamba tunapoyazungumzia maana yake serikali kuu iweze kuyaona.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba tutakuwa tunawasilisha mapendekezo yetu kwa waziri anayehusika, lakini mambo haya ya bajeti juu ya Wizara ya Afya tumekuwa tukiyazungumza kila wakati. Mhe. Spika, utaona kwamba tunamwambia Waziri wa Afya kwa sababu ndio wizara yake, lakini lengo ni kuiambia serikali. Mimi naamini kwamba Mhe. Waziri angependa awe na bajeti ya kutosha yakuweza kukidhi haja ya mambo yake yote ili mambo yote anayojipangia yaende vizuri.

Mhe. Spika, tunaiambia serikali kwamba wizara hii ina umuhimu wa aina yake, wanapotenga bajeti katika wizara mbali mbali basi wizara hii inastahiki kupewa kipaumbele kinachostahiki. Mhe. Waziri Kivuli hapa alisema kwamba bajeti iliyotengwa safari hii ya Wizara ya Afya ni asilimia 4 mimi sijafanya mahesabu lakini asilimia 4 ya bajeti ni kiwango kidogo mno ukilinganisha na umuhimu wa jambo lenyewe. Kwa hivyo, tunasema kwamba suala la bajeti katika wizara hii ni muhimu, bajeti iongezwe ili iweze kukidhi haja ya wizara hii muhimu. Tunapozungumzia bajeti kwa wakati huu haina maana ya bajeti hii iliyopita lakini tuangalie bajeti zinazokuja usoni ili tusijetena tukawa tunazungumzia jambo hili. Kwa hivyo, Mhe. Waziri na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Fedha yupo hapa anatusikia kwamba keki yake ni ndogo lakini kipaumbele kinahitajika sana katika wizara hii ili wananchi waweze kuhudumiwa na afya zao na mambo mengine yanayostahiki.

Mhe. Spika, suala la upungufu wa wafanyakazi nalo ni miongoni mwa mambo yanayosababishwa na ufinyu wa bajeti pia. Kwa hivyo, ikiwa bajeti ya Wizara ya Afya itakuwa ni nzuri fedha za kutosha basi haya matatizo ambayo

tunayazungumza hapa yataondoka ikiwemo suala la maslahi ya wafanyakazi. Maslahi ya wafanyakazi Mhe. Spika, ni muhimu na kwa sababu kwa kweli kada hii ya afya ni kada ngumu kweli kweli kukaa kumuhudumia mgonjwa ambaye pengine wala sio jamaa yako wala humjui, pengine ana maradhi mabaya sana kwa kweli jambo hili linastahiki kupongezwa sana hawa wafanyakazi. Kwa hivyo, kwa kweli wanastahiki kulipwa mafao yao yanayostahiki, maslahi yao yawe mazuri ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Mhe. Spika, wenzangu hapa wametangulia kuzungumzia juu ya *scheme of service* ambayo kila wakati tumekuwa tukizungumzia sasa imekuwa kama hadithi. Mhe. Spika, lakini utekelezaji wa jambo hili inaonekana ni mgumu kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kwa kweli jambo hili alizungumzie na alisimamie ipasavyo na bila ya kusimamia ipasavyo kila siku itabakia kuwa ni nyimbo, bajeti hii tutaambiwa *scheme of service* tayari lakini matokeo yake hakuna chochote kinachoendelea.

Mhe. Spika, jengine kuna suala la usafirishaji wagonjwa nje ya nchi, hili nalo ukilitizama nalo linahusu zaidi ufinyu wa bajeti. Hapa Mhe. Waziri ametueleza kwamba katika kipindi cha mwaka 2009-2010 kuna jumla ya wagonjwa 73 ambao wamesafirishwa nje kwa ajili ya maradhi ya figo, moyo na mambo mengine na kiasi cha dola za Kimarekani 369.000 zimetumika. Mimi nilitaka kujua Mhe. Spika, fedha hizi zipo katika bajeti hii ya Wizara ya Afya au zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa sababu sijaziona kama zimo basi atatueleza.

Mhe. Spika, jengine ni suala la hawa wagonjwa wa figo ambao wamekuwa wakisafirishwa nje ya nchi na kufanyiwa operesheni. Kwa kweli wagonjwa wa figo wanahitaji kufanyiwa kliniki maalum na kwa sababu dawa zao ni ghali kweli kweli, wale waliokwenda kufanyiwa operesheni wakarudi wanagharamika sana kununua dawa, wengine wanatoka hapa wanakwenda Dar es Salaam kwa sababu hapa bado hatujaweka kitengo maalum cha kuwashughulikia hawa wagonjwa wa figo.

Mhe. Spika, kwa kweli kama mtu hana uwezo akipata maradhi haya ya figo hata kama ameshafanyiwa operesheni basi anaweza akapoteza maisha kwa sababu kila siku unatumia madawa na ni madawa ya kudumu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri suala la wagonjwa hawa wa maradhi ya figo ambao tayari wameshafanyiwa operesheni huko nje wanaporejea hapa basi wawe wanapewa uwezo ili kuweza kununua zile dawa za kuweza kukidhi haja yao.

Mhe. Spika, vile vile katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa kweli katika hospitali hii wenzetu wanajitahidi lakini bado hali ya usafi hairidhishi, jitihada

zaidi zinahitajika kuona majengo yetu yanakuwa katika hali inayoridhisha. Mhe. Spika, ni kwamba hali bado hairidhishi tunapokwenda pale hospitali mimi binafsi kwanza nakuwa siridhiki na hali ya usafi uliokuwepo pale hasa ukitizama kwamba ile ni hospitali. Mhe. Spika, hospitlai panahitaji pawe mahala pa mfano kwa watu wengine. Kwa hivyo, juhudi zaidi pamoja na ufinyu wa bajeti lakini juhudi zaidi zinahitajika kuona majengo yetu yanakuwa katika hali ya usafi.

Mhe. Spika, jengine hapo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja umeme unapokatika. Kwa kweli Mhe. Spika, pana jenereta pale ambayo umeme unapokatika basi huwashwa jenereta lakini chakusikitisha kwamba unapozimika umeme basi yule muwashaji jenereta anakuwa hayupo afuatwe nyumbani au apigiwe simu. Kwa hivyo, inachukua muda pengine na yeye ni binadamu ana shughuli zake inachukua pale panakuwa giza na mahala ambapo kama pale pana watu wengi na huduma nyingi hebu tuangalie hali inavyokuwa.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri yule muwashaji jenereta na kulingana na hali yetu ya umeme tunajua wa kukatika katika basi aweko pale ili umeme unapokatika na yeye apatikane wakati ule ule awashe jenereta ili shughuli zote ziende pamoja kwa sababu kukaa giza pale robo saa tu katika hospitali ile ni jambo ambalo ni la hatari. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa makini.

Mhe. Spika, kuhusu suala la michango ile ambayo wenzangu wametangulia ya operesheni ya kina mama wajawazito. Mhe. Spika, mimi nataka tumuombe sana Mhe. Waziri ada hii haiondoshe kwa sababu ya maslahi ya watu na jambo lenyewe na hali halisi ilivyo, ni bora atafute mbinu nyengine za kutafuta mapato lakini ada hii ya operesheni kwa ajili ya kina mama wajawazito kwa kweli inatusononesha sana na tumekuwa tukiizungumza kila mara. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atafute njia nyengine mbadala ya kupata fedha hizi kwa ajili ya kufanya shughuli nyengine, lakini ada kwa ajili ya kina mama hawa wajawazito basi iondoshwe kabisa ili tuone tunakwenda vizuri.

Mhe. Spika, jengine ni suala la Mradi wa Hifadhi wa Nyumba za Wazee. Mimi nashukuru na naipongeza serikali kwamba imekubali kutenga kiasi cha shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo zile nyumba za wazee. Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, kwa kweli nitaangalia namna fedha zile zitakapokwenda lakini niwaombe sana Mhe. Waziri basi angalau fedha zile zinaweza zikakidhi kwa matengenezo ya jengo moja wasitengeneze yote, washike jengo moja walitengeneze limalizike mwakani Mhe. Dk. Mwinyi anaweza kutuongeza kama milioni mia mbili basi tutatengeneza majengo mawili ilimradi tuone yale majengo yanatengenezwa na kuwa yanakuwa vizuri.

Mhe. Spika, jengine wale wagonjwa wanaokatwa miguu kutokana na kisukari. Kwa kweli wagonjwa wanaokatwa miguu kwa ajili ya maradhi ya kisukari wengi wao baadae hupoteza maisha. Sasa hatuelewi ni kwa nini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu tueleze kwa nini wagonjwa wanaofanyiwa operesheni ama kukatwa miguu baada ya muda mfupi huwa wanafariki dunia kuna tatizo gani? Ni utaalamu au tunachelewa kuwafanyia operesheni.

Mhe. Spika, la mwisho kwa kuwa muda wako umemalizika ni suala la kiwanja kile ambacho kimetolewa kule Binguni kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kuu.

Kwa kweli Mhe. Spika, Mhe. Waziri hebu atueleze suala la ujenzi ule wa hospitali kule Binguni limefikia wapi? Kwa sababu kiwanja kile sasa hivi kipo na kuna hatari watu wakaanza kuvamia katika eneo lile. Kama bado serikali haijapata uwezo wa kujenga hospitali basi angalau kizungushiwe uzio ili tuone kwamba eneo lile linahifadhika na hapo tutakapopata mfadhili tujenge hospitali kama kawaida, isije ikawa kama kiwanja cha Mbweni.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata hii nafasi fupi na nitajitahidi kwenda haraka. Kwanza nitoe shukurani kwa Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa namna ninavyoishuhusia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii leo. Katika kipindi chote nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na wizara hii nilikuwa nikiifanyia kazi. Imefanya mabadiliko makubwa, imeonesha maendeleo makubwa na mengine tumeyashuhudia sisi wenyewe naipongeza wizara kwa hilo.

La pili Mhe. Spika, kitabu kimeandikika, kimesomeka na takriban mengi yamejieleza. Lakini kwa kuweka mambo mazuri zaidi katika kusoma kwangu kidogo nimekuta baadhi ya mambo ambayo hapa yanasimama kwa kutaka ufafanuzi tu. Nimekwenda moja kwa moja kwenye viambatisho.

Kwa hivyo, kwanza kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naanza kiambatisho 2.4 kwenye ukurasa wa 112. Kiambatisho hiki kinaelezea kuhusu wanafunzi wanaoendelea na masomo katika Chuo cha Afya Mbweni. Katika kukiangalia kwangu kuna mambo kidogo nataka nipewe maelekezo. Hapa pana kada nyingi zinazofundishwa katika kituo hicho cha afya, lakini kwa ufupi tu nikianza kada ya wauguzi, mwaka wa kwanza walikuweko 145, mwaka wa pili hakuna hata mmoja, mwaka wa tatu 113 na mwaka wa nne 57. Kwa hivyo, hapa kuwa mwaka wa pili hayupo hata mmoja kidogo naomba maelezo.

Clinical Officer ni hivyo hivyo, mwaka wa kwanza 79, mwaka wa pili hamna kitu, mwaka wa tatu 56 na mwaka wa nne hamna.

Pharmacy mwaka wa kwanza 70 lakini mwaka wa pili hamna kitu, mwaka wa tatu 42 na mwaka wa nne hamna kitu. *Environment Health Officer* mwaka wa kwanza 71, wa pili 0, wa tatu 49, wa nne 0 katika. *Dental Tchnician* mwaka wa kwanza hakuna, wa pili hakuna, lakini wa tatu 11 na wa nne hakuna. *Laboratory Technician* mwakwa wa kwanza 75, wa pili hamna, watatu ni 114 na wa nne hamna. Mwisho *Public Health Nurse "B"* mwakwa wa mwanzo hakuna mwanafunzi hata mmoja, lakini wa pili kuna 97, watatu hamna na wanne hamna. Na hii idadi ya chini ni 979 sijui inatokea wapi. Kwa hivyo, hiyo ni moja nataka maelezo.

Halafu Mhe. Spika, katika kiambatisho Nam. 5.3 kinachotoa taarifa ya hali ya uzazi katika wodi ya wazazi Hopitali za Mnazi Mmoja na Mwembelangu kuanzia Julai, 2008 – Machi, 2009. Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja jumla ya wajawazito waliolazwa 7,445, pamoja na maelezo mengine kuna 24 walikufa. Lakini Mwembeladu hakuna hata mmoja, pamoja na kuwa wao hawakuelezea kuwa wanafanya kazi ya upasuaji. Nataka kujua katika wote hawa 3,467 wajawazito waliolazwa hakukuwa na kifo nashukuru, lakini tukiangalia kule kuna 24, sijui hapa wizara ilifanya utafiti gani? Kwa hivyo, vifo vingi vinavyotokea ni katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Halafu kiambatisho 6.1, hiki kinaeleza kuhusu mahudhuria ya wagonjwa wa nje waliolazwa na waliofariki katika Hospitali za Idara ya Tiba kuanzia Julai, 2009 – Machi, 2010. Kwa bahati mbaya wale waliofariki hawaonekani hata mmoja wakati kwenye maelezo wamo. Kuna wagonjwa wa nje na waliolazwa lakini wale waliofariki hawapo. Kwa hivyo, tungeliwapata na hawa waliofariki tungepata takwimu sahihi na kujua namna gani shughuli zetu za tiba zinaendelea. Na hii nayo nataka maelezo.

Nikiendelea Mhe. Spika, ukurasa wa 132 kuna kiambatisho Nam. 12.6 kinachohusiana na mahudhurio katika huduma ya mama baada ya kujifungua katika kliniki, yaani kuanzia mwezi wa Julai, 2009 – Machi, 2010. Kwa bahati mbaya Wilaya ya Wete hakuna hata mmoja, wakati wilaya nyengie zote tisa zilizobakia zina idadi yake. Nataka kujua huku Wete kuna nini?

Sio hilo tu, kiambatisho Nam. 12.8 kinachoonesha idadi ya wajawazito waliyoonekana na vidokezo vya hatari katika kliniki kuanzia Julai hiyohiyo 2009 – Machi, 2010, Wilaya ya Wete hamna kitu. Ninataka kujua kwa nini wilaya zote tisa zina takwimu zake. Hiyo Mhe. Spika, ni upande wa viambatisho.

Jengine Mhe. Spika, katika kutembelea na wana kamati wenzangu kwenye taasisi mbali mbali za wizara nitoe shukurani kuwa tumeona namna Mhe. Waziri anavyojitahidi na kuimarisha hii Sekta ya Afya. Lakini kuna baadhi ya mambo tuliyakutia na niliposoma malengo makuu ya wizara kwa kipindi hiki cha bajeti kinachokaribia cha mwaka 2010/2011 sikuyakutia.

Kwa mfano, tulitembelea Hospitali ya Wete na Hospitali ya Abdalla Mzee. Pamoja na kuwa kitabu kinaeleza juhudi nyingi wizara iliyochukua ya kufanya matengenezo mambo mengi, lakini nakumbuka tuliambiwa kuwa hospitali mbili hizi kila moja inavuja na humu sikuona kuwa Mhe. Waziri kaeleza kuwa kutakuwa na matengenezo ili isivuje tena. Kwa hivyo, naomba kujua Mhe. Waziri kachukua hatua gani kwa hospitali zetu mbili hizi kubwa tunazotegemea ikiwa zote zinavuja.

Pia ni suala la kila siku tulikuwa tikilipigia kelele kuhusu Hospitali ya Aballa Mzee, kuwa kule kuna kiwanja kishapatikana na tokea zamani kulikuwa na azma ya kujengwa wodi ya watoto. Ni kweli kiwanja kiko lakini naona katika malengo hili suala sikuliona wakati *Abdalla Mzee Hospital* ndio hospitali yetu kubwa ya rufaa kwa kule Pemba tunaitegemea kweli kweli. Ikiwa haina wodi hii naona itakuwa ina mapungufu makubwa sana, hasa kwa maana ya kuwa ni watoto. Kwa hivyo, ninataka kujua Mhe. Waziri hili suala la kujenga ile wodi ya watoto pale Hospitali ya Abdalla Mzee kaichukulia vipi.

Jengine kwa bahati mbaya niliiomba sana kamati yangu kutembelea kituo chake pale Mzambarauni katika Jimbo la Mtambwe. Lakini kwa sababu ya ufinyu wa wakati na kazi nyingi iliyopangiwa haikuwezekana. Namwambia tu Mhe. Waziri kuwa hiki kituo kinatumika katika eneo kubwa. Kwa bahati mbaya kiko katika hali mbaya, kina nyufa, kuna matatizo katika vyoo na kadhalika. Kinahitaji matengenezo makubwa sana hivyo naomba msaada wake.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake na kujenga nyumba 40 ishirini Pemba, ishirini Unguja za madaktari katika vile vituo ambavyo viko mashamba na vyenye shida kubwa sana. Lakini kwa bahati vituo ni vingi na nyumba zilizopatikana ni 20 tu kwa Pemba na 20 kwa Unguja. Mpaka hivi sasa tuna vituo vya afya ambavyo viko shamba hakuna nyumba za daktari na hao madaktari wanaopelekwa kutokana na masafa wanayokaa wanalazimika kuchelewa sana kufika.

Kwa mfano, nilipata taarifa Kituo cha Uzini ni kimoja kwa hapa Unguja na kule Pemba ni vingi lakini kwa hapa nitazungumza kuhusu kituo changu cha Uondwe. Mhe. Waziri kituo hiki cha Uondwe ni kituo kikubwa sana na kina wapiga kura takriban thuluthi tatu katika tano ya wapiga kura wote wa jimbo. Kinatumika sana na wanakuja wagonjwa wengi kweli kweli, lakini kwa bahati

mbaya hatujapata daktari mwenye uwezo anayekaa katika eneo lile. Kwa hivyo, mara nyingi huwa tunapata madaktari kutoka nje ya jimbo na hasa kuwa wanatoka Wete, kufika kwao mpaka baada ya kuvuka inachukua muda mrefu sana.

Kwa hivyo, mimi ombi langu kwa Mhe. Waziri ni kuwa, kama itatokezea mpango wowote na mimi niko tayari kuanzisha, pale Kituo cha Uondwe napo pajengwe nyumba ya daktari. Lakini kwa dharura hivi sasa iko nyumba nzuri tu ya kisasa na *Alhamdulillah* maji yako, umeme uko wa uhakika, ningeliomba basi kama hali itaruhusu na ingelimruhusu ndivyo ninavyoomba hasa, tuone kuwa yule daktari wetu aliyetuletea tumpatie nyumba pale ili tuweze kupata huduma inayostahiki na kwa wakati wote.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati naona nimalizie hapo ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nikushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni. Mhe. Sp ika, naomba nitumie nafasi hii adhimu kuwapongeza kwa dhati madaktari wa Hospitali ya Wete kwa kazi nzuri waliyoifanya kuokoa maisha ya mtoto Arkam Ibrahim Said.

Mhe. Spika, mtoto huyu alianza matibabu Hospitali ya Mnazi Mmoja Unguja hali ikazidi kuwa mbaya akapelekwa Dar es Salaam mambo yakawa magumu zaidi, akaondoka hapo Muhimbili akapelekwa Hospitali ya Tumaini hatimaye kaja kutibiwa Hospitali ya Wete Pemba Wilaya ya Wete. Sasa hivi anaendelea na afya yake vizuri.

Mhe. Spika, wengi tulikuwa tukiwalaumu madaktari wa hospitali zetu Pemba, kumbe lawama zile hazikuwa sahihi, lawama tunaona inawahusu watendaji wa wizara hii, Idara ya Mipango na Sera. Hospitali zinazoshughulika na tiba ni Kivunge, Makunduchi na zile tano za Pemba.

Hali ya hospitali zetu Pemba zinatajwa na wenzangu wengi, lakini nitasimamia hii ya Wete hasa wodi ya watoto. Mhe. Spika, bajeti iliyopita nilipiga kelele nyingi kuhusu vitanda vya watoto, mama ama wanaowahudumia wao hawana mahali pa kupumzikia, hawezi mtu masaa 24 akakaa na mtoto bila ya kusinzia, anaweza kukaa pale wiki moja au mbili, hapo anapotandika kulala chini maneno mengine magumu hayafai lakini hastahiki binadamu kulala kwa uchafu. Ile wodi ni chafu, watoto kama tunavyowajua ni watoto miili yao haistahamili vishindo vya maradhi, hali iliyoko kule haifai, vyoo mtihani.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri muda wangu wa miaka mitano yote napiga kelele juu ya hospitali hii ya Wete kwa mapungufu mengi hasa haya ya daktari wa upasuaji, daktari wa akinamama na huyu wa watoto. Kuna usemi

unasema, “Msi watu ana Mungu”, wanapona kwa sababu ya rehma na zile imani za wale wanaowasaidia. Lakini sitaki nitumie maneno mabaya, wenzetu hawa wanaopanga vifungu vya matumizi hebu Mhe. Waziri kesho hatuji hapa, nakuomba sana Jumapili tunamaliza wizara hii uje na majibu sahihi ni kwanini *a location* za hospitali ya Wete, Chake Chake, Mkoani, Vitongoji, Micheweni zikafanywa hivi zinavyofanywa.

Mhe. Spika, mtiririko umo humu muda hautoshi, lakini haturidhiki hata kidogo hali hii kuiona hivi ilivyo sasa. Nataasaf na mimi kusema nitazuia fungu hili kama Mhe. Waziri hakunipa majibu maridhawa. Hali ni mbaya mno, kumbe wenzetu hawana hata sabuni za kutumia? Mambo yenyewe ndio haya.

Mhe. Spika, nije haraka haraka hapa kwenye huduma za uzazi. Mhe. Spika, tumesema sana na leo nitarudia, uzazi ni suala gumu, zito. .Mhe. Spika, sasa hivi hata Hospitali yetu ya Rufaa Mnazi Mmoja wananchi wetu wanaogopa kwenda kujifungua, si hizi shilingi 40,000 tu ambazo tumemwambia Mhe. Waziri hebu ziondoke, wala hatupotezi chochote sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu hapakuchangiwa shilingi 40 elfu ya mzazi aliyefanyhiwa operesheni. Mhe. Spika, pesa hii ni kubwa, umasikini umekithiri nchini hapa, shilingi 40, 000 nyingi, lakini kuna wasi wasi mkubwa hii pesa.

Mhe. Spika, mtu anaumwa kaugua mara mbili ni kisu. Tunayasema haya kwa sababu sisi ndio tunaopeleka wagonjwa, waliopo mama huruma na Mhe. Waziri huwa namtaja sana mama huruma na sisi tunasema hayupo na kama yupo yuko huko anakomjua yeye, anauliza mgonjwa yule pesa keshaleta? Anamtaja mgonjwa fulani pesa keshaleta? Ndio kavaa *tracksuit* hana koti lile jeupe. Kwapu kwapu mfukoni zinawekwa, tunashuhudia, utaratibu ule haturidhiki, ile pesa iandikiwe tutaona kwamba ni kweli imekwenda inakofaa. Mhe. Spika, haya yapo lakini tuasem kiujumla kwamba, 40,000 kama ni ada, ama kuchangia, kama ni vyovyote vile tunaomba iondolewe wazazi hizi hawana wala hatutaki kulisikia. Kama tutakosa kufanya shughuli zetu sisi kama serikali kwa pesa hii, mzazi keshachangia mengi makubwa yanatosha hii iondoke Mhe. Waziri hatuitaki wala usiitaje tena.

Jengine Mhe. Spika, karibuni nilikwenda kuwaona jamaa zangu Chaani, haya mambo tunayasema kwa hasira kwa sababu yanauma. Nimekwenda Chaani nimemkuta mgonjwa mzazi karudi hospitali Kivunge, hajamaliza uzazi. Sasa karejeshwa pale nyumbani patafutwe cha kupatikana aletwe Mnazi Mmoja kule hawamuwezi tena. Mimi nimetokea nimeelezwa ile kesi zipatikane lita 15 aletwe hapa mjini. Nikenda hospitali nikalipa pesa za lita 15 za mafuta. Kilichotokea *Ambulance* imekuja kumchukua pale nyumbani karejeshwa pale pale Kivunge na kafanyiwa yote ambayo angekuja kufanyiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na akarejeshwa tena pale nyumbani kuna nini?

Sasa tunapoyasema haya Mhe. Spika, hatusemi ‘kalamulaily’ tunayasema kwamba yapo. Mhe. Waziri ayafuatilie bila kukinga kifua kwanza, ayafuatilie, ayaone au aje atusute lakini asikinge kifua. Tunayasema sisi kwa kumtakia heri na fanaka kubwa. Kwa sababu mara hii hakuwa miongoni mwa wanaochukua fomu, lakini *Inshaallahutaala* huko twendako tunamtarajia na yeye. Kwa hivyo, Wazanzibari wapate imani kutoka kwake. Na mimi *Inshaallah* kama nitakuwa niko hai na tukijaaliwa Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo asaakunheri keshokutwa akafanya mambo hapo atamrithi, hakuna wasi wasi.

Lakini hili la uzazi shilingi arubaini elfu Mhe. Spika, ziondolewe na Idara ya Tiba kwa hospitali za Pemba Mhe. Waziri ukae na watendaji wako tunataka majibu sahihi.

La mwisho tukijaaliwa kwa leo, Chuo cha Afya Mbweni nasikia kuna mtu hapo hapo hapana Waziri, Mkuu wa Chuo, hakuna Katibu Mkuu hapo, yeye ndiye yeye tu, tunataka kumjua ndiye nani hasa. Maana sasa imekuwa nimno, kijana *Form III* hakufaulu chochote yuko pale. Waliofaulu mara mbili Mhe. Spika, wawekwa upande. Nasema haya kusudi nampa *challenge* Mhe. Waziri. Katika chuo hiki Mhe. Waziri kuna mtu ana vituko hatutaki sifa hizi zikuangukie wewe tunakuhitaji tukijaaliwa *Inshaallah*.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwanza nipongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Madaktari wote ambao wanamsaidia Mhe. Waziri kuongoza wizara hii na nimpongeze na wafanyakazi wake wote. Kwa sababu Mhe. Spika, ziko kazi tunafanya hapa duniani lakini malipo zaidi tunayapata huko tunakokwenda na moja katika kazi hizo baada ya ualimu na kazi hii ya kutibu wagonjwa. Kwa sababu wenzetu wanachukua jukumu kubwa la kuweza kutibu na ahsante huwa hawapati sana hupata lawama.

Lakini ukitaka kuona mfano mdogo tu wa kujua kuuguza kuwa ni kugumu, sisi sote hapa hutokezewa na wagonjwa maujumbani mwetu, basi tangu hupangiana zamu mpaka tukakimbiana kutokana na ugumu wa kuuguza, lakini wenzetu kwa kuwa wao ndio wameajiriwa wanapiga kifua konde na wanajitahidi kadiri ya uwezo wao. Mimi nawaombea Mwenyezi Mungu awajaalie waendelee kufanya kazi hiyo kwa moyo wao wote.

Mhe. Spika, nikiingia kwenye bajeti yenyewe sasa hivi nije kwenye ukurasa wa 39 kifungu 7.0 kinachozungumzia Idara ya Ustawi wa Jamii. Tunaambiwa idara hii inashughulikia zaidi kutoa huduma ya kijamii kwa watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wazee wasiojiweza na kadhalika. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa katika jitihada hizi na baadhi ya watu nao hukereketwa katika kusaidia mambo kama haya.

Mimi katika jimbo langu hivi sasa kuna vikundi viwili vimejitolea wenyewe na wanachanga fedha kutoka mifukoni mwao na kuomba kwa wadau mbali mbali, wanasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Hivi sasa wameanza kutoa misaada katika Skuli ya Chuini kusaidia sare, madaftari na kalamu. Wana mpango wakitoka skuli hiyo wende Skuli ya Mbuzini wazunguke shehia zote za Jimbo la Mfenesini.

Sasa naomba kama kuna wahusika wa suala hili basi tukimaliza bajeti tuonane na mimi isijekuwa tunafanya mambo pengine kinyume na utaratibu ama tunakwenda njia sizo. Kwa hivyo, tupate maelekezo na niwakutanishe na vikundi hivyo ili kama kuna mchango wa aina yoyote waweze kuwapa muongozo hao ambao wamejitolea kufanya suala hili.

Nikiendelea katika sehemu ya wazee wasiojiweza, tunashukuru kwamba wazee wamejengewa nyumba Sebleni, mwenzangu aliyemaliza alizunguzma. Ninachoomba mimi hivi sasa kwamba zile nyumba ziko wazi sana, sasa hivi wanyama wanaingia katika nyumba zile wanawakera.

Wanyama wa mjini sasa hivi wakikuta wali wanakula, ng'ombe anakula wali, mbuzi anakunywa mchuzi, sasa mzee anaweza kufunika wali wake katoka mara moja kuanua nguo yake anakuta wali mbuzi keshaula tunamlaza na njaa. Sasa ningelishauri kwa sababu nilikuwa nasikia huko nyuma kulikuwa na mfuko ulitolewa ujengwe uzio kuzuia angalau wale wanyama wasiingie ndani ya lile jengo. Sasa sijui suala hili limeishia wapi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kama zile fedha zimepatikana au zimekosekana basi angeziomba tena ili tukawajengea uzio wale wazee wakaweza kunusurika angalau ile riziki wanayoipata wakapata kuila kwa nafasi. Pia wazee hawa tunawasaidia fedha angalau za sabuni au kapungukiwa na chakula aweze kutumia. Lakini siku nyingi tunasema fedha hizi ni ndogo na tunamuomba waziri bado na hili alipigie kifua ili wasaidiwe wazee wapate pesa angalau kutoka shilingi 20 basi zifike shilingi 50 elfu na wataweza kuishi kwa uhakika na watakuwa hawana wasiwasi.

Mhe. Spika, *point* yangu ya pili inakuja ukurasa wa 57 kifungu cha 6.1.2 kinachohusika na usafirishaji wa wagonjwa kwenda nje. Kwanza niishukuru

serikali kwa kuweka kitengo hiki na pia niishukuru wizara. Kwa bahati nzuri mimi nishapata nafasi hizi mara mbili, nilikuwa na wajomba zangu mmoja alizaliwa na moyo mkubwa mwaka juzi akasafirishwa, sasa hivi kawa mzuri na anasoma darasa la pili. lakini hivi karibuni pia kuna mjomba wangu mwengine mwanawe alikuwa kazaliwa kafika mwaka na nusu hajaweza kutambaa wala kwenda na hata kula kwake kwa tabu. Lakini bahati nzuri kasafirishwa hivi sasa ana miezi mitatu tangu kurudi kawa mtundu ajabu kuliko watoto wote, anakula vizuri, anatembea kwa hivyo tunashukuru sana.

Ninachokiomba ni kwamba ile *process* yake ni ndefu tangu kuanza kuomba, kujulikana matatizo yake, mpaka kasafirishwa. Tulikwenda mpaka tukakata tamaa, lakini Mwenyezi Mungu analoliandika halifutiki. Siku imefika kenda na karudi mzima. Kwa hivyo, naomba kama kuna utaratibu zaidi mwepesi basi ungefanywa kuliko huu ulioko sasa hivi. Nadhani nikisema hivyo Mhe. Waziri kaelewa.

Mhe. Spika, *process* inakuwa ndefu pengine miezi miwili mpaka minne wewe unafuatilia safari ya kwenda nje tu huku maradhi yanazidi kumuathiri yule mgonjwa. Sasa naomba kama kuna njia fupi ya mara moja ingefanywa ili wagonjwa wakenda kwa nafasi na wakarudi kwa nafasi vile vile.

Mhe. Spika, sina mchango mkubwa lakini niliona na mimi lazima nizungumze kidogo kwa sababu hii ni wizara ya sahibu wangu. Mhe. Spika, nije ukurasa wa 70 Bodi ya Ushauri ya Hospitali za Binafsi. Mhe. Spika, nashukuru kwamba wizara imeweka bodi hii na kwa hotuba hii niliyoiona hapa imesaidia sana. Kwa sababu inasema kwenye kifungu 11.1.4 kwamba baadhi ya hospitali hizi zimesimamishwa kwa kasoro zilizoonekana.

Mhe. Spika, kasoro hizo ilikuwa moja ni kwamba wale madaktari dhamana wanakuwa hawafiki katika kile kituo bali wanakuwepo wanafunzi ndio wanaohudumia wagonjwa. Lakini pia wanauza dawa zimeshapitwa na muda sasa hili ni hatari sana. Kwanza kumpeleka mtu anayejifundisha lakini mwalimu hayupo, pia kuuza dawa ambazo zimeshapita muda. Nadhani haya yote mawili ni ya hatari sana kwa binadamu. Sasa napongeza kwamba hili wameliona.

Lakini kuna hospitali za binafsi nyengine wamefanya makosa kama hayo wamepewa onyo, mimi naona mambo kama hayo si ya onyo tena, zifungwe, wajirekebishe, zikaguliwe, halafu ndio wapewe kibali cha kuendelea na kazi. Nadhani wote wakifanyiwa hivyo basi kila mtu anayefungua hospitali kama hizi ataweka indhari kubwa kwa sababu kumhudumia binadamu halafu ukamfanyia masihara inakuwa ni tatizo. Kwa hivyo, naomba bodi hii iendelee na kazi hizo na kila hospitali ambayo haifuati taratibu za kisheria kama

iliyowekwa, basi tusimtazame mtu usoni bali ifungwe kwa mujibu wa sheria. Pale anapojirekebisha apewe kibali chake aweze kuendelea.

Mhe. Spika, naipongeza pia wizara kwa kuweza kunijengea nyumba ya daktari katika eneo letu la hospitali ya Selem Mfenesini. Tunashukuru sana kwa sababu tulikuwa tuna kilio kikubwa. Sasa hivi Mfenesini ni mji mdogo kama ilivyo Konde bado tu haujatangazwa, lakini tayari umeelekea kimji, pana Kituo cha Polisi, Mahakama, skuli mpaka kidato cha nne, hospitali na nyumba ya daktari. Mhe. Spika, naomba hii nyumba ije kufunguliwa na daktari aweze kukaa ili aweze kutoa huduma.

Lakini pia Mhe.Spika, kwa kuunga mkono katika kutoa huduma za afya sisi wenyewe wananchi wa Jimbo la Mfenesini tumejenga hospitali mbili tukishirikiana na halmashauri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tukimaliza bajeti yeye, Katibu Mkuu na atakayependa waje wakague hospitali hizi. Pamoja na kuwa tumekwama lakini ukwamaji wetu uko katika hatua za mwisho. Tumejenga moja katika kijiji cha Chuini hii tayari tumeshaezeka, tumeshatia milango, sasa hivi tunapiga *plaster* na *ceiling* tumalize *floor*, tukukabidhi ili uweze kututilia vifaa na madaktari.

Mhe. Spika, nashukuru Wizara ya Fedha imetusaidia sana kupitia miradi midogo midogo. Lakini hii tuliyoijenga Mkanyageni tukashirikiana na halmashauri ni hospitali kubwa inaweza kulaza wagonjwa 10 mpaka 15. Sasa hii kidogo tumeijenga tumeitia milango na madirisha tumekwama *plaster, floor, ceiling* na rangi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tukimaliza bajeti nimpeleke ili kama kuna uwezo wowote wa kutusaidia aweze kutusaidia.

Mhe. Spika, pia katika ukurasa wa 94 nizungumzie juu ya Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto. Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza lakini na mimi kwa kuwa ni mzazi bado nimeona nizungumze. Mhe. Spika, imeelezwa taarifa hapa kwamba panafanywa mikakati ya kutolewa taaluma ili angalau tupunguze vifo vya mama na mtoto ambavyo hivi sasa inafikia 130 kwa watu laki moja. Mhe. Spika, nadhani si hatua mbaya sana lakini tungezidi kuishusha zaidi ya hapa ingelikuwa jambo zuri sana. Kwa hivyo, naomba taaluma hizi ziweze kutolewa katika maeneo mengi kwa kuweza kumtunza mtoto pamoja na mama mjamzito.

Mhe. Spika, la mwisho nije katika hospitali ya Mwembeladu. Mhe. Spika, nashukuru kwamba hospitali ile inatoa huduma nzuri lakini hivi sasa imekuwa na ufinyu wa nafasi hata pakuweka gari ukenda na mgonjwa inakuwa tabu. Mhe. Spika, ningelishauri pana nyumba zimegandana sana na hospitali ile tungejaribu kuwashauri wenyewe kama watakubali, basi serikali ikazinunua nyumba zile mbili tatu pale zikavunjwa wao wakatafuta maeneo mengine ya kuishi. Hii itawezesha ile hospitali kupata nafasi angalau mtu akenda na gari

pale iweze kukaa na watu wakaangalie wagonjwa wao kwa nafasi. Nadhani hili Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri atalifanyia kazi na likafanikiwa basi tutazidi kuitia hadhi hospitali yetu ya Mwembeladu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, nia ilikuwa nimuombe msaada Mhe. Waziri kwenye hospitali zangu mbili ambazo nimeshazitaja. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, *wallahi* leo nisingekuwa na hata la kusema isipokuwa kuna moja kubwa tu ambalo limenisimamisha nilizungumze. Mhe. Spika, suala hili tumeshalisema mara nyingi na hata mimi binafsi nimeshalisemea sana, lakini naona bado Mhe. Waziri analifumbia macho au ana uzito nalo kiasi fulani. Mhe. Spika, ni suala la operesheni wa uzazi.

Mhe. Spika, jana nilipopewa hichi kitabu nikataka nitazame kwani ni kiasi gani hasa ambacho Mhe. Waziri anakikusanya kwa mwaka kwa ajili ya hii operesheni ambayo serikali au wizara hawawezi kuubeba mzigo huu.

Kati ya haya Mhe. Spika, kuna mambo mengi yanayozalika ndani yake. Wenzangu wliotangulia kuzungumza wana dhana ambazo watu huko nje wanazizungumza, moja ni ule wingi wa operesheni hizi ambazo hivi sasa zinafanyika tofauti na miaka ya zamani. Watu wanalalamika wanasema kwamba ukiugua nusu saa tu basi kisu tayari. Kwa hivyo, tukasema huku tunakokwenda siko tumshauri basi mwenzetu Mhe. Waziri. Nikatazama katika jadweli ile ambayo ametuletea ya hawa wajawazito ambao wanalazwa na kufanyiwa operesheni kiambatanisho cha 5.3. Nikaona wajawazito ambao wamelazwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ni 7,445, waliojifungua kawaida ni 4,933, upasuaji ni 1,091.

Kwa hivyo, nikajumlisha nikaona bado kwa hesabu hii ya elfu nne na elfu moja haifikii hii elfu saba ambayo katueleza hapa waliolazwa. Nikajiuliza hawa wako wapi, mbona hawaonekani, au ndio haya wanayozungumza watu kama ni asilimia 50 hivi sasa ya wanaopelekwa kule kuzaa wanajifungua kwa operesheni. Kama ni hivyo nikasema ni sababu zipi ambao wameziona wao kama madaktari kitaalam zinazosababisha operesheni hizi kuwa nyingi hivi.

Lakini pia nikaifanya hii hesabu ya 1,091 mara 40 ya wanaotozwa wagonjwa wanaolazwa pale. Nikaona Mhe. Spika, ni milioni 43,640. Nikasema basi

milioni 43,640 hizi kwa nini wizara au serikali isichukue mzigo huu, ili haya matatizo ambayo yanazungumzwa na hizi dhana ambazo zipo zikaondoka.

Lakini pia Mhe. Spika, katika kukipitia hichi kitabu nikaona Mhe. Waziri katueleza kama kinamama wajawazito ambao wanapelekwa katika hospitali mwaka huu tu ni 6,195 wameonekana kwamba wana upungufu wa damu. Mhe. Spika, nikasema hivi Mhe. Waziri alitaka kigezo gani ili aone kama watu wetu ni kweli hawana uwezo wa kulipia hizi pesa. Kwa sababu unapokosa damu moja kwa moja unakwenda kwenye lishe, lishe haipatikani ikiwa watu wetu hawana uwezo. Sasa iwapo mtu hawezi kujikimu katika hali ile ya ujauzito akahakikisha kwamba *diet* yake anai-*balance* na anakuwa na damu ya kutosha, kweli ataweza kumudu jambo la dharura ambalo linakuja kama wingu la mvua usilolitarajia.

Kwa sababu kuna maradhi mengine ambayo wizara wenyewe wanayachukulia kifua, ni operesheni nyengine. Mhe. Spika, mwaka jana nilisema hapa kwa nini huu operesheni wa mabusha ambalo mtu anakaa nalo miaka mitatu anakwenda nalo akirudi nalo, nenda mbele, nenda nyuma, ikawa Mhe. Waziri anasamehe watu wafanyiwe bure. Lakini hili la uzazi Mhe. Spika, ikawa Mhe. Waziri mpaka leo kalishikilia lazima utoe shilingi 40,000. Sasa mimi hapa ndio ninapojiuliza hapa ni mradi au ni kitu gani. Maana yake unapokosa kumfikiria mama mjamzito, sote ni waislam tunaambiwa kazi zote Mwenyezi Mungu humtuma malaika nendeni mkafanye, lakini inapofikia sehemu hii tunaambiwa anateremka mwenyewe. Sasa tuuone ule uzito wa hali kama hii.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kama wenzake hili suala la shilingi 40,000 liondoke. Maana yake nilikaa nikafikiria ile wanayotakiwa wachangie katika mfuko mkuu labda na hii wanapeleka. Mhe. Spika, Mhe. Waziri aliahidi kuchangia shilingi 19,000,000 katika mfuko mkuu wa serikali, lakini kutazama kiambatanisho nikaona hakimo, nikaona kwa kweli hii pesa haiendi katika mfuko mkuu wa serikali, itakuwa labda inakwenda katika hizo hizo operesheni wenyewe. Lakini kweli milioni 43 zisababishe zogo lote hili. Kwa nini tusifikirie wananchi wetu.

Mhe. Spika, mwaka jana Mhe. Waziri alitwambia kama kuna mama huruma. Jamani inaonekana huyu mama huruma hayupo, kama ana huruma basi ni kwa watu wengine ambao hawastahiki labda kuwa na huruma, labda ni watu wa familia tu ndio wanaopewa hii huruma. Tunasema haya Mhe. Spika, kwa kuyajua kwa sababu asubuhi na jioni tuko huko hospitali.

Mhe. Spika, ingekuwa iko hiyo huruma basi kama wawakilishi wako tungetakiwa labda ile pesa ya gari tu, kuna mzazi umpelekee gari, lakini tusingetakiwa hii pesa ya operesheni uende ukailipe. Sasa kwa nini ije kwako

wakati kuna mama huruma kule. Kwa nini mtu ajidhalilishe aje kwako, hata akija kwako kama mwakilishi wake akatoka kwenye familia ni kwa sababu hana hii pesa. Sasa huyu mama wa huruma aliyepo anamdanganya Mhe. Waziri hasaidii watu.

Kwa hivyo, ili kuliondoa hili moja kwa moja lisilete utata tuiondoe hii isiwe ni mradi wa watu, Mhe. Waziri watendaji wake ikawa wanampeleka pahala sipo. Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Waziri atusikilize kama wenzake.

Mhe. Spika, jengine niliona katika kiambatanisho 3.1 kuna ugawaji wa vyandarua, lakini niliona kuna wilaya nne tu ambazo zimepewa hivi vyandarua katika mwaka huu, ni Kusini, Kaskazini 'A', Wete na Mjini. Sasa Mhe. Spika, nilitaka Mhe. Waziri anifahamishe kama ni utaratibu gani ambao walitumia katika kutoa kipaumbele kwa hizi wilaya na akaacha wilaya nyengine.

Mhe. Spika, nizungumzie Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Mhe. Spika, nimetazama mle nikaona kama kuna *sample* 591 za chakula ambazo zilifanyiwa utafiti, kati ya hizo 453 zilipasi na 38 zilifeli. Hivyo hivyo kwenye madawa tukaona kama 42,412 zilipasi na 7 zilifeli.

Mhe. Spika, katika hili nilitaka wenzetu kwanza wanifahamishe kuwa hizi bidhaa zinapoingia ndani ya nchi yetu za chakula, dawa au hivi vipodozi. Huu uchunguzi huwa unafanywa pale mwanzo tu vinapoingia hivi vitu na vikagundulikana kama hivi vinafaa au hivi havifai kwa matumizi. Au huu uchunguzi unakuwa endelevu. Pindi pale vinapoonekana kama hivi ambavyo Mhe. Waziri katueleza katika kitabu chake kwamba *sample* hizi ambazo zimeletwa hazifai kwa matumizi. Sijui ni njia gani ambayo wanatumia kuhakikisha kama vitu hivi havitumiki.

Mhe. Spika, hivi sasa kumekuwa na matatizo makubwa ya kensa na kisukari. Kwa kweli Mhe. Spika, hivi sasa kensa inaua au inatisha kuliko hata huo ukimwi. Ule ukimwi watu wanauchukulia kama ni maradhi ya aibu ndio shtuo lake. Lakini kwa kweli kensa hivi sasa Mhe. Spika, inavyoua ukisikia utashtuka. Wengi wanasema kwamba inatokana na hivi vyakula tunavyokula vilivyokuwa havina uhakika na vilivyokuwa vimepita muda.

Lakini Mhe. Spika, ukiachia katika chakula hivi vipodozi vimo madukani. Mwenzangu asubuhi kasema vile vya Kichina vya kuongezea viungo, lakini kuna vyengine mpaka hivi vya kubadilisha rangi, viko na vinatumiwa na vinadhuru sana wananchi wetu.

Sasa isije ikawa hii kama nguvu ya povu tu ni pale hii bidhaa ikiingia, lakini baadae ikawa hawapitii kwenye maduka. Au ikawa wanapitia kwenye maduka

lakini vile ambavyo vinachukuliwa kutoka katika maduka baadae vinarudi tena kwenye maduka, au baadae ndio hivi ambavyo tunaviona mikononi. Kwa sababu kuna bidhaa ambazo unaziona mikononi vijana wanauza ukizitazama kwa makini unaona kama bidhaa hizi zimepitwa na muda. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili alifuatilie. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi nikachangia kidogo kwenye hotuba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Lakini kwa sababu ya hali yangu itabidi mnistahamilie nina kikohozi kidogo.

Mhe. Spika, nianze kwanza kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya wakatuletea hapa wenzao, ili na sisi tuje tuwachangie nini ambacho kinataka tukiboreshe, au nini waongezee ili mambo yaende vizuri.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni wizara muhimu sana inayoangalia hali zetu sisi sote hapa katika nchi. Yaani wizara hii kama haikufanya kazi zake ipasavyo basi sote tutakuwa hatuwezi kufanya kazi. Huwezi kwenda kazini kama unaumwa, kuzaa ndio hivyo tena tuna shida, watoto wakiumwa inakuwa shida. Kwa hivyo, hii ni wizara muhimu sana na kwa umuhimu wake na sisi inatubidi tuizungumzie na tuisaidie kuisemea, ili wenzetu hawa katika juhudi zao zote wanazozifanya na serikali isaidie waweze kufanya kazi zao kwa mafanikio.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri na Naibu wake wamejitahidi kurekebisha mambo mengi *Alhamdulillah* tunashukuru. Mhe. Spika, kuna mambo ambayo tunawashauri hapa Barazani na wanayachukulia hatua wanayafanyia kazi. Kwa hivyo, sisi hatutavunjika moyo kuendelea kuwashauri.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana lakini mara nyingi nitashauri tu. Kwanza naanza na Hospitali ya Mnazi Mmoja wodi ya wazazi. Mhe. Spika, wodi ya wazazi ni ndogo haitoshi. Wodi za wazazi za serikali kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ni za hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu. Pia Hospitali ya wazazi ya Mwembeladu ni ndogo haina nafasi. Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali pale katoa ushauri kasema serikali izungumze na watu jirani wauze nyumba zao tuweze kupanua lile jengo letu. Lakini mtu ana hiari yake kukubali kutoa nyumba yake na hasa sasa hivi ilivyokuwa nyumba ni mali na ataona akiondoka pale sijui atakwenda wapi.

Mhe. Spika, Hospitali ya wazazi Mwembeladu ndio hospitali saidizi kwa mjini. Mhe. Spika, mji umekua sana, zamani tulikuwa tukishafika Mikunguni tumemaliza mjini, lakini sasa hivi mji umekua umeshafika mpaka Fuoni na zaidi mbele. Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali alisema hapa kwamba na yeye tayari ana mji wa Mfenesini. Sasa mji umekua na kama mji umekua wanawake tuko wengi na tunazaa hususan wakati huu wa baridi mambo yanakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazazi ni wengi kwa sababu wanawake tuko wengi na waume zetu ni wachache wanaotaka uzazi wa mpango, bado wengi hawajaukubali uzazi wa mpango. Ukimwambia anasema Mwenyezi Mungu mwenyewe anajua namna gani kapanga uzae watoto wangapi, au Mwenyezi Mungu hafundishwi. Ni kweli Mwenyezi Mungu hafundishwi na ametuacha tuzae, lakini tukizaa sana mambo yanakuwa sio mazuri mfano ndio hiyo hospitali.

Mhe. Spika, unakuja wodi ya wazazi sijui kwa sasa hivi maana mimi nimeacha kuzaa muda mrefu. Lakini zamani tulikuwa tukikutana mle ndani mwisho inabidi tusaidiane tuwe wakunga hata sisi wagonjwa kwa sababu wafanyakazi walikuwa kidogo hawatoshi. Wakati mwengine wanaoingia zamu za usiku wanapata tabu sana kwa sababu wanakuwa kidogo mpaka *orderly* anakwenda kusaidia kuzalisha.

Mhe. Spika, si vibaya, ni vizuri, lakini sasa mimi ningeliomba kitu kimoja kwa Mhe. Waziri wale ma-*orderly* tujitahidi tuwachukue angalau waliofika darasa la 8 mpaka kidato cha 3, ili na wao tuwape taaluma ya kuweza kusaidia kazi kubwa ile iliyokuwemo mle. Kwa sababu wakiwa wao wepesi wa kuwasaidia wale ikiwa usiku wazazi wamekuwa wengi wanaweza kusaidia. Lakini ikiwa ma-*orderly* hawajui kuzalisha ndio kwanza wameanza kazi inakuwa tabu kwa yule *nurse* aliyekuwepo pale.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awape mafunzo hawa ma-orderly wetu sasa hivi wa wodi ya wazazi ili na wao waweze kusaidia hii kazi nzito inayofanywa pale na kinamama na wanayofanya hao wafanyakazi wa wodi ile.

Lakini Mhe. Spika, kuna kitu chengine Mhe. Zahra Ali Hamad kakisema na mimi naomba nikiseme kwa sababu mimi ni mama na ninahusika. Mhe. Spika, wenye uwezo ni wachache sana kuliko wasio na uwezo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kama dada yake hii shilingi 40,000 ikiwa hawezi kuiondosha kabisa basi ipunguzwe iwekwe kwenye hali ya chini kwa sababu sio watu wote wenye uwezo. Mhe. Spika, kama nilivyosema mji umekua umeshafika mbali na wanawake tuko wengi na tunazaa sana. Siku hizi ndio hayo yanayosemwa mtu dakika moja mbili ukifika pale hospitali huwahi kufanya *labour* kwa muda mrefu unaambiwa huyu anataka kisu.

Mhe. Spika, zamani sisi tulipokuwa tunakwenda wanasema wenyewe madaktari kwamba tunampunguzia kazi mama asichoke kwa hivyo anafanyiwa operesheni. Mhe. Spika, zamani ilikuwa mtu anaanza kuugua nyumbani kwake mpaka hospitali anakwenda pale anamaliza kazi. Lakini pengine mwanagenzi kenda pale hajui nini uchungu, anaona mimi uchungu nikiumwa nywi tayari nazaa, kumbe hajui kuna kazi kubwa pale ufanye halafu ndio Mwenyezi Mungu akupe nafasi ya kuweza kuzaa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atusaidie hao wanaofanyiwa operesheni wale ambao pia wanaonekana hali zao ngumu bila ya kiasi tusiwatoze jamani. Mhe. Spika, nilisema hapa Siku ya Mtoto na Mama kwamba kazi ya kuzaa ni ngumu, tena kazi kubwa sana, Mwenyezi Mungu kaufanya wakati ule milango ya pepo iwazi kwa mama kwa ajili ya uzazi. Kwa hivyo, tusiwape kinamama jukumu jengine la kufikiria mimi nimeshaandikiwa operesheni maskini baba katoka Kiboje huko ameshalima muhogo wake, pesa akiuza muhogo haitoshi hata kula yeye mwenyewe anakwenda pale anaambiwa lete shilingi 40,000 na kama huna hutoki. Maana anafanyiwa operesheni lakini anafungwa kama yuko jela, si halali. Naomba tuwasaidie wananchi wetu waweze kufanikisha.

Mhe. Spika, nikitoka hapa nakwenda kwenye *fast track*. Mhe. Spika, tulimshauri Mhe. Waziri kwamba atuwekee pahala ambapo mtu anaweza akalipa akapata matibabu na huduma nzuri. Lakini mimi ningeomba bado *fast track* inataka uboreshaji. Mhe. Spika, mimi nimekaa pale muda wa miezi mitatu, unajua nilikuwa na mgonjwa naingia nikitoka naona zile huduma zinavyokwenda. Sitaki niseme nini na nini, lakini wakuu wa mawodi yale wanajua nini kinakwenda. Mhe. Spika, *fast track* watu wanalipa kwa imani, maana yake mtu hajali anaona mimi nitoe nipate huduma.

Mhe. Spika, naomba basi *fast track* iboreshwe kiusafi, iboreshwe kichakula, iboreshwe matibabu. Inahitaji kuboreshwa ili watu wavutike zaidi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itapata mchango zaidi kila watu wakivutika kuja kule kuwapisha waliokuwa hawana pesa wakapata nafasi kwenye wodi nyengine.

Mhe. Spika, nizungumzie kidogo kuhusu madawa ya kulevya na ukimwi. Mhe. Spika, ukimwi badala ya kupungua unazidi na tunauzidisha sisi wenyewe kwa sababu tunaambukizana. Mhe. Spika, tunashukuru kuna dawa za kurefusha maisha, mtu anakula dawa za kurefusha maisha halafu anajificha yeye kama ana ugonjwa wa ukimwi, anampa mwenziwe tunaambukizana. Mhe. Spika, sasa kwa hali hii utakuwa haumaliziki, sisi tunawasaidia wapate warefushe maisha waishi, lakini utamkuta mtu yuko *healthy* ameshakula dawa za kuboresha maisha anaambukiza watu. Tuwape basi na mafunzo kwamba wewe unasaidiwa sio ukawaathiri na wenzio ukawape ukimwi kwa makusudi.

Lakini Mhe. Spika, kuna wagonjwa wa madawa ya kulevya wanapata ukimwi bila ya kujijua kwa sababu ya kutumia sindano au vitu mbali mbali wanavyotumia kwa ushirika, hususan ni sindano. Wao wanaona mimi napiga sindano napata starehe kumbe mwenziwe ana ukimwi hajui anamuambukiza na yeye. Kwa hivyo, tuwaombe wahusika wazidi kuwapa watoto wetu taaluma maana ndio wameshaathirika hatuna vya kuwafanya ili wasije wakaambukizana.

Lakini Mhe. Spika, nimeona hapa kuna upatikanaji wa mtaalam wa michoro ya nyumba ya kuwahifadhia waliokula madawa ya kulevya pamoja na wagonjwa wa ukimwi. Hapa *Alhamdulillah* mwaka 2009/2010 hiyo michoro ndio ameshapatikana mtaalam, tujihimizeni basi tupate nafasi pajengwe haraka haraka ili watoto wetu wajulikane wanawekwa wapi. Kwa sababu sasa hivi watu wanapelekwa *Mental Hospital* kukaa.

Mhe. Spika, mtumiaji wa madawa ya kulevya ni sawa sawa na mwendawazimu *(half mental).* Sasa Mhe. Spika, ikiwa unakwenda kumpeleka anakuwa mwendawazimu, wakenda kule bila shaka wanakuwa taabani hawana nguvu. Mhe. Spika, mwendawazimu aliyekuwa kashiba hashikiki anaweza akamfunda yule akamuumiza vibaya vibaya. Kwa hivyo, tujitahidi haraka haraka kupata hichi kituo ili tuwatoe huku *Mental Hospital.* Haidhuru labda mnawaweka mbali sijui lakini iwe hivyo.

Mhe. Spika, nashukuru leo nilikuwa nasikiliza taarifa ya habari kwa mara yangu ya mwanzo nimesikia kwamba kuna mtu aliyeleta madawa ya kulevya ameshtakiwa na amehukumiwa. Lakini hukumu aliyopewa ni ndogo sana kwa muuzaji au mletaji wa madawa ya kulevya. Amehukumiwa nafikiri miaka 20 na miaka 10 *is nothing,* kwa sababu ana pesa, kama hana pesa yeye basi ana pesa huyo lodi wake aliyempa yeye alete hapa atatoka tu huyo, zitalipwa pesa hizo kisha anatoka. Kwa hivyo, ile ni adhabu ndogo kuliko adhabu wanayopata watoto wetu.

Mhe. Spika, tunapiga kelele sana humu na hatupigi kelele tu kwa sababu tunapiga kelele. Tunapiga kelele kwa sababu baada ya miaka kupita, sisi wengine tutakuwa tumeshaondoka na wenda wazimu watakuwa wengi. Wagonjwa wa madawa ya kulevya mwisho wake wanakuwa ni wendawazimu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nishauri tena kuhusu wafanyabiashara. Wafanyabiashara jamani muwaangalie sana, muwe waangalifu na *health inspectors* wajitahidi wanapokwenda kwenye vibanda vya chips na mama ntilie wale wanaopika vyakula, basi waangalie na usafi wa vyakula. Kwa sababu kwenye mabanda mengine ya chips ukenda utaona uchafu kula na kwa sababu

hawapitiwi kila mara na kama wanapitiwa kila mara, wanaokwenda kuwapitia labda miwani yao inakuwa ni mizito sana hawaoni.

Kwa hivyo, tujitahidi Mhe. Spika, tuzungumze na wafanyakazi wetu, tunawalipa mishahara kwa ajili ya kufanya kitu, wawa-*fever* ikiwa yeye hakula pale basi atakula aliyekuwa wake au ni mwananchi mwenziwe ana muumiza kwa maradhi. Maradhi ya kuambukiza yapo tele, kwa hivyo tujitahidi kwa hilo.

Jengine Mhe. Spika, niseme kuhusu malaria. Mhe. Spika, malaria yapo hayajaondoka yapo tena yanarudi kwa kasi kubwa sana. Tusiache vipimo kupima vya malaria, mtu kenda hospitali apimwe malaria, usimpe *panadol* ukamwambia nenda zako au tumia hii au hii mpime na uhakikishe kwamba ana malaria au hana. Lakini malaria yapo na ikiwa hatuwapimi wagonjwa wetu malaria basi baadae ni kupata vifo.

Mhe. Spika, upigaji wa dawa wa mbu wa malaria unapigwa lakini hautoshelezi. Tunapigiwa ndani ya majumba lakini nje ya majumba kuna kuwa na madimbwi, kuna kuwa na mkusanyiko wa taka na mambo chungu nzima. Kama maeneo ya kwetu kule hata magari ya taka hakuna. Wewe mwenyewe utajijua tu utapata wapi pa kuweza kufanya taka. Lakini tujitahidi hizi dawa za kupiga zizidishwe ili hawa mbu wasije juu kwa kasi wakatumaliza.

Mhe. Spika, nizungumze habari ya upimaji wa afya. Wafanyakazi nafikiri wakiingia kazini wanapimwa afya, lakini baada ya hapo hawapimwi tena. Nauliza tu Mhe. Waziri uje uniambie, baada ya hapo huwa wanaendelezwa kupimwa afya kila baada ya muda fulani au ile ile tu ukianza kwenda kazini ndio unapimwa kwa sababu unatakiwa ukiwa unaanza kwenda kazini au kuajiriwa usiingie mgonjwa. Lakini pia ukiwemo ndani ya kazi unaweza kupata maradhi ya kila namna je huwa wanaendelea kupimwa.

Vile vile watoto wa skuli Mhe. Spika. Watoto hawa ni muhimu sana kufanyiwa vipimo. Mhe. Waziri ungeweka kitengo maalum cha watoto wa skuli, madaktari kupita maskuli kama tulivyokuwa tukifanyiwa sisi ili kujua kuna maambukizo ya kitu gani hapa, pengine pana maambukizo kama hayo ya vichocho kwetu kule nasikia Kwa Diki kuna makonokono mengi Ndagaa kule. Sasa ikiwa madaktari wanakwenda maskuli kupima na sio kama lazima atoke daktari anayekuweko kwenye wodi. Ni kwamba kiwepo kitengo maalum cha kuzungukia watoto na itasaidia pia kwa serikali kupunguza manunuaji ya madawa. Kwa sababu mtoto ukishamjua mapema kama ni mgonjwa unaanza kumtibu wakati ule kabla hajafika kuzidiwa na kwenda hospitali. Kwa hivyo, itapunguza msongamano wa hospitali, itapunguza manunuzi ya madawa.

Kwa hivyo, jitahidini hata kama hatutoweza kwa kila mwaka, lakini angalau kila baada ya miaka miwili wawe wanakwenda madaktari kuwapima watoto maskulini. Ni muhimu tena sana kwa afya za watoto wetu na mtatusaidia sana sisi kina mama kuwalea watoto vizuri na kupata makuzi mema.

Nafikiri Mhe. Spika mimi niseme ahsate. Nashukuru nimepata japo kidogo kutoa dukuduku langu.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii leo kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, kabla ya yote nimshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote wa wizara hii kwa juhudi yao kubwa ambayo wanachukua, katika kutekeleza majukumu yao kwa kuwatetea wagonjwa na wananchi pamoja na wananchi mbali mbali wanaofika katika vituo vyao vya afya.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 11.2.4.3 kitengo cha mafunzo pamoja na wafanyakazi kutoka katika timu za afya za wilaya na kupeleka wafanyakazi 41 walipata mafunzo mbali mbali ya afya. Kwenye suala hili Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa aliyoichukua kuwapeleka wafanyakazi hawa wasiopungua 41 kupata mafunzo ya afya kiwa kushirikiana na shirika la afya duniani. Kwa hivyo nampongeza sana kwa mafanikio hayo.

Mhe. Spika, isipokuwa kubwa tu ambalo nalisisitiza ni kuwa hawa wafanyakazi baada ya kupata mafunzo hayo basi ni vyema wakawa wanagaiwa zaidi vijijini angalau robo tatu wawe wanapelekwa vijijini. Kwa sababu kama tunavyojua baadhi ya vijiji vyetu vingi huko nyuma ilikuwa mara nyingi matibabu makubwa ilikuwa wanatumia tiba za asili. Kwa hivyo, kwa kuwa sasa hivi tumeshakuwa na tiba za kileo za kisayansi, kwa hivyo tulenge sana vijijini ile wale waliokuwa wanatumia tiba zile za asili basi waanze kubadilika na waweze kutumia tiba hizi za kileo.

Sisemi kuwa tiba za asili hazisaidii, zinasaidia vya kutosha kwa baadhi ya maradhi mengine. Lakini ni vyema hawa wafanyakazi wetu tukawa tunawalenga sana huko vijijini, ili kuweza kusaidia. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri katika wafanyakazi hao ambao wamepata taaluma hizi wakawapeleka wengi katika vijiji vyetu. Kama inavyoeleweka kuwa katika vijiji vingi vina zahanati mbali mbali za kusaidia matibabu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 30.3.4 katika kudhibiti maradhi ya kifua kikuu na ukoma, kinawajibu wa kuchunguza, kutibu na kufuatilia wagonjwa. Mhe. Spika, nashukuru watendaji wa afya kwa kuweka kitengo hiki. Lakini tatizo lililokuwepo, hapa Unguja kipo kitengo hiki, lakini utakuta watu wanaosumbuliwa na matatizo ya maradhi kama ya kifua na TB huwa wanapata

matatizo sana, wakipeleka vielelezo vyao wa kuchunguzwa kama makohozi au vitu vyengine huwa vinachukua muda mrefu sana kupatiwa majibu, huweza kuchukua miezi sita, mwaka mgonjwa bado yuko kitandani hayajapatikana majibu, ukiulizwa unaambiwa yamesafirishwa.

Kwa hivyo, mimi ningeomba kama kitengo hiki nchi jirani au kama kiko Pemba, basi na hapa kingekuwepo, kwa sababu kuna wagonjwe wengi wanaokutana kwa kesi kama hizi. Lakini ukenda kupeleka vielelezo vyako vya kuchunguzwa basi unaambiwa ukae miezi sita, mitatu au mwaka bado hujapata jibu. Kwa hivyo, huu unakuwa ni usumbufu ningemuomba Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, akafanya yake yote kama vifaa vinavyopimia masuala haya viko Pemba basi hapa Unguja aviweke, ili kupunguza usumbufu kwa wagonjwa wenye matatizo kama haya.

Kwa kweli wengi wao wakati mwengine huwa wanavunjika moyo, kwa kuwa majibu yanachelewa muda mrefu kuwa hawajayapati. Kitengo hiki Mhe. Waziri angekiangalia sana kama kuna upungufu wa nyenzo basi akakipatia nyenzo, ili na wagonjwa wetu wakapata matumaini mazuri ya kupata matibabu.

Mhe. Spika, kama mgonywa yule kachunguzwa lakini matibabu yake hayawezekani kwa hospitali basi wapewe ushauri, kwamba kwa hali uliyokuwanayo basi ujisaidie na dawa za kienyeji. Kuliko leo kila akienda anaambiwa majibu hayajapatikana, huku anazidi kuteseka. Kwa hivyo, ningeomba kitengo hicho akakiangalia sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, suala la kufuatilia wagonjwa wenye matatizo hayo kwa kuwa mafaili wanakuwanayo, basi ningemuomba Mhe. Waziri akatuma wataalamu wake zaidi ili kufuatilia na kupata kuhakikisha wagonjwa wetu nao waliokuwa majumbani wanafanikiwa kutibiwa maradhi hayo wakati dawa zinapatikana.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 42, kifungu cha 4.40 kuhusu afya ya wafanyakazi katika kufanya ukaguzi wa mazingira ya kazi na uchunguzi wa afya za wafanyakazi. Mhe. Spika, kwa kweli kuna haja sasa hivi kitengo hiki kikazidisha mikakati zaidi katika kuchunguza afya za wafanyakazi. Pia katika sekta mbali mbali, zikiwemo za mahoteli, ma-*bakery*. Kwa kweli humu muna wafanyakazi wengi wao wanafanyakazi lakini afya zao zinakuwa sio nzuri, wana maradhi ya kuambukiza na maradhi mbali mbali ambayo hayaruhusu kufanyakazi hizo katika vitengo hivyo kama vya mahoteli na ma-*bakery*.

Mhe. Spika, kwenye ma-*bakery* yetu hapa Unguja ukiingia tu mazingira yao, wengi wao yanakuwa hayaridhishi. Hiyo mikate ambayo tunapikiwa mingi ndio ambayo tunaitumia katika visiwa vyetu hivi, lakini ukiwachunguza wafanyakazi wake kwa kweli mazingira yao yanatisha. Kwa hivyo, ningeomba

kitengo hiki kikafanya ukaguzi wake na wasichukuwe muda mrefu, angalau katika mwaka wakawa wanatembelea vitengo hivi kwa kuwapa taaluma na kuwapima afya zao wale wafanyakazi wa kazi hizi, ili kujiepusha na maradhi mbali mbali ya mripuko au ya kuambukiza kutokana na matumiziya vyakula hivi ambavyo vinapikwa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, kuna watu humo katika sehemu hizo wanapika majikoni wanatoka majasho, hawana hata sare. Halafu Mhe. Spika, utakuta majasho yanaingi mule mule kwenye vyakula. Kwa hivyo, ningeomba wataalamu hawa wapite humo kwa kutoa taaluma ili kunusuru afya za watu wetu.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 43, kifungu cha 5.0 Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imeundwa na hospitali ya wagonjwa wa akili, wazazi wa Mwembeladu na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa juhudi zao kubwa wanazochukua katika ukarabati na ujenzi wa hospitali hizi.

Mhe. Spika, kwa kweli miaka ya nyuma tunakotoka na sasa hivi kulingana na hali ya majengo ya hospitali zetu, basi kwa mtu yeyote akiona atajua juhudi za Mhe. Waziri na watendaji wake wanavyojitahidi. Ukija kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja imebadilika vya kutosha, imejengwa majengo ya aina mbali mbali na taasisi mbali mbali ziko pale.

Ukija kwenye Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu, pia juhudi zake tunaziona zinavyoendelea. Mpaka sasa hivi wamefikiwa kujengewa ukuta ambao ulikuwa ni kero kwa kila siku, kuwa baadhi ya wagonjwa huwa wanaruka ukuta na kukimbia katika jengo lile. Leo *Alhamdulillah*, jengo limejengwa vizuri na limehifadhiwa kuta vizuri kwa kuwahifadhi wagonjwa hao.

Mhe. Spika, ukija kwenye Hospitali ya Mwembeladu, nayo halikadhalika wamejitahidi vya kutosha kuliwekea mazingira mazuri ya kileo na likapendeza jengo lile. Lakini ombi ninaloomba tu Mhe. Waziri katika vitengo vya hospitali hizi angewapatia angalau gari la wagonjwa moja moja, ili pindipo wanapotokezea wagonywa kutoka katika hospitali hizo na kuletwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, basi zikawa zinapatikana gari. Isiwe usumbufu wa kutafuta gari, kuwa mwenye mgonjwa tena ahangaike kutafuta gari la kumuondoa mgojwa pale na kumpeleka katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, ningeomba afanye mbinu zake zote, lakini hospitali hizi ya wagonjwa wa akili na hospitali ya Mwembeladu uwepo usafiri wa kuwahudumia wagonjwa ambao wanatoka hospitali zile wafike katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja pindipo ikihitajika hivyo.

Mhe. Spika, mimi nawapongeza watu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa juhudi yao kubwa wanayochukua ya kuimarisha majengo yetu hayo ya hospitali hizi kama nilivyozitaja.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 43, kifungu cha 5.1.1 kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja inatoa huduma na matibabu kwa wagonjwa wa nje na ndani pamoja na huduma za uchunguzi wa *X-Ray, Ultrasound* na *CT Scan.* Kwa kweli vifaa hivi wanajitahidi sana kuvitumia kwa wagonjwa wetu, lakini tatizo lililokuwepo ni kuwa *CT Scan* haitumiki ipasavyo. Kuna baadhi ya wananchi wanalalamika kuwa wakienda na wagonjwa wao basi hawashughulikiwi inavyopasa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe.Waziri katika kitengo hiki wagonjwa wanaohitajika kutumia kitengo hiki, basi na wao wapewe fursa ya kutumia. Madhali watakuwa na michango ya kuchangia basi na wao wapewe fursa ya kutumia. Kwa hivyo, kuhusu hili nitamuomba Mhe. Waziri watendaji wake waangalie sana ili na wagonjwa wetu wapate huduma ya kutumia kifaa hiki.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 56, kifungu cha 6.11.0 kuhusu huduma za wazazi.

Mhe. Spika: Kwa dakika mbili.

Mhe. Ali Denge Makame: Kama walivyozungumza wenzangu, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri akaangalia sana, kama kuna haja ya kuondoa huu mchango wa kuwafanyia operesheni wazazi, basi na mimi naunga mkono bora ungeondoshwa. Kama ilivyokuwa tunafanikisha masuala mengine ya kuwasamehe kodi watu mbali mbali wafanyabiashara, basi na wazazi hawa wafikiriwe kusamehewa.

Mhe. Spika, kwa kumalia tu nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa aliyochukua ya kutia dawa za malaria majumbani na kupunguza hili tatizo la malaria. Kwa kweli sasa hivi tatizo hili limepungua vya kutosha. Namuunga mkono kwa juhudi hiyo.

Mhe. Spika, kwa hayo tu namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, naiunga mkono hotuba yake hii na tunaipitisha kwa asilimia mia kwa mia bila ya matatizo yoyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, namshukuru Allah kwa kukujaalia wewe na mimi jioni hii nikapata fursa ya kuchangia mawili matatu katika wizara hii mama, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, nimeiita wizara mama kwa sababu hii ndio inayotizama hali zetu za kiafya na ndio tunayoitegemea. Wenye uwezo wanakwenda India na kwengineko. Lakini tulio wengi tunaishia katika hospitali zetu hizi za Mnazi Mmoja, Chake Chake, Mkoani, Wete, Micheweni, Kivunge na kwengineko. Wafanyakazi kusema kweli wanajitahidi kufanyakazi zao, ingawa penye wazuri na wabaya wapo, lakini wazuri ni wengi.

Mhe. Spika, pamoja na yote mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri awatizame wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mishahara midogo. *Scheme of Service* yao ifanyiwe haraka kutengenezwa na ikitengenezwa itengenezwe kweli kweli kwa wenye elimu, wenye uzoefu watizamwe, waliofanya kazi miaka mingi na walioingia jana. Mhe. Spika, hii *Scheme of Service* ya wafanyakazi ikifanywa vizuri, kama walivyosema wenzangu basi kidogo itapunguza kuwaondosha wataalamu.

Mhe. Spika, narudia tena kusema wataalamu wa Zanzibar ukitaka uwaone kama wengi hawapo hapa Zanzibar, basi panda boti ya siku ya Ijumaa jioni inayokuja Zanzibar, basi utawaona wote wamo humo. Wanakuja hapa Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wanaondoka na wengine wanaondoka Jumatatu asubuhi. Sasa hii ni kuona kwamba wataalamu wetu wengi wanaondoka, wakiwemo wataalamu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wengine hawaishii hapo Bara, wengine wanakwenda Kusini mwa Afrika huko Namibia huko, Botswana, Afrika ya Kusini kwenyewe na wengine wanakwenda nje zaidi. Kwa hivyo, hawa wote wamesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wamekuwa wataalamu wazuri na huko nje wanafanyakazi vizuri. Sisi tunasifiwa kuwa wanatoka Zanzibar, lakini tunapata hasara, kwa sababu wanaondoka na tumewasomesha sisi. Lakini wanaondoka sio kama wanapenda kuondoka, wanaondoka kwa sababu ya maslahi madogo. Kwa hivyo, hali hii itizamwe.

Mhe. Spika, tunajua kwamba sasa hivi Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii anajitahidi sana kuleta vifaa mbali mbali hapa Zanzibar ili tuendane na hospitali nyengine zilivyo. Lakini vifaa peke yake bila ya wafanyakazi kupata kitu mkononi wakapata uwezo wa kula vizuri, kuvaa vizuri na kuishi bila ya wasi wasi basi vifaa peke yake havitoshi. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kuu, mishahara ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itizamwe, *plan* ya mishahara yao ifanywe haraka haraka ili hili tatizo kidogo litupungukie.

Mhe. Spika, nakuja kwenye Hospitali ya Wete. Zamani Hospitali ya Wete ilikuwa ndio hospitali yetu kubwa kule Pemba, lakini sasa hivi hospitali kubwa ni Mkoani. Lakini hospitali ya Wete kwa Mkoa wa Kaskazini hata kwa Pemba yenyewe bado inabakia kwamba ni hospitali kubwa nayo vile vile. Lakini

hospitali yenyewe inahitaji marekebisho makubwa sana, ikiwa sio kuvunjwa kabisa yale majengo ya nyuma kule, sio hili kubwa la mbele, yale ya nyuma kwenye wodi ya wanawake, wodi ya wanaume, wodi ya wazazi na wodi ya watoto zote hizo hazifai tena na wala sio hospitali tena. Kwa kweli itafutiwe kila mbinu hospitali ya Wete ili ijengwe upya. Nyinyi wenyewe nendeni mkaikaguwe, kwa sababu imeshakuwa kongwe sana ile hospitali, hata ukiikarabati vipi haifai. Hasa kwa sababu iko karibu na bahari, hata ukiipaka rangi vipi haiwi ile hospitali imeshakuwa kongwe sana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tutafute wasamaria wema ikiwa kwa mikopo au ikiwa kwa chochote, lakini ile hospitali ya Wete ifanyiwe utaratibu kwa yale majengo ya nyuma yavunjwe hasa na fusi liondoshwe ijengwe hospitali mpya kabisa ya kisasa.

Jambo jengine Mhe. Spika, mimi nilipokuwa mdogo, nilikuwa nikimsikia bibi yangu akisema neno '*helt office'*, alikuwa haipati. Lakini alikuwa anasema *health office,* kule kulikokuwa kunapimwa maziwa na vitu vingine. Jamani haya maziwa tunayokunywa siku hizi yanapimiwa wapi, maana mimi sijui tena. Hapa Unguja sijui ndio ilikuwa afisi ya panya sijui afisi ya nani, nakumbuka maziwa yalikuwa yanapimwa. Siku hizi sisi tunakunywa tu maziwa bila kupima, sio Unguja wala Pemba yanapimiwa wapi haya maziwa na maziwa haya yanachukua viluwiluwi vingi vya maradhi.

Kwa hivyo, tunaomba huu upimaji wa maziwa na vitu vyengine. Maziwa haya yakunywa, nakusudia ya ng'ombe au ya mbuzi urudi katika hali yake basi hivi vitu vipimwe tusiachiwe tu kuvila ovyo.

Jengine Mhe. Spika, ninalotaka kusema ni kwamba napendekeza, najua hali ni ngumu lakini napendekeza kwamba wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hasa madaktari na wale wengineo, basi wapatiwe usafiri. Mfanyakazi akiwa hana usafiri hasa akiwa mkubwa kama daktari basi inakuwa haipendezi, wakati yuko kwenye zamu yake anakwenda kuchukuliwa na gari ya wagonjwa. Inakuwa kidogo haipendezi. Madamu daktari yuko *oncall* anajulikana keshatiliwa mafuta yake, ikitokea dharura anapigiwa siku anakwenda anafanyakazi yake kisha anaondoka. Lakini kama hana usafiri ni shida kidogo na haya ndio yanayowafanya wenzetu waondoke.

Jambo jengine Mhe. Spika, nimeona katika kitabu kwamba kunataka kujengwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili pale Hospitali ya Wete. Nilipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ahadi za Serikali, jambo hili tulilipigia kelele sana kwamba pale hapafai. Ripoti tuliitoa hapa hapa kwamba pale Wete palivyokaa lile jengo lake hapana tena nafasi nzuri, hapana tena nafasi kubwa, kwa hivyo hospitali hii ya wagonjwa wa akili isijengwe pale. Nyinyi mna viwanja vingi

kule Pemba mmeviwacha tu hamvitaki wenyewe, mmeviwacha sijui kwa makusudi au vipi, maana tumepiga kelele mpaka tumechoka.

Mhe. Spika, iliyokuwa hospitali ya wagonjwa wa wakoma zamani kule Makundeni, kuna eneo lenu kubwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, lile ni lenu lakini sijui hata kama mna hati miliki, sijui hata kama mnalifuatilia, sijui chochote naona tu lile eneo lipo lipo watu wanalima sasa hivi. Kila mmoja anasema hapa ni pangu. Sasa nyie mkija mkipataka mtapapata wapi na mmewaachia watu zamani wachukuwe. Sasa sisi zamani tulipendekeza kwamba kule kukajengwe kwa sababu lile eneo ni kubwa sana, kukajengwe basi hospitali ya wagonjwa wa akili kwa Pemba. Lakini tumeona kwamba pendekezo letu hili labda halikutiliwa maanani na matokeo yake hospitali ya wagonjwa wa akili inapenyezwa pale pale kwenye hospitali ya wagonjwa wazima. Je, hao wagonjwa wa akili wakija kukata kamba mule ndani na kuingia katika wodi ya wagonjwa wengine hali itakuwaje.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika ukurasa wa 100, kuna changamoto kuu ya mradi wa kuendeleza kuwepo kwa vidokezo vya hatari kwa kina mama wajawazito inaendelea hii. Lakini inaonekana kwamba wakina mama wajawazito hapa Zanzibar wanakabiliwa sana na upungufu wa damu kama ilivyoelezwa. Nadhani kule katika sehemu ya kupimiwa wajawazito na watoto wachanga bila shaka kunatolewa elimu ya afya kwa kiasi ninavyoelewa mimi. Kabla ya kazi ya kuanza kupima wajawazito na watoto wachanga kuanza basi inatolewa elimu kwanza, najua elimu hii inatolewa.

Mhe. Spika, sasa mimi ningeshauri kwamba watendakazi wa kitengo kile wanafanya, lakini wazidi kufanya hasa kwa wale wanaowapima wajawazito na watoto wachanga walioko katika vituo vya vijijini huko, basi wawaelimisha hawa kina mama kwa sababu hii ni hatari. Mwanamama akishafika mimba au ujauzito wa miezi minane anakwenda hospitali anaambiwa kuwa una damu 40 na keshokutwa anajifungua. Kwa kweli hii ni hatari. Kwa hivyo, mapema ingejulikana kwamba huyu ana upungufu wa damu atasaidiwa vipi, lakini na hawa wazazi waambiwe kuwa japo dagaa wawe wanakula sana, mboga ziko kwa wingi waelimishwe kula sana.

Vile vile jambo jengine Mhe. Spika, wanawake wajawazito tatizo jengine linalowafika ni lile pengine la kupata kifafa cha mimba. Tatizo hili mara nyengine linajulikana mapema kwamba huyu atapata kifafa cha mimba. Kwa hivyo, pia elimu itolewe, mtu akijiona vipi basi akimbizwe hospitali haraka. Kwa sababu kuna ukaidi fulani, hasa huko vijijini. Mtu ukishaanza kuumwa na ukishaambiwa wewe ukiona uchungu tu basi kimbilia hospitali, anashindwa wakati mwengine kukimbilia hospitali, anakuja hospitali pengine hali imeshakuwa ni ya hatari. Kwa hivyo, inabidi madaktari na manesi wapate kazi

ya ziada ya kumsaidia. Kwa hivyo, elimu zaidi itolewe ili tuweze kuwaokoa kina mama wasipoteze maisha yao.

Mhe. Spika, nakuja katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuhusu usafi wa hospitali. Jamani ile ni hospitali yetu ya rufaa. Mimi mzazi wangu alikuwa akifanya kazi hospitali ya Chake Chake. Kwa hivyo, kwa sababu mama yangu alikuwa anafanyakazi hospitali nilipokuwa mdogo zamani likuwa siondoki pale hospitali ya Chake Chake. Saa nyengine nikitila huko simuoni au sikuona chai nyumbani, basi mambo ya kitoto namfuata mpaka kazini. Lakini nikifika pale hospitali basi naisikia harufu ya hospitali inanukia, hainuki. Wewe mwenyewe ukipelekwa hospitali kama unaumwa, sisi tulivyokuwa wadogo unaanza kulia, maana unasikia harufu nyengine ya madawa. Mhe. Spika, kulikuwa ni kusafi, huoni mtu kutema mate ovyo, madude ya kutemea mate yamewekwa pale pembeni pamoja na dawa ni kusafi hasa kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha hivi karibuni nilikwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kule kwenye uchochoro wa madaktari wa Kichina. Niliyoyakuta, sitaki kuyasema, lakini nitayasema kinyesi karibu na mlango wa daktari kimeshakauka, watu wanakipita wakikipituka na mlango huu wa pili kuna wafanyakazi wamekaa kitako wale ambao wanahusika na kusafisha eneo lile pale. Sikustahamili Mhe. Waziri, nilikwenda moja kwa moja mpaka kwenye kile chumba cha pili. Nikawaambia mimi ni nani, nilijijulisha kwa cheo changu na nikawaambia hili nitakwenda kulisema, mnaacha kinyesi hapa mnakiona, mnakipita mkikipituka. Hawa madaktari mabigwa wa Kichina waliopo hapa ni wageni, wanatu-tathmini vipi sisi. Haa! Maana yake. Maana yake vipi, toka asubuhi hamkioni hiki kimeshakauka. Ndio akatokea msafishaji anayesafisha eneo lile, ndio akajakusafisha pale na kupangusa akazoa na kuweka usafi. Nikawaambia sasa nimekuja mimi basi, lakini akitokea mgeni mwengine au akitokea Rais hapa kwa ghafla kajakukagua au Waziri Kiongozi kwa ghafla kaja kukagua mtasema nini. Wakabaki kupwesa pwesa hawana la kusema.

Sasa tunasema tumeondosha unyapara wa kusimamia kazi, lakini si unyapara kwani hata nyumbani watoto hatuwasimamii kazi tukeshakuwapanga kazi zao.

Kwa mfano, weye fyagia hapa, yule kosha vyombo na baadaye unatoka kwenda kuangalia kama kweli kumefyagiwa au kumesafishwa, kwa sababu watoto unapowapangia na ukawaachia, basi kila mmoja hujitia chumbani kwenye kitanda au akatizama televisheni na kupuuza ile kazi uliyompangia. Lakini akijua kwamba mama atakuja kuangalia baadaye, basi ataifanya ile kazi.

Mhe. Spika, tusiogope kusimamia kazi hasa jengo kubwa kama lile la hospitali, ambalo linahitaji usafi na pale si pahala pa uchafu isipokuwa ni sehemu ya usafi tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika katika

hili pamoja na watendaji wake wakubwa kwenye Hospitali ya Mnazimmoja awaambie Hospitali ya Mnazimmoja waitizame sana kwa usafi, kwa sababu ndio hospitali yetu mpya.

Kuhusu suala la *Operation* shilingi 40,000/- napita tu na wala hatuitaki wenzangu wengi wameshasema kwamba tuondolewe hii. Chakula na Vipodozi Mhe. Spika kwa kweli vinatuua. Mwaka jana nilisema kwamba Darajani kuna vyakula vingi vinavyouzwa ambavyo tayari zimeshapita muda, yaani wale wanaouza kwenye vimeza au chini. Kwa kweli wanafuta zile tarehe kwa ufundi kabisa, halafu vyakula vinaendelea kuuzwa na wala sikuona hatua iliyochukuliwa na mambo yanaendelea.

Mhe. Spika, kuhusu sisi wanawake tunapokuwa wadogo tunakuwa vichinchiri, wembamba, wazuri, yaani tunapendeza. Lakini tukianza kuzaa mtoto wa kwanza wa pili, basi tunaanza kufumka na hasa matumbo. Kwa hivyo, tunaomba kule hospitali kwa sababu naamini yapo mazoezi ya kuondoa mambo haya. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, wale wanawake wajawazito waambiwe na wafundishwe hasa, baada ya kwisha kujifungua kiasi muda wa siku saba njoo hapa ufundishwe mazoezi ya kutoa matumbo, kwa sababu watoto wetu wanaharibika *shape* baada ya kuzaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndio maana baada ya miaka miwili au mitatu baba anakwenda kutafuta mke mwengine kwa sababu yule tayari ameshaharibika *shape*. Kwa hivyo, naomba kama hakuna kitengo hiki basi kitafutwe mbona wengine hawafanyi matumbo na tunafanya sisi tu. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nizungumzie kwenye bajeti mwaka jana 2009/2010 ilikuwa ni 10,810,300,000/-. Lakini mwaka huu 2010/2011 ni 10,638,000,000/- kwa kazi za kawaida na mishahara ni 1,020,000,000/-. Sasa mambo haya hivi Mhe. Spika, mwaka jana ilikuwa kubwa na mwaka huu ni ndogo, unatarajia tupate nini hapo.

Mhe. Spika, kila mgonjwa mmoja wa Zanzibar anatibiwa kwa shilingi 5,000/- mwaka jana, mwaka huu anatwambia vipi na bajeti ameiteremsha ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi amedharurika. Kwa hivyo, naomba nimwite Mhe. Asha Moh'd Hilal kwa ajili ya kutumalizia muda.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru mimi kupata nafasi hivi sasa kwa ajili ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kufanikisha baadhi ya majengo yake na kuweza kufanyakazi vizuri.

Mchango wangu nianzie na Idara ya Kinga na Elimu ya Afya ukurasa wa 21. Mhe. Spika, kwanza niwapongeze kwa elimu wanayoitoa. Pamoja na hayo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kuwa ajikite zaidi kwenye elimu ya watumiaji wa madawa ya kulevya, kwa sababu hawa ni vyanzo cha matatizo yote.

Kwa mfano, sindano moja wanatumia watu wanne, yaani wanapokezana moja baada ya mwengine na hapa virusi vinaenea. Kwa hivyo, moja kwa moja madawa ya kulevya yanatuenezea virusi vya UKIMWI kwa kutumia sindano, kwa sababu wanaweza kutumia kuanzia wanne hata kumi. Hali hiyo, inapelekea kuenea kwa urahisi maradhi ya UKIMWI kutokanana na madawa ya kulevya.

Vile vile hawa wanaotumia au wanaokula madawa ya kulevya wanatia ufukara pamoja na jamii kwa jumla, kwa sababu mtu kama hajapata madawa basi kwa vyovyote vile lazima aibe na kwenda kuuza kwa bei yoyote, ili apate fedha na kuweza kukidhi haja yake. Hili ni tatizo kubwa Mhe. Spika.

Suala jengine tunakosa vijana wa kufanyakazi, kwani vijana ndio nguvu kazi ya jamii pamoja na taifa kwa jumla, lakini hawawezi kufanyakazi kutokana na *weakness* ambayo wanayo.

Mhe. Spika, jambo jengine inawarudia kazi wao hospitali inabidi watayarishe madawa kwa ajili ya kuwashughulikia hawa watu wakati wanapokuwa hawajiwezi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wajikite zaidi kwa hawa wanatumia madawa ya kulevya kwa lengo la kuwapa elimu, ili waache kutumia haya madawa.

Pamoja na hayo, nampongeza Mhe. Waziri kwa kufanikisha Mradi wa Maliza Malaria Zanzibar na kubakia asilimia ndogo sana, watu kutoka nje na kuja kusoma hapa kwetu jinsi gani tumeyakomesha maradhi haya.

Mhe. Spika, kuna maradhi zaidi ya malaria ambayo yanaua sana kama vile Maradhi ya Sukari, lakini tunapiga kelele hapa yapewe kipaumbele, zaidi amejikita kwenye masuala ya Maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano, maradhi haya ya UKIMWI yanaua watu 1,000, lakini wanaokufa kwa maradhi ya Sukari

zaidi ya 2,000. Kwa hivyo hapa tutaona kama hawafi wagonjwa hawa wa Sukari, kwa sababu maradhi haya ni *silence killer* labda hatushughulikii hizi takwimu.

Lakini atakubaliana na mimi kwamba hawa wagonjwa wa Sukari na *Pressure* wanakufa zaidi kuliko wagonjwa wa UKIMWI. Mhe. Spika, nadhani kuna haja ya kuyapiga vita maradhi haya kama maradhi ya Malaria kwa kuwapa watu elimu au kuna mambo mengine ambayo wanayajua wao wataalamu, ili kuwafundisha kwa lengo la kuyatokomeza kama hayo mengine au yapungue kasi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 33 Kitengo cha Afya. Mhe. Spika, zamani wafanyakazi walikuwa wakipitiwa na kufanyiwa *checking* afya zao, lakini hivi sasa utaratibu huo umekufa na wala haupo kabisa.

Kwa kweli utaratibu wa kufanyiwa *checking* afya zetu ni mzuri, kwa sababu watu wengine wamo kwenye taasisi tofauti. Kwa mfano, walimu, pengine mwalimu anayo maradhi ya kuambukiza lakini hajui na kuendelea na kazi na pale anayo jamii ambayo anaisomesha. Kutokana na hali hiyo, maambukizi yanaweza kufanyika na wanafunzi wakapata maradhi bila ya kujua. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba utaratibu wa kufanyiwa *checking* afya zetu urejee.

Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu wazazi. Kwa kweli Mhe. Waziri sote kila mwenye kusimama hapa tunapiga kelele kuhusu mchango wa wazazi hospitali, kwa sababu dunia nzima hawa watu wanathaminiwa na kuengwa engwa, kwani uzazi ni mgumu na wala sio mchezo. Mhe. Spika, katika kitu kigumu duniani ni uzazi, kwa sababu kuzaa sio mas-hara nadhani atusikilize Mhe. Waziri, kwani sisi ndio tunaozaa na kuona hii shughuli. *(Makofi)*

Kutokana na shughuli hii unakuwa husikii kitu na wala hufahamu, kwa nini hutaki kuiondoa na sisi sote tunapiga kelele kuhusiana na suala hili. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri awe muungwana na kutuondolea suala hili na wala tusibuburushane, kwa sababu kila bajeti na kila mwenye kusimama anazungumzia suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo natoa mfano kwa mara ya pili Malkia wa Uingereza, watoto wote wanaozaliwa kwa sababu anapewa *first priority* mzazi, kutokana na hali ngumu ya uzazi, basi anathamini mzazi pamoja na wengine. Kwa mfano, kwa wenzetu Tanzania Bara mzazi anathaminiwa. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, awe muungwana kwa hisani yake aliondoe hili. *(Kicheko/Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu pia namuomba tena Mhe. Waziri kitu kimoja kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuna madaktari *specialist* ambao wanaingia usiku. Kwa kweli wale ni watu ambao wenye kazi ngumu, ambayo wamepangiwa ya kuangalia pamoja na kuwashughulikia wagonjwa kwa usiku ule. Sambamba na hilo kuna *emergency case* kama vile *an accident* au mtu anaumwa *serious* ameletwa pia azishughulikie.

Lakini wale watu kwa ushahidi kamili mimi mwenyewe si mara moja wala mbili wameshawahi kunisikitikia, wale watu posho lao hawapewi wamefanyakazi kiasi muda wa miezi mitatu na halafu halilingani kabisa na zile kazi zao wanazozifanya.

Suala jengine *Ambulance* ndio usafiri wao. Mhe. Spika, nadhani tufanye kwa makusudi tuwatunze hawa wataalamu wetu wasitukimbie, tuwatafutie usafiri wao pamoja na kulipwa maposho kwa wakati muafaka. Kwa mfano, sisi hata kama tutaeleza humu hao wataalamu, yaani tumesema hapa tutakuwa na mafunzo ya udaktari *Wallahi* watatukimbia wote hatobakia hata mmoja kama walivyokimbia tuliowasomesha nje.

Kwa hivyo, tujaribu kuwaridhisha na kuwalipa yale malipo yanayolingana, kwa sababu hawa watu wanafanyakazi ngumu na sisi wenyewe tunaiona na wao wanaijua, kwani kila wakati wanazunguka. Hivyo, tuwe wepesi kwa hili, yaani tuwalipe posho pamoja na wasaidizi wao, kwa sababu anao wasaidi na wala sio kama anafanyakazi peke yake, anao wasaidizi na sio kama mashine na wanakuwa pamoja na *staffs* wa *shift* ile ya usiku.

Mhe. Spika, ajali nyingi zote anashughulikia mtu mmoja na posho lenye alidai mpaka kijasho kimtoke, kwa ushahidi kamili si mara moja wala mbili, kwa sababu mimi mwenyewe niliwahi kwenda kumchukua daktari kwa ajili ya kuja kumshughulikia mgonjwa pale.

Kwa kweli daktari anachoka sana kwa sababu mpaka alizunguke lile jumba lote, basi amerudi kwake kwa ajili ya kupata riziki ya chakula, nilikwenda kumchukua Mtoni na kuja hospitali na kumnusuru mgonjwa na wala hakufa, kwa sababu tatizo lake ilikuwa chango zake zimepandana na wakati wa kufanyiwa *operation* umeshapita.

Kwa hivyo, hawa tuwajali na tuwape maposho yao wakati wanapomaliza *shift* ama kwa wiki au mwezi, basi tuwape na sio tuwachanganyishie mishahara tukawashughulisha, yaani kuwe na utaratibu mzuri hasa kwamba posho lao na ameingia siku ngapi na kulipwa posho lake. Mhe. Spika, nadhani utaratibu huu unaweza kusaidia na wale ambao tunao wanaweza kudumu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri alishughulikie suala hili kama si hivyo hawa wanne waliobakia watakimbia na hatimaye tubakie na ma-*orderly*, watakufa watu kama nzi au nzige, yaani kila wanapopelekwa watu watakuwa wanakufa, kwa sababu si *specialist* na wala hajui kitu nafikiri atakuwa akiingia na kutoka. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nimshauri Mhe. Waziri kuhusu hawa ma-*orderly* wetu tuwa-*trained* vizuri. Kwa hivyo, wanapokuwa pale wajaribu kutumia lugha nzuri kwa sababu wengine ni waheshimiwa wasiwe wanawajibu ovyo na wengine wanakuwa wanyonge, anapoambiwa kidogo basi anarudi nyuma hawezi kusema kitu, lakini mwengine ambaye yuko ngangari hakubali mpaka mwisho.

Kwa mfano, anaomba namba ya simu ya *doctor* basi anamwambia haipatikani wakati mgonjwa hali yake iko *serious*. Vile vile *season* kama hizi za kutoka na roho, yaani dakika za majeruhi, sasa umnusuru yule mgonjwa na sifa yako iende. Kwa hiyo, kwenye familia nzima kura zako unazo bila ya wasi wasi, sasa yeye anakwambia namba ya simu haipatikani na *doctor* sijui ana hivi na vile na mwengine atakwenda zake, lakini mwengine hakubali. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awafahamishe wale ma-*orderly* pamoja na wahusika wanaokuwepo pale kama ni *staffs*, watakapokuja hawa muwasikilize vizuri, kwa sababu yeye anaijua hali halisi na anaujua umande ulivyo. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Asha Moh'd Hilal, tunakushukuru sana kwa mchango wako huo.

Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa nitoe taarifa ya shughuli kama tunavyoelewa kwamba jana mwenzetu Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin alipata msima wa kufiliwa na mwanawe na kesho tunategemea kuwa na hitima yake yule marehemu, ambayo itafanyika baada ya Sala ya Laasiri katika eneo la Bububu kwa Mdoe, yaani kwenda huko unapita njia ya Mwanyanya ambayo iko Bububu Skuli.

Kwa hivyo, tunaombwa tushiriki katika kisomo hicho cha hitima ya mtoto wetu ambaye alifariki ghafla jana Hospitali ya Mnazimmoja.

Baada ya maelezo hayo, Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano na ninakinaahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumapili tarehe 4 Julai, 2010 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 04/07/2010 saa 3:00 asubuhi)